

**CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION**

**(CKRC)**

**VERBATIM REPORT OF**

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS,**

**KAJIADO SOUTH CONSTITUENCY, HELD AT**

**LOITOKTOK SOCIAL HALL**

**ON**

**WEDNESDAY, 10<sup>TH</sup> JULY 2002**

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, KAJIADO SOUTH CONSTITUENCY HELD AT LOITOKTOK  
SOCIAL HALL ON WEDNESDAY 10<sup>th</sup> JULY 2002**

**PRESENT**

Com. Bishop Bernard Njoroge  
Com. Ibrahim Lethome

**SECRETARIAT STAFF IN-ATTENDANCE**

Joash Aminga - Program officer  
Osogo Ambani - Assistant Program officer  
Alice Thuo - Verbatim recorder

**The meeting was called to order at 9.40 a.m.**

**Com. Bishop Njoroge:** Habari ya asubuhi. Inaonekana kutakuwa na watu wengi leo. Nataka tuanze kwa maombi. Mchungaji unaweza kutuongoza na maombi na ukiomba useme jina lako ili liweze kuingia kwenye record.

**Rev. Simon Kanaiya:** Hamjambo nyote? Mimi kwa majina naitwa Rev. Simon Kanaiya, kanisa la Charismatic Episcopal Church, parokia ya Ngarua Kajiado. Basi, natuombe.

**Maombi**

Baba Mungu tunakushukuru, tuna jambo la kukuinua asubuhi hii. Asubuhi njema katika maisha ya kila mmoja wetu. Tunakushukuru kwa ajili ya uhai, kipawa cha ajabu umetupatia. Ambayo ndio imetuwezesha kuja hapa katika umoja, katika nia moja, katika lengo moja, katika upendo mmoja. Kwa ajili ya taifa hili ambalo Mungu unalipenda sana, taifa la Kenya. Nakushukuru, naomba kwamba Mungu katika shughuli ya leo ambayo Mungu umetukusanya hapa ili tuweze kufikiri katika hekima na ufahamu wa Mungu, katika kutayarisha na kufikiri ili Mungu utupatie mawazo yetu katika kutengeza Katiba kwa ajili ya taifa hili. Utupe hekima, utupe ufahamu, utupe maarifa, utupe upendo kwa ajili ya taifa hili na ni katika jina la Yesu, tunaomba na kushukuru. Amina.

**Com. Bishop Njoroge:** Jina langu naitwa Commissioner Bishop Bernard Njoroge na ningetaka kuwajulisha wale tulio nao hapa. Tuna Commissioner Ibrahim Lethome, ambaye ameketi hapa, nitampatia mic. awasalimie.

**Com. Lethome:** Watu wa Loitoktok hamjambo? Asanteni.

**Com. Bishop Njoroge:** Tuna ma-officer kutoka kwa Tume, tuna program officer ambaye atatujulisha wafanyikazi wengine aliokuja na wao.

**Joash Aminga:** Habari zenu? Kwa majina mimi naitwa Joash Aminga, mimi ndio program officer, tuna verbatim recorder ambaye atakuwa akinasa sauti ya yale maneno mtakayoongea, anaitwa Alice Thuo. Pia kuna Osogo Ambani, ambaye anaandika yale yote mnayoyanena! Asante.

**Com. Bishop Njoroge:** Pia tuna District Co-ordinator ambaye atakuwa akifanya kazi katika district hii ya Kajiado na ningetaka aje hapa mbele aseme kama kuna members wa committee wake, atujulishe kwao kwa dakika moja. Karibu Co-ordinator.

**Ben Ole Mulei:** Mimi kwa majina naitwa Ben Ole Mulei na tumekuwa pamoja na nyinyi wote, karibu. Nafikiri wote tunajua. Na nasema karibuni sana. Leo ndio ile siku tulikuwa tunangojea. Pamoja na mimi, nimekuwa na msaada kutoka kwa wenzangu ambao wametoka katika committee hii ya kushughulikia mambo ya kufundisha watu juu ya Katiba. Niko na Chairman wetu wa CCC, wa Kajiado South Constituency naye ni Councillor Jacob Lesingo, yuko hapa. Tuko na Bwana Daniel Somoiyee. Yuko hapa. Wenzetu, kwa sababu ya wingi wa kazi, tuligawana. Wengine tulikuwa Kimana jana, tulikuwa Rombo wengine kwa sababu ya haya matayarisho tu na nimeshukuru. Mmeitikia kuitwa na ninahakikishia Ma-Commissioners wangu kwamba bado watu wanakuja. Watakuja. Na kwa hayo machache, singependa kupoteza muda, ningerudisha tu kwa Commissioners waendeleo na kazi yetu.

**Com. Bishop Njoroge:** Kila mahali tumeenda, tukija hapa - tumetoka Turkana, Pokot, Marakwet - tumefurahia ile huduma Provincial Administration wamefanya kwa ajili ya kazi hii. Kama Lodwar tulikaa siku nzima na wamekuwa na msaada kwetu sana. Wakati tulipokuja hapa jana, tulikuwa na D.O wa Loitoktok ambaye ametuhudumia vizuri na tumeshukuru. Kwa hivyo ningempatia D.O. atukaribishe rasmi ili tuweze kuendelea na mkutano wetu.

**Malim Mohammed:** Commissioner Njoroge, Commissioner Ibrahim Lethome, Co-ordinator wa CKRC, Bwana Mulei, Program Officer ambaye ako hapa na wenzake wengine: Mwenyekiti wa KANU, viongozi na madiwani, Ma-Chifu na wananchi kwa jumla hamjambo? Basi, nafikiri kwanza ni kushukuru Mwenyezi Mungu kwa sababu ni siku nafikiri tulikuwa tukingojea kwa muda, na wengi wangelipenda labda kuja kupeana maoni yao kwa ajili ya hii Katiba, lakini hawako na sisi leo. Kwa hivyo wale tuko hai, inafaa tushukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika siku ya leo. Ni bahati kubwa sisi Wanakenya baada ya uhuru kupewa fursa ya kuja kuongea mambo ya Katiba ya nchi yetu. Kwanza kabisa nachukua hii nafasi kuwakaribisha Commissioners wa Tume ya kurekebisha Katiba, Bwana Njoroge, Bwana Ibrahim Lethome na maofisa walioandamana na hawa katika sehemu ya wilaya ndogo ya Loitoktok.

Watu wa Loitoktok, wanawakaribisha kwa moyo dhati kwa sababu haya mambo ya Katiba ni mambo ya maisha ya Wakenya. Ama sivyo? Kwa hivyo nafurahia. Jana tulikuwa Rombo na kusema ukweli Wamaasai watu wanasema hawajasoma, lakini yale mawazo walipeana nina uhakika hata wale wameenda University hawataweza. Na hiyo ni kwa sababu ya uongozi bora tukiwa na Mheshimiwa, tukiwa na madiwani, tukiwa na wafanyikazi wa Serikali, viongozi wa dini, viongozi wa chama. Tumesema watu wajulishwe katika kila sehemu kuja kupeana maoni yao kwa mambo ya Katiba. Kwa hivyo nafikiri wale Wamaasai tulikuwa tunasema labda maoni yao itakuwa ni kasoro kwa sababu hawana masomo, lakini yale wamepeana, tunataka watu wa Loitoktok, hata mvuje record zaidi. Kwa sababu wasomi si wako hapa?

Wale wasomi tunajivunia katika hii sehemu, si mko hapa? Kwa hivyo tunataka mpeane maoni yenu na mimi niko hapa kukaribisha hao wageni. Baada ya kuwakaribisha nitakuwa raia mwema kama nyinyi. Msinihesabu kama D.O. Kwa sababu ni lazima nije nisikize mambo ya Katiba. Leo niko D.O., kesho nitakuwa raia mwema kama nyinyi. Kwa hivyo ni kitu inahusu maisha yetu. Kwa hivyo Bwana Commissioner, kwa sababu muda nao ni kidogo na watu ni wengi, na bado watakuja wengi. Nasema karibuni Loitoktok na tunashukuru kwa nyinyi kufika, asanteni.

**Com. Bishop Njoroge:** Asante Bwana D.O. Sasa mimi nataka kuwaambia vile tutaendelea. Kwanza nataka kutangaza kikao hiki kama kikao rasmi ya Katiba na tunapoketi hapa tujue tuna sheria ile inayo tusimamia kwa yale mambo ambayo tutafanya hivi leo. Jambo la kwanza, kila mtu atakuwa huru kusema maneno ambayo anafikiria inaweza kusaidia katika kuunda Katiba. Kama mjuavyo, Katiba hii ni watu wenyewe waseme wanataka iwe namna gani. Kwa hivyo msiogope kwamba D.O. yuko hapa. Hata wakati tuna P.C au Mawaziri wa Serikali, wanajua kwamba watu ni lazima wawe huru kusema yale wanayohitaji kusema. Hakuna mtu anaweza kufuatwa kwa sababu ya yale aliyoyasema leo. Ile Act ambayo inatutawala inasema, kila mtu ana uhuru. Lakini ningetaka kusema hivi; hakuna mtu ana uhuru kuzungumza juu ya mtu binafsi kwa njia yeyote mbaya ama njema. Kwa sababu ni Katiba tunafanya nini? Tunatengeneza. Ninataka kutoa mfano. Mtu anaweza kusema, tunataka mamlaka ya Rais ipunguzwe. Haya ni mapendekezo, inafaa. Lakini huwezi kusema juu ya mtu katika Serikali kwa njia yeyote mbaya kwa sababu hiyo haitaenda katika Katiba. Tumekubaliana hivyo? Na mtu akisema hivyo, nitamkataza kuendelea kwa sababu ni lazima tuwe na mapendekezo ambayo yataingia kwa Katiba. Unaweza kuwa na Mbunge na huna furaha naye, huna ruhusa kusema juu ya Mbunge. Unaweza kusema tunahitaji barabara. Sawasawa? Hayo ni mambo ya Kikatiba. Kwa hivyo hata kama tuna uhuru, hatuna uhuru wa kusema mabaya ya watu. Si hapo tumekubaliana?

Jambo la pili, sisi ni Wakenya, tunajua kuna shida nyingi. Tunajua kuna watu wengi hawana pesa ya kwenda kununua madawa. Tunajua mara ingine kwa mahospitali hakuna madawa. Kwa hivyo usitumbie zile shida kwa urefu, tuambie mapendekezo yako ni nini, ili tutatue shida gani? Shida hiyo. Tukifanya hivyo, tutatumia muda mfupi na yale ambayo unasema, itasaidia kutengeneza Katiba hii. Kwa hivyo tunataka mapendekezo. Kama jana, kama vile D.O. alivyosema na Councillor pia alisema vizuri huko Rombo kwamba tunahitaji tu mapendekezo. Kwa sababu hiyo ndio itaenda kwa Katiba.

Jambo la tatu, mjue ya kwamba hii exercise ni muhimu. Tuna Program Officer pale, kazi yake ni kuchukua zile memorandum. Kazi yake ni kuwa na kitabu ile ameandika kila moja ambaye atazungunza hapa. Tukipata hizo memorandum, ofisi yetu Nairobi, tuna watu zaidi ya arobaini na kazi zao, ni memorandum hizi zikifika Nairobi, kama leo tunatoka kesho kuelekea Nairobi, tukimaliza Kimana. Hizo memorandum, zinaachwa ofisi. Ili hawa watu arobaini waanze kuzifanyia kazi na kuchukua mapendekezo kutoka katika memorandum hizi. Na hizo memorandum zinaingizwa katika ma-computer.

Kila pendekezo inaingia mahali pake na mtu aliyetoa pendekezo hilo. Mengine inakaa ofisini mwetu, mengine inapelekwa national archives, mengine inafichwa mahali pengine. Kwa sababu haya ni mambo ya maana. Kwa hivyo msijali kama mkisikia nikisema, huna haja kusema mambo yote, hakuna mambo yako itapotea. Kuna mahali itaenda. Mnaona huyu msichana. Chukua hako kadunde juu. Tuna kadunde kale ambapo tuna-tape maneno yote mnasema. Na pia tuna watu wengi huko ofisini, kazi yao ni kuchukua haya maneno ni kuchukua haya maneno na ku-type katika computer na kutoa kama walaka. Mkifanya kelele, kelele ndio zitachukuliwa na hii record na hiyo si mzuri. Tafadhali tusifanye kelele na mtu akija kutoa wazo lake hapa, na usikie hupendi vile anasema, don't shout him down. Those are his views. Wewe ngojea wakati wako, uje useme maneno yako. Tafadhali tufanye haya mambo kwa heshima kwa sababu huu ni wakati muhimu katika nchi hii. Katika kuongoza hali hii, tunaenda kwa vile list ilivyoandikwa.

Hatutaki watu wengine kupita wengine kwa sababu huu ndio mwongozo wetu. Lakini tuna mtu kama D.O., tuna mama kama mja mzito, akija hapa hatuwezi kumuweka sana. Tuna mtu disabled ambaye hawezi kukaa kwa muda mrefu. Huwa tunakubali ili waweze kutoa nini? Kutoa maoni. Mbunge wenu anaweza kuja hapa, ni lazima akae karibu one hour. Lakini tunampatia nafasi kwa sababu unajua siku hizi hata kama haupendi mtu, lakini ndiye kiongozi wenu. Si ni kweli? Tusidharau uongozi. Wakati ukifika kama haupendi utamuondoa lakini wakati ako, unamheshimu kwa ajili ya cheo chake. Kwa hivyo tutaendelea hivyo.

Ukiitwa, utakuja ukae kwa kiti kile. Nitakupatia five minutes, dakika tano. Ninajua mtasema ni chache. Wacheni niwaambie, tumekwenda Mombasa, tumekwenda North Eastern Province, tumekwenda Central, Eastern, kwa hivyo tunajua tuna ujuzi wa kazi hii. Tunajua dakika tano ni dakika mingi sana kwa mapendekezo. Lakini tukiona kuna kitu umebakiza, we are not too strict. Tunaweza kuongeza moja, mbili, au tatu. Sawasawa? Ili kila mtu aweze kuongea. Sasa nataka tuanze na Mr. Francis Ole Legis. Unaweza kutumia lugha yeyote. Ukiwa wewe ni MuMaasai na hujui Kiswahili, unakubaliwa kutumia lugha ya KiMaasai na mtu mwingine atafsiri.

**Francis Ole Legis:** Kwanza sijui...Honorable Commissioners, hiyo itakuwa address mzuri? Sasa langu kwa sababu ya time factor na dakika tano naona kama ni kidogo lakini mmekwisha pata experience. Maoni yangu itakuwa hasa juu ya ile historia ya Wamaasai. Jina langu ni Francis Ole Legis. Na yale nitakayoyasema, mtanisamehe. Mimi kwa kuzaliwa kwangu, I am a nationalist lakini mambo mengi nitakayozungunza hapa yatalenga hasa zaidi ya Wa-Maasai. Na ninataka kuanza kwa historia ya Wa-Maasai kidogo.

Historia ya Wa-maasai - they extended from L. Rudolf to L. Manyala in Tanzania na katika ile treaty ya Wazungu ya 1904, 1911, Wamaasai nchi yao ilichukuliwa kiasi ya seventy percent. Hapo ikafuatwa na kitu kingine baada ya kupata uhuru ambayo inaitwa Land Adjudication Act. Katika nchi hizi zote mbili, zimechukua sehemu ya nchi ya Wa-maasai. Ile ya British Agreement ya 1904-1911 ilichukua seventy percent of the Maasailand na hii Land Adjudication Committee ilifungua njia ya nchi ya Wamaasai kuchukuliwa na watu wa nje. Na hapo utaona kwamba ilikuwa ni kitu ya ajabu kufanya hii Land Adjudication Act na ikafuatwa na Land Control Board ambayo mimi nimekuja kuiona kwamba si Land Control Board, ilikuwa kama Land Disposal Board. Kwa sababu kutokana na hiyo, watu wengi kutoka nje walikuja wakaingilia nchi ya Wa-Maasai katika all the highland and all arable land, ile pahali ambayo inaweza kulimwa na inaweza kutumiwa kwa njia kama hizo. Hasa upande wa Loitoktok na Ngong na imekwenda hasa Loitoktok na upande wa Ngong. Imekwenda kama fifty percent. Hasa kwa upande wa Loitoktok, imeumiza Wa-Maasai sana maana upande wa msituni huku, kama wakati wa njaa. Ng'ombe walipata njaa na ng'ombe ndiyo maisha yao. Walikuwa wanahama upande wa juu kutafuta nyasi kwa sababu huko hakukuwa kumekauka kama vile kulikauka upande wa chini. Sasa wamesukumwa kwa sababu ya culture na sababu ya kununuliwa nchi, wamekwenda mpaka huko chini ambapo jua ikitoka kidogo kunakauka na ng'ombe wanakufa. Hapa karibuni mimi naona kama Wamaasai watakosa kitu na watakuwa bado maskini kuliko watu wengine katika Kenya nzima.

Ya pili, ningalitaka mambo ya kuuza nchi. Serikali isaidie Wamaasai na namna ya kuuza nchi, isiwe nchi inakuwa katika ile hali ya kuwa kila mtu anaweza kuja ku-buy land katika Kenya na uko namna hii. Wamaasai wasaidiwe kwa kutengeneza land buying committee ambayo wao wenyewe ndio watasimamia. Halafu watakuwa kwa hiyo committee. Itafanya kazi ya kununua shamba kwa yule mtu anayetaka kuuza na hiyo committee ya Wa-Maasai watajua watauzia akina nani. Hapana kila mtu, kutoka North, South, anakuja anachukua ardhi ya hapa.

Nyuma yake, Wamaasai wanabaki. Wamekwisha sukumwa wamekwenda katika the most arid land na ardhi yote imeisha kwenda kwa wale watu ambao ni werevu. Ni kama vile vile Wazungu walivyowasukuma kutoka huko. Wanasema in agreement, can you imagine? A century ago, a century ago, Wamaasai - watu ambao wamekwisha kwenda kwa ndege, wanakuja kufanya agreement - it was a mockery na watu ambao katika wakati huo, hiyo century hakuna mtu mmoja hata alikuwa anajua ABCD ni nini katika Kenya nzima, let alone the Maasai. Kwa hivyo mimi nataka Wamaasai wakae hivyo.

Katika sheria, nasema powers zote zisiwe invested ndani ya mtu mmoja. Kuwe na institution ya President and Prime Minister. Kuwe Prime Minister anaweza kuwa ni mtu ambaye ndiye anaendesha day to day work of the Government. President atakuwa ni mtu anaachwa kubaki hapo halafu awe ndio anatia break kama mambo yanakwenda nini... kuwa na mtu mmoja tu ambaye ndiye mkubwa wa kila kitu, nafikiri it is not democracy. Sasa katika upande wa Administration, kwa maoni yangu nataka Provincial Administration ibaki kama ilivyo. Iwe the go between the police and the courts. Maana ikiwa sasa raia watakuwa na authority ni mbili tu ya kuendea, ni polisi na korti, itakuwa ni ngumu kwa watu wengine. The Provincial Administration should remain so that it can be the go-between the police and the courts.

Imebaki ngapi hapo?

**Com. Bishop Njoroge:** Nakupatia dakika mbili.

**Francis Ole Legis:** Ama hutaki hilo swali Honourable Commissioner? Sasa - na kweli nimesoma, karibu nimalize. Kwa hivyo - nilikuwa nimesema nimetanguliza hiyo - kusema yale mambo ya nchi. Kama tunavyojua Wamaasai wafikiwiwe maana bado wako nyuma. Let us know, kama tukiendelea kuachwa kama vile walivyo, there is a fear - to avoid vitu mbili. The Maasai being sub-merged by other tribes. Kitu ya pili, a situation like that in Namibia - although not by the Government but by the people. Also, that which we nearly saw happening in Narok and Subukia. To do that, this is why I suggested, we should have a land buying committees owned and led by the Maasai and they will know who to sell to and who not. Kwa hivyo Bwana Commissioner nimemaliza.

**Com. Bishop Njoroge:** Utakwenda pale na memorandum yako. Umeona sasa umezungumza mambo ya maana. Tupate Rev. E. Ole Ntoipo.

**Rev. Elias Ntoipo:** Mimi kwa maoni yangu katika Constitution - jina langu ni Rev. Elias Ntoipo. Nitazungumzia mambo machache juu juu kwa sababu kuna memorandum hapa ambayo nitapeana. Nitazungumzia juu ya ardhi. Ardhi na rasilmali katika nchi ya Wamaasai. Ni kwamba Constitution ama Katiba hii ambayo tunaiandika, iweze kuulinda nchi ya pastoralists. Wamaasai wakiwa sehemu moja ya pastoralists. Kwa sababu watu wanapona sehemu zile za nyanda za chini, wanasema hakuna watu. Wanasema hakuna kilimo na tukianza sote mambo ya kilimo, basi ya watu wengine kama Wamaasai inaharibika. Kwa hivyo katika land, land ya Wamaasai iwe protected. Kusiwe tena na Land Control Board, kuwe katika Constitution, Customary Land Control Board ili Wamaasai waweze kugawa nchi yao.

Kwa sababu kwa wakati huu, ni kama Land Adjudication iliyofanyika ilikuwa njia ya kunyang'anya Wamaasai nchi. Pia na agreement zilizotelewa 1914-1911, haikuwa agreement kwa sababu, Lenana hakuwa kiongozi wa Wamaasai, so the question is this: Isipokuwa Lenana nani alikuwa hapo? Hakuna aliyekuwa hapo. Kwa hivyo hakukuwako na agreement yeyote kati ya Wamaasai na British. Jambo lingine ni kwamba sehemu ya Nakuru, Laikipia, sehemu ambayo bado haijakaliwa ambayo bado Wazungu wanakalia, ni heri irudishiwe Wamaasai maana ni nchi yao. Amboseli iwe chini ya Wamaasai, a part of Tsavo West na Chyulu hills ambayo ilichukuliwa na National Park. Hizo resources zote ziweze kurudishwa kwa Wamaasai ili waweze kufuata kwa ajili ya kazi zao.

Nikija kwa upande wa education: Education pia ni kwamba tumekuwa watu ambao wamekuwa neglected sana. Hakuna regime ambayo imezangatia elimu ya pastoralists. Economy haijazingatia, zile ziko hazijazingatia na kwa hivyo tunataka quota system katika University, vile vile Pastoralists. Na University ijengwe katika nchi ya pastoralists ili kuweka wao motisha ya kwamba kuna elimu baada ya Secondary. Hiyo nayo tunahitaji Constitution iweke kwamba elimu ya pastoralists izingatiwe na kulindwa ili

iveze kufaidi wao.

Katika Culture, Constitution hii ambayo tunaiandika, tunaomba kwamba culture ya Wamaasai iwe-protected, ilindwe kwa sababu ni yao. Sasa imekuwa unakuta watu hapa ambao si Wamaasai, wanafaa KiMaasai, wanaenda Ulaya, wanajifanya Wamaasai maana wale hawajui na wapata mapato kwa kutumia culture ya watu wengine. Kwa hivyo hiyo nayo culture iwe protected. Kila culture iwe right ya wale watu kuitumia lakini sio watu wengine kuitumia.

Nikija kwa upande wa governance, maoni yangu ni kwamba tuwe na Serikali ya Majimbo. Kama vile ilivyokuwa hapo mwanzo. Kwa sababu Serikali ya Majimbo itakuwa na watu kuweza kukaa pamoja kwa sababu italinda masilahi so closely kwa community kuliko wakati sasa inapozambaza. Kwa hivyo mimi naomba kwamba katika Katiba hii, tuzingatie Serikali ya Majimbo ambayo itakuwa na Regional Assembly, itakuwa na House of Representative. Itakuwa na Executive President, itakuwa na Prime Minister, itakuwa na Vice President na mamlaka vile vile.

Tusiweke mamlaka yote kwa mtu mmoja hata awe Rais wa nchi. Isiwe hivyo. Mamlaka igawe ya korti, ya Executive isi-intefere na korti, Legislature, isi-intefere na Executive. Kila sehemu isiamame sawasawa ili nchi iveze kutawaliwa vizuri. Kwa hivyo katika hayo tunayozungumzia ni kwamba ningependa vile vile kuzungumzia juu ya resources. Nikisema resources yote, hiyo ni pamoja na mineral, ile iliyo katika nchi yetu, iwe inafaidi na vile vile kufaidi ile nchi. Maana kama tutapata Regional Government basi itakuwa, kwa sababu ninaposema Regional Government, tumeona nchi ambazo zililazimishwa kukaa moja. Kama nchi ya former Yugoslavia. Unajua ya kwamba ilikuwa nchi moja lakini kwa sababu haikuwa mapenzi ya watu kukaa hivyo, baadaye tuliona matokeo yake. Hatukai katika nchi hii. Tunataka watu wakae katika sehemu zao bila kuingiliana while at the same time tuko katika nchi moja ambayo tuko chini ya Rais mmoja. Basi mimi kwa haya, nashukuru kwa kunisikiliza.

**Com. Bishop Njoroge:** Kuna swali.

**Com. Lethome:** Reverend, umependekeza Serikali ya Majimbo. Tungependa utueleze, haya majimbo ungeyapenda katika ngazi gani, ni ngazi ya wilaya au ngazi ya mkoa. Pili, unasema watu wakae katika sehemu zao. Hebu fafania unakusudia nini? Una maana kuwa kama ni Wamaasai wakae kwao, asiyekuwa wao, aondoke ama vipi?

**Rev. Elias Ntoipo:** Sisemi hivyo. Nasema hivi: Kama kwa mfano, ile napendekeza ni kwamba, hata Rift Valley igawe mara tatu.

**Com. Lethome:** Majimbo iwe katika kiwango ya Mkoa?

**Rev. Elias Ntoipo:** Kwa hivyo si kwamba iwe ya kikabila. Lakini wale watu wanakaa katika region hiyo, hayo makabila ambayo yanakaa katika mkoa fulani. Nataka kusema hivi, tuwe na Local Authority. Tuko na Authority ambayo itakuwa katika



Constitution. Ambayo katika district, itakuwa tu wakati kura inafanywa elections. Tuwe na Local Authority, kutoka Local Authority tuwe na Regional Authority.

**Com. Lethome:** Hiyo Regional Authority itakuwa katika ngazi gani?

**Rev. Elias Ntoipo:** Unamaanisha nini unaposema ngazi gani?

**Com. Lethome:** Will it be at the Provincial level?

**Rev. Elias Ntoipo:** Yes. It will be at the Provincial level.

**Com. Lethome:** Majimbo will be a Province?

**Rev. Elias Ntoipo:** It will be a Province. Ndio. Kama Rift nasema kwamba, igawe mara tatu, iwe North, iwe South, na Central. Hiyo ndio namaanisha. Kwamba ni region, sio katika kikabila. Aah ah - katika wale watu ambao wanakaa katika sehemu fulani ya given area.

**Com. Bishop Njoroge:** Asante kwa maoni hayo. Palashina Ole Sunkuri.

**Palashina Ole Sunkuri:** Mimi kwa majina ni Palashina Ole Sunkuri. Maoni yangu ni kwamba wakati mzungumzaji alipozungumzia mambo ya nchi kukuja kugawanywa kama sehemu ya Loitoktok hii. Ilikuwa iko kiwango ambayo wale wataalamu wa zamani walikuwa wanatuweka. Anasema kila mtu ni elfu moja. Lakini wakati huu, sijui vile ilifanyika mpaka wengine wanapata elfu tatu kwa kazi na wengine wako na zaidi ya elfu tatu. Nikaona hapo ni kama wagawaji ardhi wananyanyasa wengine. Tunataka kila kitu kiwe sawa.

Kwa sababu kuna watu ambao hawana uwezo na wanaweza kunyanyaswa na wale ambao wako na uwezo. Sasa, kuja hapo tena kuweka ile tunaita Land Control Board, imemaliza watu kabisa. Ziko familia ambazo saa hii, hakuna hope hata ya acre moja. Kwa sababu ile kitu inatendeka hapo, tunakuta familia ni Mzee anaenda kuuza shamba, watoto hawajui, mama hajui, ni karatasi tu tunapelekea Mzee, aambiwe katika hiyo land ambayo alikuwa anaishi. Hiyo tumeona hapo, ni wanyanyasaji wakubwa kwa sababu hawa wananchi wenyewe wapewe ardhi yao. Waangaliliwe ardhi yao vile wanakaa. Kwa sababu mambo mengine unaona kama Commissioner wa Land huko Kajiado, hata huyu anaishi Kajiado, hana pesa ya kwenda huko kulalamika. Wanakimbia hapa hapa tu, kuzunguka kama chura akiwa ndani ya maji na hakuna kitu mtu anaweza kufanya. Sasa ardhi inaenda namna hiyo. Sehemu moja.

Ya pili, tuko na mila, ambayo saa ingine tunakuwa kama Uongozi.

**Com. Lethome:** Mzee, mambo ya land unapendekeza nini? Unajua umeeleza matatizo.....

**Palashina Ole Sunkuri:** Tunapendekeza kwamba, mambo ya ardhi irudi kwa wenyewe wale wanaohusika. Basi nikitoka hapo, naingia mambo ya elimu. Elimu kweli inatakiwa watu wote wasome, lakini katika sehemu hii, elimu sio sawa. Kwa sababu walimu ni haba, hakuna mashule zingine, hakuna walimu wa kutosha na hata kukuta walimu wa Serikali ni watu sita au watatu tu ambao wako katika shule. Sasa unaona ile elimu katika pande za huko chini, inaenda chini sana kwa sababu walimu hawako. Ni lazima walimu wagawe sawa. Kila shule ipate Mwalimu mmoja ili elimu iwe sawasawa kabisa.

Kwa upande wa uongozi, tuna pahali tunaita Local Government. Tunachagua Ma-Councillors hapa, lakini kuna uchaguzi mwingine ambao wanaenda kuchagua Chairman. Ni haki wananchi wachague Chairman kwa sababu saa ingine, hivyo ndivyo ardhi inaingia kwa yule kiongozi wao. Ndio anamaliza sisi kufa. Wananchi wanatoka kuja leta mzozo kwa sababu mtu mwingine anaingia kwa ardhi yako. Kwa sababu ardhi yao imegawa na wengine. Unapata inamalizwa bure na wananchi wale wengine wako hapa hawana ardhi na ardhi ni yao. Ni vizuri, Councillor, Chairmen watoke kwa raia. Ili raia ajue amechagua nani kwenda kumsimamia.

Ya tatu tulikuwa tunasema mamlaka pengine ya Rais. Mimi napendekeza Rais, asiwe Mbunge. Awe ni mtu ambaye anachaguliwa katika Council kwa sababu Rais ni mtu wa kusimamia watu wote wa nchi. Asiwe ni mtu ambaye anasemekana ametoka Kajiado, na anasimamia Kenya nzima.

Finally nikija kumalizia, upande wa uongozi kama Ma-Chiefs - Chiefs saa ingine wengine wanasema Chiefs hana kazi, lakini Chief huwa na kazi. Kwa sababu hata saa ingine mama akigombana na mzee, watoto, nini - hata wengine wanaweza kusuluhisha mambo ya barabara hii - Hizi kesi haziwezi kwenda kortini, anamaliza mambo kama hlo.

Jambo la mwisho kabisa ni kwamba, nataka kuanalia mambo ya kortini. Saa ingine, kuna watu ambao hawajui Kiswahili, tunaye mkalimani. Naye huyo mkalimani hawezi kusema yale maneno mtu alikuwa anasema. Yule ambaye yeye hajui hiyo lugha.

**Com. Bishop Njoroge:** Ngoja kidogo hiyo gari ipite. Kwa sababu hiyo kelele inaweza kumaliza maoni yako.

**Palashina Ole Sunkuri:** Nilikuwa nasema mambo ya mkalimani katika korti. Unaweza kusikia mkalimani anatoa maneno yake yale ambayo yanatoa yale maneno tofauti na yale mtu anasema na anapoteza yale mambo muhimu ya yule mtu. Kwa sababu yule mtu mwingine hajasoma. Napendekeza kama ingewezekana kila korti ziwe zikitumia lugha zetu. Ili wale watu ambao hawajui Kiswahili waweze kusikia vile huyu anasema, na yeye vile vile anasikia mwingine anavyosema. Kwa sababu saa ingine inaweza kuwa hapo, inaweza kuleta tatizo.

Ya mwisho, tuko na mambo ya ndovu. Wale wanyama wa pori, wanaua watu. Mtu akiua ndovu, idara ile ya Serikali inaingia ile area na kubeba mtu sijui na nini. Lakini mtu akiuliwa na wanyama wa pori, huo utaratibu unaenda pole pole mpaka miaka kumi. Na malipo ni kidogo. Mtu anaweza kulipwa elfu thelathini. Sasa si mtu ako na thamana\* kuliko mnyama wa pori. Ni vizuri kuandikwe, ile mtu ambayo mtu anastahili kulipwa.

**Com. Bishop Njoroge:** Pesa ngapi?

**Palashina Ole Sunkuri:** Hata kama ni milioni mbili.

**Clapping from the audience.**

**Palashina Ole Sunkuri:** Maana imeua mtu. Unajua maisha ya mtu kulipa. Saa ingine hauwezi kulipa mtu, nikuambie ulipe huyo mtu maanake ako na thamana\* yake. Kwa hivyo kwa mazungumzo yangu, ninafikishia hapo. Ninasema asante. Asante kwa maneno hayo mazuri.

**Com. Bishop Njoroge:** Philip Leshinka. Hatutaki kusikia watu wakifanya makelele. Ikiwa kuna mtu anataka kuzungumza na mwingine, anahitaji kutoka nje, akimaliza mazungumzo, anarudi ndani ya nyumba. Kikao hiki ni kikao maalum, let us give this place the dignity it requires.

**Philip Leshinka:** Asante, kwa jina naitwa Philip Leshinka na maoni yangu ni kama yafuatayo. Kwanza tunaanza na MP, mwakilishi wa area. Utakuta ya kwamba MP akichaguliwa, kuna wengine ambao hawezi kabisa ku-deliver. Kwa hivyo ingalikuwa ni vizuri, wananchi wapatiwe mamlaka tena wamuondoe mbali na election ifanywe afresh. Pia kabla MP hajachaguliwa, ingalikuwa ni vizuri sana, yule MP angaliweza kukaguliwa aeleweke ni mtu wa aina gani. Ni mtu mfidadi ama ni mtu ambaye ni kamili. Ili asiingie katika Bunge na kuanza kutumia yale mamlaka, either kujitajirisha ama kufanya mambo mengine ambayo hayapendezi wananchi. Kwa sababu tunamweka pale kama mwakilishi wetu, aweze kuendeleza masilahi yetu.

Jambo la pili ambalo nachangia ni juu ya President. President awe ni President aliye na mamlaka ili aweze kuendeleza nchi. Na kabla ya awe President, akaguliwe ajulikane ya kwamba ni mtu ambaye kweli anaweza kuendeleza wananchi, ana experience. Si mtu tu ambaye atakuja kuleta mambo hata pengine hawezi kujua ataendeleza wananchi namna gani.

Pia President asichaguliwe kama MP. Awe amechaguliwa kama President wa nchi kwa sababu akichaguliwa kama MP, an elected MP, kwanza ataangalia masilahi ya area yake. Na kwa hivyo ni vizuri awe sio sitting MP. Pia, President akiwa na mamlaka na mamlaka hayo ayatumie vibaya, sisi wananchi ndio tulio mli-elect, na kwa hivyo mamlaka yetu wananchi

itarudishwa kwetu tukiona ya kwama yeye hafai. Na kwa hivyo tutarudishiwa na wananchi watapewa maoni yao. Wakishatoa yale maoni, yale maoni ndio yatapelekewa wale Ma-MP na vote of no confidence ambayo itakuwa ni fifty five percent. Ikipitishwa basi yule President anatoka na tuna-elect another President.

Huduma za lazima: Huduma za lazima ni kama elimu, health na kadhalika. Sasa katika huduma za lazima, kwanza katika elimu. Elimu ni muhimu katika nchi na kwa hivyo, lazima elimu iendelezwe na wale ambao ni professional. Sio mtu tu ambaye hawezi kuendeleza elimu. Wanasiasa wameachiwa mamlaka mengi sana katika kuendeleza elimu. Kwa mfano tukichukua 8-4-4, ilikuwa ni elimu mzuri lakini kwa sababu wanasiasa waliingilia, wa leo utakuta kwamba inaonekana ni kama sio chombo ambacho kilikuwa ni cha muhimu. Na ingali ilikuwako ni kumsaidia yule mtoto, akitoka nje iweze kumsaidia katika pande mbalimbali. Kwa hivyo maoni yangu ni kwamba professionals waachiwe ku-draw the curriculum na waachiwe pia kuendeleza katika elimu. Pia health hivyo hivyo.

Biashara zimewekwa vikwazo vingi sana. Lazima uwe na licence, pia kodi ziko nyingi nyingi na hizo kodi utakuta ya kwamba yule, kama ni kijana ama ni mzee ambaye amekuwa retrenched or so, hawezi akaendeleza ile biashara kwa sababu ile kodi iliyoko ni nyingi sana. Kwa hivyo kodi iondolewe katika pande za biashara na hata ikiwa ni katika mambo ya kutoa vitu hivi, kama ni biashara kidogo kidogo, mama anakwenda jikoni kununua vitu vidogo vidogo, hizo biashara zimewekwa kodi ya aina yeyote, ziondolewe.

**Com. Bishop Njoroge:** Bwana Philip, umetumia dakika kumi, nakupatia dakika moja.

**Philip Leshinka:** Sasa tunaanza mashamba. Mashamba wakulima wapatiwe mbegu kwa sababu ukulima ni uti wa mgongo katika nchi hii. Wapatiwe mbegu na chemicals za kuweza kuondoa wadudu na kadhalika. Pia soko wakulima wapatiwe.

Halafu jambo la mwisho ni juu ya mazingira. Mazingira ni jambo la muhimu zaidi na ni lazima kila mtu ahimiziwe kuweka mazingira safi. Kama ni mambo ya ukataji wa miti, ukataliwe mbali, kama ni mambo ya kwenda kulima kando kando ya miti, ukataliwe mbali. Kama ni mambo ya kuenda kukata miti, pahali ambapo vianzo vya maji zipo, ukataliwe mbali. Na ni hayo tu.

**Com. Bishop Njoroge:** Tupate Bernard Kamau.

**Bernard Kamau:** Asante sana kwa kunipa muda wa kusema. Kitu cha kwanza, pesa ya Serikali inatakiwa itoke kwa Bunge. La pili, jina ukabila lipigwe marufuku hata ikiwa ni kwa mkutano. Ya tatu, tunatakiwa tuwe tukiuliza maswali kwa mkutano. Ya nne, Kenya inatakiwa kuwe na vyama vitatu. Ya tano, Mbunge angetoka chama hiki, aende chama kingine, kusifanywe uchaguzi tena, kukae namna hiyo. Yangu ni hayo.

**Com. Lethome:** Neno ukabila umesema liwe katika mkutano? Hebu fafanue.

**Bernard Kamau:** Kwa sababu hilo jina ni kama mtu ku-protest. Ukiliweka mahali ambapo halikuwako, - lakini hilo jina mtoto anazaliwa, anakuta hilo jina, linafutia tabia mbaya.

**Com. Lethome:** Ni jina ukabila peke yake ama unasema nini?

**Bernard Kamau:** Hata kusema jina ukabila. Ninasema ya kwamba kama mkutano ukifanywa, ukabila unazungumzwa hapo. Na hayo mambo ndio inaharibu. Huo ukabila. Kwa sababu mtoto anazaliwa, anakuta hilo jina linafutia yale mabaya.

**Com. Lethome:** Umesema, Mbunge akihama chami chake, tusichaguane tukae hivyo hivyo?

**Bernard Kamau:** Hiyo ikae namna hiyo.

**Com. Lethome:** Nani atawakilisha hiyo sehemu yake ya ubunge?

**Bernard Kamau:** Mbunge aliyekuwa anataka kutoka, atumie pesa yake, uchaguzi ufanywe. Kwa sababu sasa mtu anatoka hapa na hofu. Anatoka chama anaenda kingine. Tena, Serikali iwe sponsor wa uchaguzi. Sasa hapo ni pesa ya Serikali ndio inatumika.

**Com. Lethome:** Apoteze kiti chake ama asipoteze?

**Bernard Kamau:** Ikae namna hiyo.

**Com. Lethome:** Asipoteze?

**Bernard Kamau:** Akienda huko, hiyo siasa anataka kwenda, apatiwe kiti na wanachama. Lakini mahali anatoka, akae namna hiyo. Liko lingine?

**Com. Bishop Njoroge:** Hapana hakuna lingine. Ningepata Honourable Sing'aru.

**Honourable Sing'aru:** Waheshimiwa Commissioners, Co-ordinator pamoja na timu yake. Jina langu ni Mheshimiwa Philip Sing'aru kutoka district ya Kajiado. Nafikiri nina maneno machache na ninataka kuanza moja kwa moja.

**Rais:** Rais awe na mamlaka. Na mamlaka yake agawanye na Waziri Mkuu. Maneno ya Deputy Prime Minister sikubaliani nayo. Kwa sababu ya hivi; nikiangalia Nigeria, nimeona pia na Uganda na Zimbabwe, wale wote deputy Prime Ministers hawako.

Kwa hivyo katika Africa, ningependa Rais awe na mamlaka lakini mamlaka yake iwe reduced na Prime Minister apewe ingine lakini President awe na say ili aweze kutawala nchi.

Bunge: Bunge pia iwe na control although wao ni lawmakers. Kwa sababu, kama mnavyoona, wamejipatia mishahara mikubwa na wao kama lawmakers, wangukuwa fair. Maana civil servants, the labour force hata wao wangeinuliwa ile mishahara. Mishahara ya wabunge na civil servants ama wafanyikazi wa Serikali, iwe kidogo – Ikiwa kama hiyo sasa ni mingi, iwe reduced na igawanyiwe wananchi wengine wa Serikali maana wanafanya kazi muhimu katika Kenya. Ili hiyo nafasi ipewe wengine ambao wako chini na wengine wako juu. Nafikiri wakati huo watakuwa fully independent of the people. Maana hata sasa, raia wanalia. Hata ingawa wanawatala na kuwaongoza kwa sababu ya pesa nyingi ambazo wamejipatia kwa sababu wanataka mamlaka ya kufanya hivyo.

Jambo lingine ni KWS: Elephant problems and their destruction. Ningependa KWS katika hapa UMaasaini ama pastoralists, wanyama wale wako katika national parks ni wachache na wale wako katika group ranches ni wengi kuliko wale ambao wako katika council.

Sasa, international donors wanatuma pesa nyingi kwa sababu ya hawa wanyama wa porini ili ile ecosystem ambayo sasa wanataka kusaidia community kwa kupata hiyo pesa. Lakini hiyo pesa ni kidogo inakuja kwa wananchi, kwa community. Pesa nyingi inachukuliwa na wale wasimamizi wakubwa ambao wanafanya kazi katika KWS. Hiyo pesa yote iwe ikiingia kwa wale wananchi ambao wanyama hawa wanawaua, wanaharibu mimea yao na wanaua ng'ombe zao na kueneza tickborne disease. Pia ili wananchi wafurahi na waweze ku- conserve wale wanyama wa porini kwa njia ile ambayo inafaa kwa sababu tunajua ya kwamba, wanaitea Kenya pesa nyingi za kigeni.

Nikija katika Provincial Administration, mimi ninaunga mkono Provincial Administration waendele. Bwana Commissioner, ulikuja saa hii na ukampongeza D.O. kwa sababu ya ile arrangement amefanya mpaka hii kazi yote inafanywa. Tena ukiangalia amani na ushirikiano wa wananchi uko. Kama Provincial Administration ikiondolewa, iwe ni politician kama mimi ama kama wengine, tuta-create tribalism, nepotism na mambo yale mengine ambayo ni tajiri ya kila community. Na Provincial Administration - huyu D.O. ametoka Mandera, lakini mimi nikiingia hapa nina-clan, nina age group, nina party lakini yeye hana. Anafaa wale wananchi properly vile inavyohitajika kulingana na sheria ya nchi.

Nikija katika Elections - Election process. Tunataka mambo ya elections yasimamiwe na Electoral Commission hata agents wote, ili kusiwe na rigging. Kuna mambo mengine ambayo hayafai. Ili tupate uchaguzi wa haki, wananchi wapate ule uchaguzi ambao wanahitaji ambao wao wenyewe wanapenda. Maana kama mimi nikija kutoa agent, huyo agent hatapenda yule mpinzani wangu na mpinzani wake hatanipenda. Hata wale wa ku-decide ni sisi raia, tunaangalia tunampa kiti na sisi ni binadamu. Lazima Wamaasai wampatie kiti na sheria inapotea hapo tunataka kila kitu kichukuliwe na Electoral Commission - usimamizi wote wa uchaguzi ili tuwe na fair and just elections.

Local Authority: Tunataka Local Authority isimamiwe na Serikali kwa sababu ukiangalia kutoka locations, Councillors wanaenda hapa, all the plots anafanya kama property yake na ni mali ya wananchi wa pale. Inatakiwa all planning, plots ziwe zikidhibitishiwa pale, ziki-allotiwa pale na ziende kwa wale watu ambao wanastahili kupata badala ya an individual kuja kuzipatiana kwa watu marafiki na kutumia political party apatie wale watu anapatia ama anyime wengine. Maana plot ni ya all the parties sio ya party moja. Kama mimi sasa nikiwa Chairman wa KANU, niseme watu wa KANU wapewe, wa D.P. wasipewe. Hakuna justice hapo. Tunataka plot ziwe pale na watu wote waangalie pale na Provincial Administration ya mahali pale waangalie na viongozi wengine. Ili wananchi wapate haki yao kama plot ni hali ya kila mtu ambaye ako katika hiyo sehemu.

**Com. Bishop Njoroge:** Mheshimiwa you have used almost fifteen minutes. So please wind up.

**Honourable Sing'aru:** National Park: Hapa Maasaini ni national park. Tunataka kama hizi national parks, hizi national parks zirudishwe kwa wananchi maana wanyama wanatoka ndani ya park, wanakuja kula mashamba na kurudi katika park. Na ng'ombe hawawezi kuruhusiwa. Tunataka hata ng'ombe waruhusiwe maana wanyama wale wako ndani ya group ranches, are more than those animals that are in the group ranches.

Education iwe compulsory na tukitaka education iwe compulsory, Chief Act irudishwe maana kuna watu wengine ambao hawajui faida na maana ya elimu. Ili sasa watoto walazimishwe kwenda skuli.

Ya mwisho ni KMC. Unajua sasa liberalization imeua biashara, mapato ya wakulima hawapati. Hata KMC iko pale kama picha na haisaidii chochote. Na unajua pastoralists, hawana shamba lingine, hawana kahawa, hawana majani, wanategemea nyama. Tunataka iwe-revived ili iweze kusaidia wafugaji wa aina yeyote. AFC, isiwe (inaudible) iwe kama bank. Malipo ya hii AFC iwe kidogo ili iweze kusaidia wananchi ambao wako pale.

Nikimalizia ya mwisho, AFC ziwe banks na interested rates ziwe chini na iwe kama bank. Ya mwisho ni Maasai customary law, unajua Maasai Customary law, kama mwanaume akifa na bibi hana wavulana ni wasichana, yule mwanamke anafukuzwa. Tunataka mama akibaki arithi bwana yake katika ardhi na katika property ya aina yeyote.

Political Parties: Tusiwe na mingi kama hizi arobaini na tano, tuwe na four strong political parties katika nchi. Ili mtu akiona, this party is not good, aingie hiyo ingine. Yangu ni hayo na ninasema asante kwa kunisikiliza. Thank you very much.

**Com. Bishop Njoroge:** Asante sana Mheshimiwa, utajiandikisha pale. Paul Njuguna.

**Paul Njuguna:** Asante. Mimi naitwa Paul Njuguna, mfanyibiashara Loitoktok na pia Secretary wa DP katika location. Kwa

maoni yangu, ni upande wa Commissions of the Government. Kila Serikali, sasa hivi inapoundwa, mimi naona ingefaa kuwe na Parliament za aina mbili. Kuwe na Upper and Lower ili wakati tunapochagua Parliament ya chini, iwe ya juu ndio inaweza kusimamia Serikali by that time, wakati wa Uchaguzi. Wakati pia tunachagua Parliament ya juu, kuwe Parliament ya chini nayo ndio imesimamia ule Uchaguzi ukifanyika. Yaani Serikali wakati uchaguzi wote unaendelea. Kusiwe President by that time, ambaye yuko. Ana uwezo wa kuwa katika Serikali ama kuwa na powers. Akiwa anang'ang'ania kiti, awe hana powers hata kidogo. Awe ni mtu ambaye anang'ang'ania kiti kama raia mwingine yule.

Ya pili, kuwe na Prime Minister. Mimi sijaona kazi ya Ma-Chiefs. Ma-Chiefs sioni kazi yao kabisa, because once mkikosana na Chief wa area yako, huyu ni mtu ambaye hamtatoka hapo milele na milele. Wewe ni neighbour yake, labda ng'ombe hukula kwake na watoto. Akiweka *kitati* hakuna wakati mtakuja kugundua. Chief, na Sub-Chief waondoke katika formation ya Serikali. Kuwe na D.O. D.O wanaweza kuja hapa hata watatu ama wanne. Na sababu D.O. atapigwa transfer, yule mtu walikuwa labda wamechukiana na yeye, ana uwezo tena wa kujiinua. Ana uwezo wa kujiinua wakati huyo D.O. atakapoondoka.

Life ya watoto: Kuwe hakuna kitu kinaitwa chokora. Serikali iangalie, ishike hawa watoto wote na iweze kuwasomesha. Yaani kuwe na masomo ya compulsory na iwe free. Kusiwe kuna mtoto hata mmoja anamangamanga huko town.

Kitu kingine ni expenses za Serikali: Kuwe kuna watu ambao wanakaa chini. Tuseme kama ni Bunge itafunua hicho kitu ama itapewa hiyo mandate, iwe ndio inaweza kujua Serikali this time itatumia kiwango fulani. Na kusiwe kuna safari ovyo ovyo, safari inatokea tu ghafla ya State. Pesa zinatumika, kutumika, kutumika na hazina mpangilio wowote.

Kitu kingine ni upande wa Parliament, yaani Member of Parliament. Mimi naona hivi, kuna watu ambao wanatumwa kutoka constituencies zao, wakifika kule wanaenda wanalala. Ni njia gani raia anaweza kumuondoa yule mtu hata kabla ya siku ziishe? Kwa sababu ni miaka mitano, na miaka mitano ni mingi. Kama MP hatawafanyia kazi yeyote na nyinyi mnangoja tu miaka mitano iishe na hakuna kitu anayofanya, basi it is a waste. Mtakuwa mme-waste ile miaka yote mitano. Kuwe na njia ambapo those people ambao ni wa hiyo constituency, wana njia wanaweza kumuondoa. Kama President ana njia ya kuondolewa na wao, kwa nini wao wasiwe na njia ya kuondolewa na nani? Na wale waliowachagua. Vote of no confidence ya raia, iingizwe na njia ambayo itaweza kumuondoa Councillor ambaye hafanyi kazi yoyote.

Kitu kingine ni mambo ya uuzaji wa mali: Kusiwe kuna kuingiliana. Kama ni shamba, shamba ni lako, wewe ni mnunuzi, hata huwezi penda mtoto wako akiwa tu na mali moja ama kitu kingine. Na huwezi penda akiingiliwa wakati anataka kununua kitu chochote. So, kama ni kuuza, mwenye mali aki-decide kuuza, kusiwe kuna kuingiliana kwingine. Huyu sijui ameachwa bila ama amefanya nini. Kama akili zake zimemuonyesha kuuza, auze ni mali yake.

Kitu kingine ni upande wa education: Education imekuwa haya mambo ya quota system, mimi sioni kama kuna haja ya kuwa na



quota system ya education. Because zile subjects tunazofanya ni moja everywhere. Mtihani ni mmoja. Kwa nini mtoto hapa, apate marks six hundred, mwingine huko chini apate five ama apate four hundred, na kuwe ule wa four hundred anaenda shule nzuri kuliko huyu wa six hundred. Mtihani ulikuwa mmoja, mwalimu amefundishiwa pahali moja. So, iwe mtoto kutoka pale mwanzo mpaka mwisho, watachukuliwa kulingana na mapato yao.

Kitu kingine ni Local Government. Local Government hawafanyi kazi yao. Local Government hatuoni kazi yao. Kazi ya Local Government iwe wamepangiwa kazi fulani, kama ni kuweka maji area hii, waweke maji. Kama ni barabara wamepangiwa, wawe kazi yao ni ya barabara. Lakini sio pesa tu ziwe zinatumika tu na hata hatuelewi vile zinavyotumika. Thank you.

**Com. Bishop Njoroge:** Kuna swali.

**Com. Lethome:** Umesema mtu akitaka kuuza mali yake, let's say mtu anataka kuuza land, mtu awe na uhuru wa kuuza kile anachotaka, uwe ni mbaya uwe ni mzuri, asiingiliwe. Na je unaonaje kwa mfano kama family itakuwa involved katika hilo shamba? Hiyo ndio unaita kuingiliwa kama bibi na watoto - is that what you are suggesting?

**Paul Njuguna:** A family is a part of you. So, you are - kuhusu, familia sasa ndio nimewalifikiria hilo jambo.

**Com. Lethome:** Swali lingine. Kuna mahali pengi tumeenda na watu wamesema kazi ya Chief ni muhimu sana kwa sababu yuko karibu na watu. Lakini wamesema Chief wawe wakiwa-transferred katika eneo lingine katika district hiyo au division hiyo. Unafikiria hiyo itaondoa shida hiyo ukiwa na kisasi na Chief? Chief aweko, lakini can be transferred within the division or the district.

**Paul Njuguna:** Ndio nilikuwa nauliza, kuna haja gani ya kuwa na Chief na kuwa na D.O. ambaye amesoma? The best thing ni kuwa na D.O. ambaye amesoma hata kama watakuwa watatu, waje wafanye ile kazi ya Chief. Lakini si kuwe na Chief ambaye hawezi kuondoka pahali pale kwenye kijiji.

**Com. Bishop Njoroge:** Can we have Paul Mwangi?

**Paul Mwangi:** Jina langu ni Paul Mwangi. Kwa maoni yangu ningeonelea, Administration iliyoko kwa wakati huu iendelee lakini katika upande wa Chief, tubadilishe. Tuwe, badala yake, tuwe na Councillor ambaye ana nguvu. Ule mshahara ambao unalipwa Chief, uongezwe kwa Councillor ndio miaka mitano ikiisha, yule Councillor tunaweza kumuondoa na kuweka mtu mwingine.

Pia, ningeonelea tuwe na Prime Minister ambao watasaidiana kazi na President. Katika uajiri kwa Serikali kama vile Electoral Commission, Central Bank of Kenya navitu kama hivyo. Watuambayo ni makubwa ambao wanateuliwa na Rais, mpaka

Ma-DC na Ma-PC wapitie Bunge. Wale ambao wanataka hiyo kazi, waombe katika Bunge, ijadilie jambo hilo ili kupatikane mtu ambaye ana kiwango ambacho kinawezekana na hiyo kazi. Kwa hivyo hayo madaraka yasiwe ya Rais, iwe katika Bunge. Katika mashamba, kila mtu awe na uhuru wa kununua shamba popote pale katika nchi ya Kenya, mahali ambapo anafaa akae. Thank you.

**Com. Bishop Njoroge:** Thank you very much Paul. Jacob Partimo karibu.

**Jacob Partimo:** Kwa majina mimi naitwa Jacob Partimo Munge, mkaaji wa Loitoktok. Ningependa kuchangia nikisema ya kwamba, kile ambacho ningependelea Katiba ichukue ni kuwe na Serikali ya Majimbo. Ninaposema Majimbo, nasema kwanzia ngazi ya Mkoa, hadi katika kijiji. Rasilimali zilizoko, ziweze kutawaliwa na lile jimbo, iweze kusaidia wakaaji wa ile sehemu. Mauzo za rasilimali hizo, ziuzwe katika vijiji. Wazee wa vijiji wanajua vile watakavyoweza kusaidia kila familia iliyoko pale.

Ningelipendelea pia katika Katiba ya kwamba, masomo yawe ni ya bure, kwanzia darasa la kwanza hadi chuo kikuu na kuwe - tuangalie kuna sehemu zilizoendelea tangu wakati wa ukoloni. Unakuta mtoto wa Kajiado ambaye amepata B + hapati nafasi ya kuingia katika chuo kikuu. Kuingia katika Chuo Kikuu iangaliwe kulingana na kadiri na vile watu walivyo. Pia ningeweza kusema ya kwamba, Serikali iliyoko katika mamlaka, itupilie kitu kinachoitwa soko huru. Iweze kutunza wananchi wake.

Wanyama pori: wanaua binadamu na malipo ni shilingi elfu thelathini. Napendekeza hizo sheria zinatudhulumu hivyo, zitupiliwe na iwe ni zaidi ya shilingi milioni tano kwa binadamu mmoja. Pia mifugo na uharibifu wa mashamba uweze kutunzwa. Wawe compensated. Serikali pia iweze kulinda haki ya kila mmoja. Ninaposema hivyo, nasema ya kwamba sheria za Ma-Chief, ziwe kama zilivyokuwa hapo awali. Sio ile ya 1998. Ili kuweza kutunza kila mmoja. 75% ya sheria za nchi hii ambayo inahusu Commissioner wa Ardhi ama Waziri wa Ardhi, aweza kutangaza sehemu kuwa ni sehemu ya wanyama wa pori. Hiyo sector itupiliwe kwa sababu wanakijiji wanajua manufaa ya hiyo ardhi.

Kazi: Kazi, kulingana majimbo - mahali ambao umetoka, upate kazi pale lakini wataalamu wawekwe katika Serikali kuu. Asilimia sabini na tano, ipewe wenyeji. Rasilimali zilizoko katika sehemu, wananchi waweze kuwa na uhuru wa kuziua. Kwa mfano mali wauze na wafanye matumizi katika kujiendeleza hali yao.

Habari ya uuzaji wa ardhi: Nilisema ya kwama wanakijiji waweze kutawalana ndio tumesema Serikali ya Majimbo itoke kwanzia vijijini mpaka mkoani. Asante.

**Com. Bishop Njoroge:** Umesema kwamba rasilimali ziwe za jimbo na jimbo litawale hizo rasilimali. Unaweza kutuambia, kama tutakuwa na Central Government, na Central Government itakuwa ni nini? Pia ningetaka kukuuliza, kama yale maji inakunyiwa Nairobi, inatoka Mt. Kenya na watu wa Central Province wakipewa ruhusa ya kutawala hayo maji, inaweza

kusemekana watu wa Nairobi - nikisema Nairobi, hamtapata maji hawawezi. Now, port ya Mombasa ndio mnapeleka mavuno yenu na watu wa Mombasa wakisema kutoka leo port...kuna nyingine ambazo zitadumishwa na Serikali na zingine zidumishwe na Jimbo?

**Paul Njuguna:** Ninaposema hivyo, nasema ya kwamba, maji hayo huwa yanauzwa hata hapo Nairobi, lakini hizo pesa maji inapouzwa, zirudishiwe wananchi walioko pale.

**Com. Bishop Njoroge:** Alais Ole Kisonokoi

**Alais Ole Kisonokoi:** *Neaku ta pe airo ena enkutuk ormaasai. Ore ta ene dukuya kaji Alais ole Kisonokoi.*

**Translator:** Ninaitwa Alai Ole Kisonokoi.

**Alais Ole Kisonokoi:** *Na ara ata olopeny ena area le Ntonet ene naamanya.*

**Translator:** Mimi ni mwenyeji katika area ya Endoneti.

**Alais Ole Kisonokoi:** *Ore maoni ai na iji eikunino.*

**Translator:** Maoni yangu ni kama yafuatayo,

**Alais ole Kisonokoi:** Ore enchoto edukuya naishari ana Amboseli, ana Tsavo na kijoito enkop ang apa neshomo mikiyiolo kaoitoi apa eshomokie.

**Translator:** Ile ardhi yetu kama Tsavo West, pamoja na Amboseli, tunasema sisi kama Wamaasai ni ardhi yetu na imenyakuliwa.

**Alais Ole Kisonokoi:** *Nikijo oi teneshukunye alotu enkop ang ana ake.*

**Translator:** Tunasema ya kwamba, tungehitaji irudi ama irudishwe kwa wenyewe.

**Alais Ole Kisonokoi:** *Amu ore nena nguesi na iyiok leitu ear amu ikiyiolo muhimu ene na iyiok otapala.*

**Translator:** Maana wanyama wa pori ni sisi kama wenyeji wa Maasai, tulikataa kuwaua kwa hivyo tulikuwa tunajua umuhimu wake na hata hivyo hatuku....

**Alais Ole Kisonokoi:** *Kigira aomonu ore inakop ang apa kinitapalie nena nguesu naba neija nearita iyiok nearita nkishu ang nimikiata napatao nikitumito ikidolita ajo enkop apa nashomo tenkoitoi nguesi.*

**Translator:** Tunaona ya kwamba nchi hiyo yetu imenyakuliwa na wanyama wale wako hapo wanaendelea kuumiza wenyeji. Na tunaona ya kwamba hiyo nchi imenyakuliwa kwa njia mbaya. Kiasi ya kwamba ni kama kulikuwa na mpango wa Serikali kunyakua hiyo nchi ili Wamaasai waumizwe na wanyama.

**Alais Ole Kisonokoi:** *Nikijo ikiningu ake ejoitoi ore nena nguesi netara kumpk neeta eneba.*

**Translator:** Huwa tunasikia tu....

**Alais Ole Kisonokoi:** *Atejo ore to nguesi kining ajo eleki kake eitu aikata kidol ilo olaaki.*

**Translator:** Watu wengi wanaumizwa na wanyama na tunasikia ya kwamba wanalipwa na mpaka wa leo hatujawahi kuona mtu amelipwa.

**Alais Ole Kisonokoi:** *Ore nena nguesi naarita iyiok na iyiok otapala eitukiar nikijo oi peshukunye aku enang pekilaki ate nena nguesi near iyiok amu mikijo pikiishu amu kitodua ajo keeta faida kop.*

**Translator:** Tunasema ya kwamba wanyama wako katika area yetu, na area ni yetu. Tunasema ya kwamba turudishiwe hiyo area maana hatutamaliza wanyama lakini tutakuwa tukijua vile tutajilipizia wanyama wanapoumiza watu.

**Alais Ole Kisonokoi:** *Ore peaku enchoto enkisuma na ikidol ajo kijo pe ishoru serikali enkisuma e pesho kuanzis nursery mpaka university.*

**Translator:** Tunasema ya kwamba kupitia upande wa elimu, tunaomba elimu ya bure, Serikali iruhusu kutupatia elimu ya bure, kutoka ngazi za chini nursery school mpaka University.

**Alais Ole Kisonokoi:** *Ore ena majimbo nikiyieu.*

**Translator:** Tungependa majimbo irejeshwe.

**Alais Ole Kisonokoi:** *Kake me ikiyieu enikijo pe kingoro ajo ena abila o ena amu kira ormaasai iyiok oitayu lowakaaji leine neaku neishori ina majimbo.*

**Translator:** Kusema majimbo tupewe sio kwamba eti ni kusema ya kwamba Wamaasai wenyewe waende wenyewe, lakini tunasema mkaaji wa ile sehemu awe na jimbo katika jimbo hilo hilo. Awe ni kabila ya aina yeyote ile.

**Alais Ole Kisonokoi:** *Amu ina kata kitum airita kuna mali napuku tiatua iyiok.*

**Translator:** Maana ndiposa tutaweza kuchunga rasilimali zetu ili ziweze kutusaidia.

**Alais Ole Kisonokoi:** *Ore pe eaku ena shoto olaiguenak na iji, kijo si ina ore olaiguenani peton ak edou pe eta egeli oshi tata olaiguenani orministai obo.*

**Translator:** Upande wa Ma-Chief, tunasema ya kwamba, Ma-Chiefs wanaweza kuwa wanachaguliwa na mtu mmoja.

**Alais Ole Kisonokoi:** *Negelaki iltunganak kumok lena area.*

**Translator:** Huyo mtu mmoja akichagua Chief anamchagulia watu wenu.

**Alais Ole Kisonokoi:** *Nelotu ilo laiguenani ajo nanu ta otegeluaki neme iyie likitegelua aas ena enayieu.*

**Translator:** Huyo Chief anakuja anasema ya kwamba, “mimi nimechaguliwa na sio nyinyi mmenichagua.”

**Alais Ole Kisonokoi:** *Nikijo oi ena aku na, kake io eneaku na iyiok nagelu.*

**Translator:** Tunapendekeza ya kwamba, Chief awe akichaguliwa na raia.

**Alais Ole Kisonokoi:** *Ore ene mwisho na ata na eishua kulikae tunganak enetejo najo ashe te ina kiti muda nanoto.*

**Translator:** Ni hayo tu, asante.

**Com. Bishop Njoroge:** Mzee, kuja ujiandikishe, asante kwa maneno yako mazuri. Mtungeyi Mpaaye.

**Mtungeyi Mpaaye:** Mimi kwa majina naitwa Mtungeyi Ole Mpaaye na maoni yangu ni hivi. Nazungumza kwa Kimasai kwa sababu mimi ni Mmasaai na hiyo lugha ndio najua kuliko Kiswahili. *Najo na iji, ore duat ai na iji etiu.*

**Translator:** Maoni yangu ni kama yafuatayo.

**Mtungeyi Mpaaye:** *kidol ajo ore na ntokitin apa nikiata tenejokini na iyiok maiturai ena kishon e tata na kiata baa kumok nikijo amu otunguaye ore peasayu negelieki iyiok ana olopenye enkop.*

**Translator:** Kulingana na mambo ama maisha ya sasa, kuna mambo mengi yanatendeka ambayo ni ya kusaidia lakini inapaswa kuwa tunaulizwa kwanza kabla haijatendeka.

**Mtungeyi Mpaaye:** *Ana e Amboseli.*

**Translator:** Kama vile Amboseli.

**Mtungeyi Mpaaye:** *Amu ore apa enaibungayieki naake mikiyiolo.*

**Translator:** Maana Amboseli ilipochukuliwa, hatukuhusishwa kama wakaaji wa sehemu hii.

**Mtungeyi Mpaaye:** *Nikidolita ajo enkop ang apa etipat oleng.*

**Translator:** Na tunaona ya kwamba ni area yetu ambayo ni area ya mojawapo muhimu zaidi.

**Mtungeyi Mpaaye:** *Na tenewaki apa mikiyiolo faida enye nikietuo aiyiolou.*

**Translator:** Na kama ilichukuliwa kabla ya sisi kujua faida yake, sasa tumeshajua faida.

**Mtungeyi Mpaaye:** *Nikidol na apa ewaki tenkoitoi e giza.*

**Translator:** Na tunaona ya kwamba, hiyo ardhi imechukuliwa kwa njia ya giza.

**Mtungeyi Mpaaye:** *Nikietuo adol ajo eitauto faida sapuk nimikitumito.*

**Translator:** Tunaona ya kwamba iko faida nyingi lakini hatuoni sisi kama wakaaji wa sehemu hii.

**Mtungeyi Mpaaye:** *Nikidol ajo enarikino peshukokini iyiok metotiu ana apa.*

**Translator:** Ningependekeza Amboseli National Park irudishwe.

**Mtungeyi Mpaaye:** *Arashu ake ninye ore entoki natiuneki tena kata.*

**Translator:** Au kile kitu ambacho ama faida yeyote ambayo inatokana na Amboseli kwa sasa,

**Mtungeyi Mpaaye:** *Neaku are neaku ore asili mia sabini na tano na nguna ang.*

**Translator:** Asilimia sabini na tano iwe ni yetu sisi kama wenyeji.

**Mtungeyi Mpaaye:** *Ore enkae.*

**Translator:** Jambo lingine,

**Mtungeyi Mpaaye:** *Ore enkare nijo nena Ontureishi na ninye egira oloitoktok na enata apa eitegelieki iyiok peishori.*

**Translator:** Haya maji ya *Ontureish* ambayo ni yetu kama wakaaji wa Loitoktok, ingefaa inapochukuliwa, tuhusishwe kama wenyeji.

**Mtungeyi Mpaaye:** *Ore esiai e KWS.*

**Translator:** Mambo kuhusu wanyama wa pori,

**Mtungeyi Mpaaye:** *Ore ana peponui ajokini iyiok nena KWS neaku osina teyiok.*

**Translator:** Tangu K.W.S ilipoanzishwa, katika sehemu hii ya Umaasaini, imekuwa ni hasara kwetu,

**Mtungeyi Mpaaye:** *Osina eyaka iyiok badala e faida.*

**Translator:** Imeleta hasara badala ya faida.

**Mtungeyi Mpaaye:** *Amu etuo tata nepuonu ajo ngunenye nguesi.*

**Translator:** Maana watu wa K.W.S. wamekuja wakasema wanyama ni wao,

**Mtungeyi Mpaaye:** *Newaita si ena ale lang na olalang.*

**Translator:** Na wamechukua ardhi na ardhi ni yetu.

**Mtungeyi Mpaaye:** *Ore kuna nguesi na iyiok oirita na iyiok eishorita hasara.*

**Translator:** Na wanyama hao ni sisi tunaangalia na bado wanatuletea sisi hasara.

**Mtungeyi Mpaaye:** *Nemeeta na entoki nikigira atumie.*

**Translator:** Na hakuna faida yeyote ambayo tunapata kutokana na wanyama hawa,

**Mtungeyi Mpaaye:** *Neeniar olndome obo nepuonu iltunganak to ntekei te Nairobi.*

**Translator:** Unapoonu tu ndovu moja imeangushwa chini,

**Mtungeyi Mpaaye:** *Nepuonu ndegei aingua Nairobi.*

**Translator:** Ndege zinakuja kutoka Nairobi,

**Mtungeyi Mpaaye:** *Ne enear enaduo ngues oltungani lang tene.*

**Translator:** Na mnyama anapoumiza mwenyeji wa hapa,

**Mtungeyi Mpaaye:** *Niishu ewiki eitu atum oladuo tungani liyieu liliki.*

**Translator:** Hata unaweza maliza wiki moja bila kujua utampelekea nani hayo maneno.

**Mtungeyi Mpaaye:** *Na tenilo doi ninye ade aliki.*

**Translator:** Na unapokwenda kumueleza,

**Mtungeyi Mpaaye:** *Nikijokini kietuo aingora neigeri pelaki.*

**Translator:** Unapambaswa tu unaambiwa ya kwamba “tunakuja kuona na italipwa.”

**Mtungeyi Mpaaye:** *Ore nena pisai naji pelaki.*

**Translator:** Hizo pesa ambazo tunaambiwa ya kwamba tatalipwa,

**Mtungeyi Mpaaye:** *Mpisai nemeitsha tonkulie wuejitin o jeneza.*

**Translator:** Ni pesa ambayo hata haitoshi jeneza ya kumzika huyo marehemu.

**Mtungeyi Mpaaye:** *Nai melakitoi ninye keduwa ngunyi.*

**Translator:** Na hata ikiwa pamoja na kuwa kidogo, hatujawahi iona, hailipwi.

**Mtungeyi Mpaaye:** *Nateneitu eidimayu pe eitayuni lelo tunganak neishori iyiok ina aria peaku lopeny nguesi.*

**Translator:** Ikiwezekana sisi kama wenyeji tupewe hayo mamlaka ya kuangalia wanyama na turejeshewe mamlaka hayo, sisi tutakuwa tukijua namna ya kujilipia.

**Mtungeyi Mpaaye:** *Nenare pelak ilo tungani ana nkunenye nkishu.*

**Translator:** Maana lazima huyo mtu atalipwa kulingana na vile inatakiwa maana sisi tunajua hasara ya binadamu na mnyama.

**Mtungeyi Mpaaye:** *Ore duo amu neta entoki naidim pelaki oltungani.*

**Translator:** Kwa sababu kama tujuavyo ya kwamba, mwanadamu huwezi kumlipa,

**Mtungeyi Mpaaye:** *Incho elaki millioni tomon.*

**Translator:** Ilipwe kama milioni kumi.

**Mtungeyi Mpaaye:** *Neingorari tana keisaidia na nkuti olongi.*

**Translator:** Tuone kama itasaidia hiyo familia siku chache.

**Mtungeyi Mpaaye:** *Ore enkae.*

**Translator:** Inginge,

**Mtungeyi Mpaaye:** *Ore ena najoitoi pemeetae olainguenani kenarikino peetai.*

**Translator:** Vile watu wanavyosema ya kwamba ma Chiefs waondolewe hiyo haiwezekani.

**Mtungeyi Mpaaye:** *Kake teneidimayu pegeluni ana orkansolai negeluni.*

**Translator:** Ikiwezekana kama ni uchaguzi ichaguliwe kama diwani ni sawa.

**Mtungeyi Mpaaye:** *Amu menarikino pegelu orbungei olainguenani peaku ninye olotu aitore laduo tungani.*

**Translator:** Maana mwanasiasa hafai kuwa anamchagua Chief.

**Mtungeyi Mpaaye:** *Amu ore olchekut obaya ake...*

**Translator:** Maana huyu Chief atakuwa akijuta ya kwamba atakuwa akinyeta. Atakuwa akinyeta ya kwamba, nimechaguliwa na Mbunge.

**Mtungeyi Mpaaye:** *Ore ene mwisho.*

**Translator:** Ya mwisho,



**Mtungeyi Mpaaye:** *Ena najo majimbo*

**Translator:** Ni kuhusu Majimbo.

**Mtungeyi Mpaaye:** *Ore ina naji majimbo nenare pekiata te shumata mpaka abori.*

**Translator:** Majimbo inatakiwa tuwe nayo kutoka ngazi za chini mpaka ngazi za juu.

**Mtungeyi Mpaaye:** *Pa ore ninye kulo kutikuti likitum na oitalakuni nikitum nkuti na kuna nkumok na nai na alang napuo shumata.*

**Translator:** Hata hizi pesa ndogo ndogo tunapata katika ngazi za chini, hazitusaidii.

**Mtungeyi Mpaaye:** *Nenare si sipitali peaku ene mwisho peaku ene pesho.*

**Translator:** Ya mwisho,

**Translator:** Matibabu yawe ya bure.

**Mtungeyi Mpaaye:** *Ashe.*

**Translator:** Asante.

**Com. Bishop Njoroge:** Asante sana Mzee kwa hayo yote. Fredrick Kimani, yuko wapi? Simeli Ole Nsempai.

**Simeli Ole Nsempai:** Mimi maendeleo yangu nilikuwa napenda kama....jina langu naitwa Simeli Ole Nsampai. Mapendekezo yangu nilikuwa nataka kama, unajua mimi sijui Kiswahili sana.

**Translator:** Yeye kwa maoni yake anaona Serikali inatunyima haki yetu.

**Simeli Ole Nsempai:** *Amu kisom inkera badala peidip form four nedumuni neyai lorin netai ena kop nemeetai neima te mutihani.*

**Translator:** Maana unasomesha mtoto, unapomtafutia mtoto wako shule, inabidi umpeleke shule za hali ya chini kwa sababu hachukuliwi.

**Simeli Ole Nsempai:** Kwa sababu mimi nilizunguka kwa sababu niliandikwa 1975 kwa kazi ya Serikali, anaenda mashambani kila pahali, anakuta walimu wote. Anajua elimu yote ilikuwa ni ya Wakamba, wanasomesha mandugu zao na lazima hao watoto wapite. Halafu napendelea Serikali itakayoingia, irudishie watoto wetu kusoma ili wakuje kusomesha mandugu zake.

Ya pili, siku hizi Serikali imenyima sisi haki. Kwa sababu wakati tuliandikwa sisi kazini, ichague mtu amesoma kwa sababu kazi ya bunduki sio lazima usome. Kazi ya kuandikwa kama askari sio lazima usome. Lakini siku hizi Wamaasai wametupwa kando, hawaandikwi kwa kazi, wanakuja kuandika watu wengine wanasema ni watu wa Kajiado, wanaacha wa Loitokitok. Tunapendekeza uajiri kama wa zamani, inasaidia. Kwa sababu ukifika area ya Umasaaini unakuta mtu amemaliza Standard eight, Form four yuko nyumbani. Serikali itusaidie sisi, tujisaidie sisi, tuandikwe kama zamani vile tulivyoandika na tulimaliza kazi yetu. Hatujasoma lakini hiyo kazi inaendelea vizuri mpaka wa leo tuko kazini. Sasa mimi sina mengi sana kwa sababu niligusia pahali ya majimbo na pahali ya masomo ndio nafaa nigusie kidogo. Kwa sababu area yetu imeenda kwa sababu tunapatiana kwa yule mtu ako na hope kidogo. Yule ambaye anaambiwa, 'nifanye kitu fulani halafu nikupatie kazi.' Serikali iangalie hapo. Sasa mimi sina mengi sana, ilikuwa ni hivyo tu na naomba Serikali iangalie kwa mambo hayo.

**Com. Bishop Njoroge:** Haman Ole Nsuki. Isaiah Ole Samana. Isaiah?

**Isaiah Ole Samana:** Yangu nitaanza moja kwa moja kulingana na vile nilivyoanza. Kwa majina naitwa Isaiah Ole Samana, mimi ni mkaaji wa Loitokitok sub-district. Yangu ya kwanza ni kuhusu Provincial Administration ama utawala wa mikoa. Utawala wa mikoa kwa mapendekezo yangu, ningependa iendeleo kudumu. Sababu ni kwamba utawala wa mikoa, hiyo inaunganisha ama inapatanisha mtu kwa mtu. Utawala wa mkoa unaimarisha maendeleo na kuunganisha wananchi. Ni chombo cha kuunganisha wananchi na Serikali.

Kuhusu madiwani: Madiwani mimi katika mapendekezo yangu, madiwani wanyimwe mamlaka. Kwa sababu gani? Diwani anapochaguliwa kuwa diwani, anakuwa na chance ya kunyakua ardhi ama kunyakua plots. Na kwa mapendekezo ningependekeza kuwe na kamati katika ward ya huyo diwani ambayo itakuwa ikihusika na mambo ya kupeana plot kwa wananchi.

Kuhusu wafanyikazi: Wafanyikazi wa kila idara, tungependa wawe asilimia sabini. Wawe ni wenyeji wa hiyo sehemu. Kwa sababu tunaona ya kwamba wafanyikazi wengi unakuta wanatoka katika nje, sio wakaaji wa hii sehemu na wakaaji wa hii sehemu wengi wao wamesoma. Lakini kwa sababu ya godfathers huko mbele, unakuta wale wenyeji weanakosa kazi. Kwa hivyo kwa mapendekezo ninaona ya kwamba wafanyikazi wa kila idara wawe wenyeji wa hiyo sehemu. Asilimia sabini.

Kuhusu Land Control Boards: Mashamba: Ningependekeza ya kwamba watu wanapouziana mashamba, waanze katika ngazi ya chini mashinani. Kwa sababu tunaona ya kwamba watu wengi siku hizi wanauziana mashamba na wanapelekana katika kazi ya mbele, ya juu zaidi. Bila kupitia ngazi za chini. Watoto hawajui, jirani hawajui, relative ya huyo mwenye kuuza hawajui. Kwa hivyo tungependekeza hiyo sheria ibadilishwe iwe mawelewano ya kuuziana mashamba ianze huko chini ndio wenyewe wapate kujua ya kwamba watoto watabakishiwa na sehemu ama huyo mtu asiuze kwa sababu kutakuwa na vile tutaweza msaidia hiyo ardhi ibaki.

Kuhusu masomo: Masomo kulingana na vile ninaona ya kwamba, masomo katika Kenya tunaambiwa ni ya bure lakini tunaona bado haijakuwa ya bure. Masomo tungependa iwe ya bure kwa sababu watu wengi katika Kenya hawana rasilimali, hawana mapato. Na tunaona watoto wao, hasa ndio unakuta wanapita katika shule. Lakini kwa sababu ya kuwa hawana mapato, watoto hao wataendelea na masomo. Kwa hivyo masomo iwe ya bure. Vile vile, matibabu. Tunaona ugonjwa hauchagui tajiri kwa sababu ndio ana pesa ya kujitibu. Tajiri na maskini wanapatwa na ugonjwa hali sawa. Kwa hivyo ningependekeza matibabu yawe ya bure. Ili watu waweze kuokolewa maisha yao.

Kuhusu ardhi, kusema ukweli ardhi ya Wamaasai, imenyakuliwa kwa njia ambayo hatujui imetokana na nini. Kwa sababu wanyama sio eti kwamba wanyama wanazaliwa Maasaini peke yake. Lakini tunaona ya kwamba ardhi yetu iliyonyakuliwa kam Amboseli na Tsavo West National Park, tunaona ni ardhi ambayo ingeweza kusaidia wananchi hasa katika hali ya kilimo na kupanda miti rasilimali ya aina mingi, tunaona ardhi yetu imenyakuliwa ambayo tunaweza pata manufaa nayo. Ningependekeza hiyo ardhi irudishwe kwa wenyewe. Maana tangu Wamasai walipopatikana, hakuna siku Maasai amekuwa adui na mnyama na ndio maana kwao ndio wanyama wanabaki. Na watajua vile wataendelea kukaa na wanyama.

Kuhusu MPs, ningependekeza kuwa, uchaguzi unapofanyika, Mbunge achunguzwe na watu wake kwa miaka miwili, akionekana hakuna kazi anaweza fanya, itolewe kura ya kusipokuwa na imani naye, aondolewe. Ili wananchi wasiendeleo kuumia kwa muda huo wote. Kwa sababu kama wananchi watakuwa wakikaa kwa miaka mitano katika taabu, hata mwezi mmoja ni shida licha ya miaka mitano. Unakuta.....

**Com. Bishop Njoroge:** Nakupatia dakika moja.

**Isaiah Ole Samana:** Hata hivyo nimemaliza. Kwa hivyo ningependekeza ya kwamba iendelee. Kuhusu mambo ya Ma-Chiefs, Ma-Chiefs waendeleo kwa sababu wao ndio wanaelewa shida na taabu ya familia zile ziko karibu na wao. Wao ndio wazaliwa na wanajua shida, na umaskini na unyanyasaji wa wale watu. Kwa hivyo ningependekeza Chief aendelee kubaki, Provincial Administration yote kutoka Sub-Chiefs, mpaka Province iendelee. Asante.

**Com. Lethome:** Ngojea kidogo kuna swali hapa. Kuhusu zile National Parks, wasema ardhi ya Wamaasai, warudishiwe Amboseli na Tsavo. Wa-Sumbaru nao wakisema yao warudishiwe, Meru National park warudishiwe. Unapendekeza yaani Kenya tusiwe na any National park ama vipi? Kwa sababu it has to be curved out kutoka kwenye ardhi ya watu fulani. Kwa hivyo unapendekeza katika Kenya tusiwe na National Parks zozote ama vipi?

**Com. Bishop Njoroge:** Ningetaka kuongeza hapo, katika mapato mengi kutoka National Park, zinaenda kwa Central Government na ndio expenditure ya Serikali inatokana hapo. Hivi ni kusema kwamba mapato hayo sasa haitakuwa ya Central Government, ungetaka iwe ya Jimbo, kwa hivyo Central Government itafute njia kufanya mapato yake.

**Isaiah Ole Samana:** Kuhusiana na vile nilisema National Park, nikiongelea kuhusu Amboseli na Tsavo West, hiyo ningependekeza kusema National Parks zote zilioko upande wa Umasaaini, zirejeshwe kwa wenyewe maana mapato yake huwa Wamaasai wanapata mapato ndogo kuliko zile ambazo zinaenda katika ngazi za juu. Kwa hivyo turejeshewe ili mapato iwe yetu. Maana sisi tutajua vile tutakuwa tukitumia kuliko tuwe tuna-controliwa na watu wengine ambao hawajui manufaa na hasara ya Wamaasai.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo wa-retain National Parks, lakini under their management?

**Isaiah Ole Samana:** Yes.

**Com. Bishop Lethome:** Tupate Ole Lekishoni. Kasaini Ole Mbugua. Utaongea kwa Ki-Maasai, anza kwa jina lako.

**Kasaini Ole Mbugua:** *Kaji james naitwa Kasaine ole Mbugua. Kalo nanu airo tenkutuk* Nitaongea kwa lugha ya Ki-Maasai kwa sababu ndio nitaweza kuwa naelewa. *Ore enai nanu nanu aloaimaki nakalo aitayu tendorop.*

**Translator:** Lake ni fupi,

**Kasaini Ole Mbugua:** *Ore nanu kaimaki baa are.*

**Translator:** Mimi nazungumzia mambo mawili peke yake.

**Kasaini Ole Mbugua:** *Alo aimaki ajo kiyieu nai ore Katiba e tata.*

**Translator:** Tungependekeza Katiba ya leo,

**Kasaini Ole Mbugua:** *Ore sipitali pemokini aku kebaki iltunganak pesho.*

**Translator:** Hospitali iwe ya bure.

**Kasaini Ole Mbugua:** *Amu ore iltunganak mekure eti oltungani ota engolon.*

**Translator:** Kwa sababu kwa wakati huu hakuna mtu ana uwezo.

**Kasaini Ole Mbugua:** *Ore eniare.*

**Translator:** Ya pili,

**Kasaini Ole Mbugua:** *Na esiai naipirta ingues.*

**Translator:** Ni kuhusu wanyama.

**Kasaini Ole Mbugua:** *Ore enguesi na sidan eti enkop.*

**Translator:** Na wanyama ni vyema sana kuwa katika dunia ama kuwa katika area.

**Kasaini Ole Mbugua:** *Kake ore eti atua enkop neyieu si na iltunganak eita serikali tipat alang ninche.*

**Translator:** Inapaswa hata kama tuko na wanyama.

**Translator:** Lakini inafaa mwanadamu awe muhimu zaidi ya mnyama.

**Kasaini Ole Mbugua:** *Ikiningito oshi ake iltunganak oarita nguesi kake eitu aikata kidol nitu kining olatalaki.*

**Translator:** Maana huwa tunasikia watu wanaumizwa na wanyama lakini hatujawahi kuona mtu ambaye amelipwa.

**Kasaini Ole Mbugua:** *Nikiyieu nemokini alaki iltunganak amu eishori oltungani oleng.*

**Translator:** Inafaa mtu awe katika laini ya mbele kwa sababu mtu ndio muhimu kuliko mnyama.

**Kasaini Ole Mbugua:** *Amu kinyo nai ore tentoki namokini alak oltungani tenear ngues.*

**Translator:** Kwa sababu malipo ya mtu kulingana na vile ninavyopendekeza, malipo ya mtu akiumizwa na mnyama,

**Kasaini Ole Mbugua:** *Keyieu kemokini alakaki milioni imiet.*

**Translator:** Awe akilipwa milioni tano.

**Kasaini Ole Mbugua:** *Kiata si ake ilchambai tiatua.*

**Translator:** Tuna mashamba ndani.

**Kasaini Ole Mbugua:** *Kepuonu nguesi nanya ilchambai loitunganak neaku nibaki ake teine wueji kake midol entoki ho nabo nikilakini.*

**Translator:** Unakuta mashamba yanaliwa na wanyama, wanaharibu mimea na hatuoni faida yeyote ambayo tunarudishiwa ama malipo ambayo tunalipwa.

**Kasaini Ole Mbugua:** *Neaku ipiri alo aisitayie nena nguesi na pookin entoki nikijokinii nena nguesi ongira aisomita nkeru.*

**Translator:** Unapokimbia kwenda kuripoti kwamba wanyama wameharibu shamba langu, unaambiwa hao wanyama ndio mnapata mapato ya kulipia watoto shule.

**Kasaini Ole Mbugua:** *Nikiyieu nemokini si alaki lapurok tenenya nena nguesi nchambai lenye.*

**Translator:** Na tunataka wakulima wawe wakilipwa pesa ama hasara ile imeletwa na wanyama wakati wanapoingia

mashambani.

**Kasaini Ole Mbugua:** *Ore elakinoto neitegemea ana ewuei nainosa engues.*

**Translator:** Na malipo inategemea na mahali wanyama wameharibu.

**Kasaini Ole Mbugua:** *Ore teneinosa ekai are nikilakini ake ana enkishakinoto wo eda naba enaitau ilo shamba.*

**Translator:** Kama wamekula ekari mbili, ulipwe kulingana na hasara ile umepata.

**Kasaini Ole Mbugua:** *Tena guniani tomon oshi intayu te eka nikilakini ake lelo.*

**Translator:** Kama ni gunia kumi ndio unatoa kwa eka, ulipwe.

**Kasaini Ole Mbugua:** *Na tana tikitam nikilakini ake lelo.*

**Translator:** Ama ni arobaini ulipwe.

**Kasaini Ole Mbugua:** *Ajo ore nanu ene wueji aitibaiki.*

**Translator:** Kwa hivyo anafikisha hapo,

**Kasaini Ole Mbugua:** *Ajo she oleng.*

**Translator:** Asante sana.

**Com. Bishop Njoroge:** Thank you very much. David Ole Karia. Yuko? Karibu.

**David Ole Karia:** Kwa majina, naitwa David Ole Karia, mimi ni mfanyikazi wa Serikali. Nachangia tu kuhusu mambo ya elimu. Elimu katika sehemu nyingi Kenya, itiliwe mkazo. Hasa kwamba watu wa jeshi. Ningeomba tu kama ingewezekana, elimu iwe ni free education kwa watu wote nchini Kenya. Halafu mnapokumbuka early ages, wengi walikuwa wanasoma, sasa hivi tunaona wengine wanatoka shuleni kwa sababu hawajiwezi kimaisha.

La pili ni land issues: Kuhusu ardhi. Ardhi mimi nikiwa mmoja ama nikiwa Mu-Maasai, hasa nataka kutetea mambo ya ardhi, kwamba zile colonial boundaries zirudishwe na tuheshimu zile treaties ambazo zilikuwa zimewekwa. Hasa tuchukuliwe ya kwamba, mmoja wetu mkimbuka juu ya historia kulikuwa na mtu alikuwa anaitwa Ole Lenana. Yeye aliweka land treaty na hivyo iheshimiwe. Asante sana.

**Com. Bishop Njoroge:** Virginia Ruguru?

**Virginia Ruguru:** Mimi naitwa Virginia Ruguru. Maoni yangu ni moja tu ama mawili, nayo ni kuhusu education of our children.

Yaani elimu ya watoto wetu. Watoto wetu tunawosomesha vizuri sana. Wanasoma kutoka Nursery, Primary na Secondary lakini wakifika Secondary na wakitoka wanapita vizuri sana. Lakini hapo ndio mwisho, hawapati colleges ama kazi. Kwa ajili gani? Kwa sababu Ministry of Education hutoa hayo majina nje ya shule ya kuonyesha ya kwamba hao watoto wamepita. Lakini hawachukui jukumu la kuorodhesha hawa watoto katika ma-colleges. Ningependekeza hapo nikaona ya kwamba, watoto wakiwa wamepita, wawe wanachukuliwa huko maofisini. Ama kwa ofisi ya Ministry, wanapelekwa katika ma-colleges ya Serikali. Wanaitwa katika ma-colleges ya Serikali. Badala ya mzazi mwenyewe kuchukua hilo jukumu la kumchukua mtoto, tena anakwenda kumtafutia college. Yangu ni hayo tu.

**Com. Bishop Njoroge:** David Kiumu, headmaster.

**David Kiumu:** Kwa majina naitwa Mr. David Kiumu. Mimi ni Mwalimu kutoka Ilasit Secondary. Ningetaka kuzungumzia hasa mambo kuhusu elimu. Kwanza kuna jambo moja ambalo limetusumbua sana. Watoto wetu wamekuwa wanatolewa shuleni, wamekuwa wakitolewa shuleni na watu kabla ya kumaliza shule. Ningependekeza ya kwamba kuwe na sheria ya kwamba mtu yeyote atatoa mtoto shuleni ili amuo, ashikwe na kushtakiwa. Hiyo itawawezesha, watoto wetu wapate kuendelea shuleni bila kusumbuliwa.

Ya pili, ningependa kuomba Serikali wakati wa Budget, ipatie elimu au Ministry of Education pesa za kutosha ili waalimu waweze kupewa mishahara ya kutosha ili wasifanye business yeyote. Wakipata hizo pesa wataweza kuwafundisha hao watoto wote. Ili shule zote nchini ziwe na usawa.

Jambo lingine, lingelikuwa ni jambo bora kuendelea kujenga shuleni vifaa kama laboratories, kama vile Serikali ilikuwa inafanya hapo mbeleni, kusaidia shuleni ili pia kuwe na ule usawa. Serikali pia ipatie mashule vitabu vya kutosha. Pia, Serikali itoe mabasi, at least kila shule iwe na gari. Ili wakati ambapo watoto wanasoma, waweze kupelekwa sehemu mbalimbali kwa sababu katika masomo fulani kama Geography, lazima watoto watoke nje. Shule nyingi zinakuwa na shida ya usafiri hasa mahali kama hapa, ambapo usafiri ni shida. Pia, shule zipewe stima ili masomo ya computer iweze kuendelezwa.

Pia, kuna shule zingine, unakuta siku hizi mashule yana shida kwa sababu wafanyikazi yaani wale non-teaching staff wanalipwa na shule. Hapo mbeleni, Serikali ilikuwa inapeana pesa, hao wafanyikazi wa shule wanalipwa. Na shule zilikuwa zinaendelea vizuri bila shida. Kama vile hapo nilikuwa nimesema mbeleni, waalimu hasa katika hizi sehemu kame, watumwe wa kutosha. Kusiwe na waalimu wengi, tuseme kama Nairobi, Machakos, Mombasa na sehemu kama hizi, kuwe na shida kwa sababu ni mahali ambapo kuna matatizo mengi ya vifaa. Kuwe na walimu wa kutosha ili kuwe na usawa wa vile watoto wanaweza kufanya shuleni.

Kitu kingine ambacho ningependekeza ni ya kwamba, siku hizi kumekuwa na mikasa mingi katika mashule. Na ingelikuwa jambo la busara kuwe na security hata ingawa shule itakuwa na wafanyikazi wawili, watatu ambao labda hawajahitimu. Lakini

at least, kuwe na security moja ambapo kukiwa na shida kubwa sana huyo mtu ataweza kusimamia hali ya security katika shule.

Kukitokea mikasa fulani fulani, waalimu wakuu wasilaumiwe. Kwanza kufanywe uchunguzi ili Mwalimu asiingizwe katika shida. La mwisho, ningependa kupendekeza, shule zote....

**Com. Bishop Njoroge:** Hawa Wazee wako hapa mbele. Mheshimiwa, tafadhali msifanye makelele. Chief, tuheshimu kikao hiki na yule anayezungumza.

**David Kiumu:** La mwisho, hata ingawa kuna lingine ambalo karibu ningesahau, tuwe na at least clinical officer katika mashule. Huyu atasaidia labda tukiwa na shida kama labda watoto wameanza kushikwa na magonjwa kama S.T.D. hivo anaweza kusaidia. Na pia kukiwa na emergency, labda kumezuka shida fulani, huyo clinical officer anaweza kusaidia.

Lingine shule ziwe na Chaplains. Kuwe na mtu kama Pastor hivi mtu ambaye kwa kweli ataweza kuongoza wale watoto walio shuleni kwa njia ambayo ni nzuri.

Ya mwisho, shule zote ziwe na a strong religious foundation. Sponsors wapewe nafasi yao ili waweze kusaidisha hizi shule ziwe na mwelekeo mzuri ili watoto wetu ambao tunalea, wawe na mwelekeo mzuri ili pia waweze kuwa viongozi wema wa nchi hii wakati ujao. Asanteni sana.

**Com. Lethome:** Unapendekeza au unasema nini kuhusu wanafunzi ambao wako sehemu ambazo zina matatizo (hardship areas). Au pengine entry points zao ni za chini kuliko wale ambao wako katika sehemu ambazo wana facilities nyingi. Sijui unasema nini?

Ya pili, umesema habari ya wale wazee ambao wanawatoa watoto wanaenda kuwauza. Huu ni wakati wa kuzungumza ukweli, kuna waalimu pia wanachafua watoto wa kike shuleni. Sijui ungependa sheria iwachukulie hatua gani waalimu kama hao ambao wanachafua watoto wa kike? And the most that can be done, anafanyiwa transfer from one school to another. Unampatia chance ya kwenda kufanya huo uchafu mahali pengine. Wewe kama Mwalimu Mkuu ungependekeza kitu gani?

**David Kiumu:** Ningependekeza, waalimu kama hao, wachukuliwe hatua ya kinidhamu kabisa kabisa. Mwalimu kama yule asiruhusiwe kufundisha shule ingine. Aende akatafute kazi mahali pengine kwa sababu hao watoto ndio ambao tunafundisha na inatakikana Mwalimu awe kiongozi mzuri. Yaani awe a good role model. Mchungaji wa mbuzi hawezi kuwa ndiye anachukua zile mbuzi anachinja halafu labda anamwambia mwenyewe, 'Oh mbuzi zimepotea.' Kitu kama hicho. Sheria imuchukulie hatua na Mwalimu kama huyu asipelekwe katika shule ingine. Awe dismissed instantly. Awe charged in a court of law. Hiyo ingekuwa ni mzuri.



Lingine, quota system ni sawasawa, mimi naona ni kitu ambacho kinatusaidia. Shule kama hizi ambazo ziko katika mahali pakavu, ingelikuwa ni vizuri, watoto ambao wana points ambazo sio chini sana, waweze kufikiriwa kwenda katika shule ambazo zimeendelea. Kwa sababu saa ingine unakuta kwa sababu ya zile facilities na ukosefu wa waalimu wa kutosha, kuna watoto ambao ni wazuri sana hapa lakini hawafanyi vizuri kwa sababu ya ukosefu wa hizi facilities ambazo nimetaja. Asante.

**Com. Bishop Njoroge:** Thank you very much Mwalimu. Jackson Lokoile. Paul Kinyala.

**Paul Kinyala:** Jina langu naitwa Paul Kinyala.

**Com. Bishop Njoroge:** Utazungumza Kiswahili au Kimaasai.

**Paul Kinyala:** Nitazungumza lugha ya Kimaasai.

**Translator:** Kwa jina ni Paul Kinyala.

**Paul Kinyala:** *Ore ene dukuya naihusu Katiba na eikijo ashe.*

**Translator:** Ninashukuru Tume hii ya kurekebisha Katiba kwa kufika.

**Paul Kinyala:** *Amu eitu aikata kidol katiba na iyiok lopeny enkop.*

**Translator:** Maana hiki ni kitu ambacho ni cha muhimu sana, wenyewe ama wananchi kutoa mapendekezo yao.

**Paul Kinyala:** *Na eikishipa si tene nyaki ashukokino lipeny enkop Katiba.*

**Translator:** Tumefurahia Katiba ikiwa inarudi kwa wenyeji.

**Paul Kinyala:** *Amu kijo oshi enake epuoyi aimaki intokitin eitu eyieu.*

**Translator:** “Namwambia aingie kwa point.”

**Paul Kinyala:** *Ore na engelunoto ena pae e Rais.*

**Translator:** Kuhusu mamlaka ya Rais,

**Paul Kinyala:** *Ole kabila nara.*

**Translator:** Awe wa kila kabila.

**Paul Kinyala:** *Na olonyor iltunganak pooki.*

**Translator:** Tungetaka Rais ambaye anapenda kabila zote.

**Paul Kinyala:** *Na olota si maendeleo.*

**Translator:** Tungependekeza Rais awe ni mtu wa maendeleo.

**Paul Kinyala:** *Amu kidolita ajo ore Katiba edukuya.*

**Translator:** Kwa sababu tulikuwa tunaona Katiba ya hapo mbele,

**Paul Kinyala:** *Na keti wueitin neitu edamuni aitas maendeleo.*

**Translator:** Kuna sehemu ambazo Serikali haijafikiria kuweka maendeleo.

**Paul Kinyala:** *Amu ore maendeleo naleng na orbaribara.*

**Translator:** Sanasana maendeleo kama ya barabara.

**Paul Kinyala:** *Nikidol kulie wueitin neti olami.*

**Translator:** Tunaona sehemu zingine rami iko kila mahali.

**Paul Kinyala:** *Neti kulie pookin wueitin nemeeta.*

**Translator:** Na kuna sehemu katika nchi hii ambazo hazijafikiriwa kuwekwa rami.

**Paul Kinyala:** *Ore enkae toki eare.*

**Translator:** Jambo lingine,

**Paul Kinyala:** *Na enkisuma.*

**Translator:** Ni kuhusu masomo,

**Paul Kinyala:** *Kidol ajo etonyora iltunganak enkisuma oleng.*

**Translator:** Tunaona masomo siku hizi imekuwa ni muhimu sana kwa kila mtu.

**Paul Kinyala:** *Nepikita nkera sukul.*

**Translator:** Na watu wote sasa wamefikiria kupeleka watoto shule,

**Paul Kinyala:** *Kake metumito nkera esiaitin.*

**Translator:** Lakini watoto mara wanapomaliza shule hawapati kazi,

**Paul Kinyala:** *Na ina pidol nkera eti nkuapi enye.*

**Translator:** Na ndio unaona watoto wako nyumbani.

**Paul Kinyala:** *Ore ene uni.*

**Translator:** Ya tatu,

**Paul Kinyala:** *Na ikidolita si ajo ore pe ebaiki kutoka engilisi kiti.*

**Translator:** Kutoka madarasa ya chini,

**Paul Kinyala:** *Mpaka engilasi e isiet.*

**Translator:** Mpaka darasa la nane,

**Paul Kinyala:** *Ikiyieu na pae na peaku pesho enkisoma enena kera.*

**Translator:** Tungetaka hawa watoto wawe na masomo ya bure,

**Paul Kinyala:** *Kake kiomon si mwalimuni.*

**Translator:** Lakini ningependekeza walimu,

**Paul Kinyala:** Ana enikidolita.

**Translator:** Kama vile tunavyoona,

**Paul Kinyala:** *Ore headmaster pookin nakeyiolo wueitin nara.*

**Translator:** Ma-Headmasters wote,

**Paul Kinyala:** *Nebaiki na niche oarita sukulini.*

**Translator:** Tunaona shule zinaharibika kupitia waalimu.

**Paul Kinyala:** *Amu ebaiki nesotu ntoiwo ropiani.*

**Translator:** Wazazi mara wanapotoa pesa,

**Paul Kinyala:** *Ore pesotu nena ropiani.*

**Translator:** Wakitoa pesa,

**Paul Kinyala:** *Nebaiki ne neimin nena ropiani tiatua irmwalimuni.*

**Translator:** Hiyo pesa inapotelea mikononi mwa Mwalimu.

**Paul Kinyala:** *Ore si pinepu ntoiwo eishirita.*

**Translator:** Ukikuta wazazi wanalalamika,

**Paul Kinyala:** *Meta si duo atua nai oladuo mwalimui.*

**Translator:** Unakuta huyo Mwalimu, hakuna hatua Serikali inachukulia huyo Mwalimu.

**Paul Kinyala:** *Naikiyieu si nepaini engoruni pe etum sininye atua hatua nai lelo mwalimuni.*

**Translator:** Tungependekeza waalimu, itafutwe hatua fulani ambayo watachukuliwa mara wanapoharibu shule.

**Paul Kinyala:** *Ore enkae eongoan.*

**Translator:** Ya nne,

**Paul Kinyala:** *Ne esiai naihusu laiguenak.*

**Translator:** Ni kuhusu uongozi wa Chief.

**Paul Kinyala:** *Kiyieu napae ore laiguenak etumi.*

**Translator:** Tungependekeza Ma-Chief,

**Paul Kinyala:** *Na oyiolo nkutukie pookin.*

**Translator:** Ingetakiwa Ma-Chief wanaolewa.

**Paul Kinyala:** *Nikiyieu si neponikini iyiok.*

**Translator:** Na tungetaka Ma-Chief waongezwe,

**Paul Kinyala:** *Pe tenelamisho ninye irmaasai na keiput.*

**Translator:** Maana Wa-Maasai ni watu wa kuhamahama.

**Paul Kinyala:** *Nikidim ashomo enkae kutoto nalakua.*

**Translator:** Ni watu wa kwenda sehemu mbalimbali.

**Paul Kinyala:** *Nemeeta oltungani napayie osaru hata teneari.*

**Translator:** Hata unakuta Chief anasimamia sehemu kubwa, mtu akihama anakaa mbali na Chief.

**Paul Kinyala:** *Na ina pekiyieu neponikini iyiok.*

**Translator:** Na ndio maana tunataka area yetu iongezwe Ma-Chief.

**Paul Kinyala:** *Ore peaku ene imiet.*

**Translator:** Ya tano,

**Paul Kinyala:** *Ne esiai e KWS.*

**Translator:** Kuhusu wanyama wa pori,

**Paul Kinyala:** *Nidolita ajo ore mapato onkera.*

**Translator:** Tunaona mapato ya watoto wetu,

**Paul Kinyala:** *Na kidolita ajo kiti.*

**Translator:** Tunaona mapato ni ndogo sana,

**Paul Kinyala:** *Nemeishorita tadoi iyiok kake iyiok kiti.*

**Translator:** Wanatoa lakini ni kidogo sana,

**Paul Kinyala:** *Na enkop ang si eti nguesi.*

**Translator:** Na wanyama wanakaa kwetu,

**Paul Kinyala:** *Na ekiyieu mpisai neponikini iyiok.*

**Translator:** Tungetaka pesa ya K.W.S iwe mingi.

**Paul Kinyala:** *Na ikiyieu neisho iyiok millionini ongoan.*

**Translator:** Tungetaka kila mwaka milioni nne.

**Paul Kinyala:** *Ore enapayian ana enaimakaki tene.*

**Translator:** Kulingana na vile imezungumziwa hapa,

**Paul Kinyala:** *Kituata tenkaraki nguesi.*

**Translator:** Sisi tumeangamia kwa sababu ya wanyama.

**Paul Kinyala:** *Na ekijo meingorita iltunganak serikali ne wueitin pookin.*

**Translator:** Na tunaona ya kwamba Serikali haiangalii watu.

**Paul Kinyala:** *Amu kumok iltunganak oinosita nguesi.*

**Translator:** Kwa sababu wanyama wanaua watu wengi.

**Paul Kinyala:** *Neitu aikata kining lotalakaki.*

**Translator:** Na hatujawahi fikia malip ile ambayo inalipwa.

**Paul Kinyala:** *Na kiyieu nelakini.*

**Translator:** Na tunataka watu walipwe.

**Paul Kinyala:** *Kiyieu ore oltungani pemoki engues aar.*

**Translator:** Tunataka mnyama mara anapoua mtu.

**Paul Kinyala:** *Melakini milioni imiet.*

**Translator:** Huyo mtu alipwe milioni tano.

**Paul Kinyala:** *Ore enkiteng amu ninye kiasie iyiok kirambeeni.*

**Translator:** Na ng'ombe vile vile inapoumizwa na mnyama,

**Paul Kinyala:** *Na ninye si kishetie sukul.*

**Translator:** Na ng'ombe unajua ndio tegemeo letu.

**Paul Kinyala:** *Ore ake pear enganjai arashu neny a lokuaru.*

**Translator:** Kama ndovu inaangusha ng'ombe, ama simba ikila ng'ombe,

**Paul Kinyala:** *Nelaki elaki nabo onusu.*

**Translator:** Ilipwe kama laki moja na nusu.

**Paul Kinyala:** *Neingori sininche nkishu naasie biashara ekule.*

**Translator:** Serikali ifikirie akina mama, akina mama wapewe nguvu na wapewe uwezo.

**Paul Kinyala:** *Ashe oleng.*

**Translator:** Asante.

**Com. Bishop Njoroge:** John Muthama, akifuatwa na Kennedy Macharia.

**John Muthama:** Naitwa John Muthama kutoka Ilasit. Katiba ile tutatengeneza tukiichukua, isiwe ni kitu ya kubadirishwa na kila mtu wakati anapofikiria. Iwe labda itachukua muda mpaka tena ije kuwa na review.

Muundo wa Serikali: Rais awe ni symbol of unity to our nation. Tunaweza faulu hapa na kuwa, hawakilishi jimbo lolote katika eneo la Kenya. Tumchukue kama mtu wa kuakilisha Kenya nzima. Kwa hivyo hapo hatapigania kiti cha ubunge. Na hapo tena tunaweza kupigana na hizi vyama vingi kwa sababu watu wengi wanaogopa, hakuna mtu atasimama kama Rais ambaye anaogopa anaona chance zake za kupita ni adiri. Vice President, tuwe na Vice President ambaye anachaguliwa na roles zake ziwe zinaeleweka vizuri. Kwa Katiba zilizopita ama zile tumekuwa tukijivunia, tumekuwa na Vice President ambaye haeleweki kazi yake ni nini. Hata wakati labda roles hazijakuwa defined. Hakuna kitu kama Vice President anafanya ni nini. Tungetaka kuwe na Serikali ambapo tuna Prime Minister ambaye atakuwa Head of the Government.

Mawaziri: Ningeonelea ingekuwa na vizuri kama tungekuwa na Mawaziri professionals. Hata kama ingewezekana, hata wangukuwa some of them nominated hata kama sio elected ili tuweze kuwa na Mawaziri ambao wanaelewa. Hawa Mawaziri wamekuwa ni watu wa kutuaibisha. Hata labda ukiwa umetoka nje, hajui saa ingine kile kitu kinaendelea. Wanaulizwa mambo kwa Bunge, hawezi enda kujibu, haelewi ni nini, kinachoendelea. Hawa watu naona saa ingine kama wanatumia pesa zetu bure. Kwa sababu saa ingine alikuwa alichukua a very illiterate Minister ambaye sisi tunaona kama saa ingine wanakuwa tu hapo kula mishahara.

Wabunge wangewekewa kiwango fulani cha elimu. At least a Form Four. Naona kama ni mtu angekuwa anaelewa kidogo. Tusiwe na watu ambao wengine hata labda kuongea kujieleza inakuwa ni ngumu. Mawaziri wa Serikali na senior Government officers na anybody a civil servant, akiwa na scandal yeyote. Kama ametajwa kwa scandal yeyote, kitu cha kwanza iwe ni ku-resign ambapo tunaendelea kumchunguza zaidi kama kweli haya makosa alifanya.

Naona Wananchi tungepatia nguvu kuwa na kitu kinaitwa referendum. Uwezo wa kuondoa labda Serikali kama imeshindwa ku-perform. Wananchi wa Kenya tungekuwa na haki ya kurithi na kuweza ku-own property in any part of this country na Serikali yetu itu-guarantee security ya misitu na maji yetu wakati tuko huko.

Judiciary: Mahakama naona ingekuwa kitu ambacho kiko huru zaidi na isiwe na mtu ambaye anaweza ku-interfere nayo. Ku-influence judgement ambazo zinafanywa huko kortini. Ingekuwa ni hatia hata kama ni Rais mwenyewe anapogusa mambo ya kesi inayoendelea kortini.

Majukumu tunayowapatia watu Serikalini na civil servant ingekuwa inafuatilia, qualifications zake, experience yake na tusiwe tunafuatilia mambo ya ukabila au kwa sababu mtu unamjua. Nomination ya parliamentarians, kunakuwa na watu wengine wana-nominatiwa na Parliament. Naona hili jukumu lingepatiwa special group may be like COTU, labda kunakuwa na group ya

watu, inamtuma mtu wao wa kuwakilisha kule. Lakini hili jukumu naona labda halingepatiwa political partie au labda President au anybody else. Tuipatie special groups in the societies.

Tume-experience tortures mingi na polisi, wakati wanashika watu. Labda unaanzia kuwa tortured na naona kuna sehemu kwa sheria za Kenya inayosema. Somebody is innocent until proved guilty. Sasa hii torture, nafikiri our police force ingeweza kupata training, ijue jinsi ya kuweza kujua kama kweli mtu alifanya jambo au hakufanya badala ya kuenda kwa torture.

Kuwe na free education, Serikali inaichangia kwa budget yake. Tungekuwa also na free medical care. Kwa upande wa biashara labda kungekuwa na free education. Ingejaribiwa kuwekwa kwa kila pahali na kuwe na minimum charges kwa sababu naona baadaye labda itapata tax hapo, it will make money. Lakini saa hii inakuwa ni shida sana, wanaingiza labda a million. Kuweka sehemu fulani watu wafikishe (inaudible) kama wanataka nini. Inakuwa ni vita, watu wanakusanya, mnaambiwa labda mtapewa million, two million na hii kitu naona kama itaturudisha nyuma sana. Kama Serikali ingeweka halafu iendelee kutu-tax pole pole. Naona kama tungefaidika sana.

**Com. Bishop Njoroge:** Thank you very much John. Kennedy Macharia. Joyce N. Peniti.

**Joyce Peniti:** Kwa majina ni Joyce Peniti na ninaanza na education. Education inatakiwa ichukuliwe iwekwe maanani kabisa, zaidi kwa wasichana. Kwa sababu kuna mahali kwingine, makabila zingine kama Wamaasai na Wasomali na Wasamburu hawachukulii maanani kwa wasichana kuenda shule. Kwa sababu wanapenda kusema wanauza wasichana. Iwekwe maanani kabisa na iwekwe sheria ya kwamba kama mtu hajasomesha mtoto anachukuliwa hatua. Hilo ni la kwanza. ‘

La pili ni kwamba, kama habari ya wanyama, wanaumiza watu sana na Serikali haichukulii maanani. Maana kama mnyama ikiua mtu, Serikali haisikii uchungu. Lakini raia akiua mnyama, Serikali inasikia uchungu sana sana. Inatakiwa vile inasikia uchungu kwa mnyama, isikie uchungu kwa binadamu.

Ya tatu ni kwamba Administration iendelee kama zamani. Kwa sababu kama hatuna Ma-D.O au Ma-DC, na Ma-Chiefs, wananchi wataumia. Kwa sababu tukisema eti, Councillor anasimamia mahali ya Chief au mahali ya D.O., mambo itabadilika. Kwa sababu saa ingine, sikumpendelea yule Councillor au sikumchagua lakini nikienda na shida yangu, atanipinga maana sikuwa nimemchagua. Kwa hivyo Administration iendelee kama zamani.

Mahali ya Rais: Rais anatakiwa achaguliwe na akae muda wa miaka kumi. Baadhi ya Councillor, Mayor na Ma-Chairmen, wachaguliwe na raia. Tunapopiga kura, tupige kura kwa njia ya kuchagua Mayor na kuchagua Council chairman. Ni hayo tu.

**Com. Bishop Njoroge:** Asante sana Joyce kwa hayo maoni mazuri. Mletee kitabu. Aminga, can you register her from there? John K. Gichia. Akifuatwa na Samuel Nyaoga.



**John K. Gichia:** Kwa majina mimi naitwa Bwana John K. Gichia. Mwanabiashara wa hapa Loitoktok. Yangu kwanza ningeanza kusema, wananchi wawe huru kuchagua Mbunge wao au madiwani wao. Isiwe ni Serikali ama chama yeyote inayochukua jukumu la kumchagua mtu huko mbele halafu tunakuja tunaambiwa fulani ameteuliwa na Serikali. Awe ni diwani au awe ndio Mbunge wetu, halafu awe labda ndiye atapingana na vyama vingine. Kwa hivyo tunaomba tuwe na haki ya kumchagua yule mtu tunataka ili tumpigie kura yake.

**Com. Bishop Njoroge:** Unamaanisha nini?

**John K. Gichia:** Nataka kusema, panaweza kuwa na ukora wa aina fulani ama ufisadi wa aina fulani, wamchague bila sisi kujua.

**Com. Bishop Njoroge:** Party nominations?

**John K. Gichia:** Party nominations, ndio hizo mimi nataka kumaanisha. Ya pili ningeliza, vitambulisho viwe vikipeanwa mfululizo, isiwe eti kuna siku hazipeanwi, kuna mwezi hazipeanwi. Labda wanajaribu sijui kungojea nini. Kwa sababu kila wakati, vijana au watu wanatimiza ile miaka ambayo inahitajika wachukue vitambulisho. Pia hapo hapo, mambo ya kura, hizi kadi za kura. Zinahitajika pia ziwe zikiendelea kupeanwa mfululizo. Kwa sababu kuna wengi bado watapitwa na wakati. Kwa sababu watasema labda ilikuwa mwezi fulani, alikuwa karibu. Tungeomba iendele mpaka wakati uchaguzi unafika halafu wakati huo ndio inaweza kufungwa.

Upande wa chakula: Nimegusia kidogo tu hapo mambo inayohusu chakula. Yaani bei ya chakula iwe ni bei moja, nchi nzima. Kwa sababu hapa tunauza gunia ya mahindi, shilingi mia tano. Unasikia upande wa Western, inauzwa elfu na mia mbili au inachukuliwa na cereal boards. Hizo boards zetu hapa tumeona zimechukuliwa na watu private na bado Serikali hata hatujui ni nini inafanya kuhusiana na majengo kama ya (inaudible) ambayo iligharimu pesa mingi na haisaidii mwananchi yeyote wa hapa Loitoktok.

Wanasiasa wote kutoka vyama vyote, wanaruhusiwa wapewe idhini au wapewe haki yao ya kufanya mikutano wakati wowote wanaohitaji na pia popote wanapohitaji kufnayia ule mkutano. Hapo wananchi wawe huru na pia wapewe ulinzi mkali ili waelewe ni nini kinachoendelea na nini wanachoelezwa. Mbunge au diwani, tungeomba wawe na kiwango cha elimu. Councillors wawe labda kama form four, kwa sababu ndio ile kiwango ya maana ambayo anaweza elezea watu. Wabunge wanaweza hata kuwa ni University graduates. Kwa sababu hao pia wanaenda wanakutana na Ma-Professors huko, wataweza kuelezana. Tusiwe tunachagua kama ni mtu Councillor, tunaambiwa tuchague mtu hata kama ni wale wanahimiza watoto waache kusoma. Kwa sababu watachaguliwa tu, kwa sababu yeye labda anafaa vizuri, ana kitambi au anaishi na njia yeyote. Naomba mnielewe hapo vizuri. Tungeomba iangaliwe kiwango cha elimu. Kusiwe labda tunachukua mtu Standard one, Standard two, Standard three namna hiyo. Tungeomba Waalimu au madaktari, wasijaribu kutishiwa wanapodai haki zao

walizoahidiwa na Serikali hapo awali. Kama ni mshahara wapewe kwa sababu waliahidiwa. Au kama aliyeahidi aseme alikuwa wapi wakati aliahidi. Kwa hivyo wapewe nafasi wajieleze na wapewe haki zao kwa sababu wakiambiwa watafutwe sababu wanaitisha haki zao, wataletwa wale wengine ambao hawana ujuzi, pia kama madaktari hivo hivo.

Katika upande wa elimu, kuna bursaries ambazo zinatoka kutoka kwa Serikali na tungeomba zipewe watoto kutoka makabila zote wakati zinapogawanywa kwa mashule. Tusiambiwe eti wewe umetoka karibu na Kiambu, upelekewe huko, wewe umetoka wapi upewe huko. Kama ni hapa, wapewe watoto wote wale wanahitajika kupewa ambao hawana uwezo wa kuelimishwa. Wafanyi biashara pia hapa au sehemu zote labda nchini, wananyanyaswa na Serikali ya Wilaya sijui kama ndio wanasimamia upande wa County Councils. Ma-licences inakuwa juu zaidi, watu hawaridhiki hata kama wanalipa lakini wanalipa shingo upande. Kwa hivyo hapo, pia waangalie kama watapunguza. Kwa sababu hakuna kitu tunaongezewa, ile pesa tunaongeza. Lakini hiyo biashara au vitu vina nini.....na soko isiwe huru sana. Wananchi wanaumizwa.

Kuna wafungwa: Wafungwa pia katika nchi tunaona hakuna haki. Unakuta hata kama ni mtu amechukuliwa kama suspect hapa, pahali popote hata kama si hapa. Unakuta anachukuliwa kama tayari amefanya ile kitu na kumbe hata hakuna investigation ilifanywa. Akihukumiwa kufungwa, anateswa, hali ya kutosha au pia wanawekwa kama magunia ya mahindi katika cell. Ningeomba waangaliwe.

Nominated Councillors kama wale labda wataanguka upande huu, waangaliwe kama yule ambaye alikuwa namba mbili kushindwa. Kwa hivyo wasichague tu, fulani kama ni wa DP, upewe DP. Kama ni KANU, lazima wachague nominated kutoka kwa .

Ya mwisho kuna hizi enquiries zinatengenezwa na Rais kila wakati. Unasikia labda mtu ameuawa, enquiries zinaundwa Nairobi, zinakaa miaka sita, sisi tuingojea tusikie baada ya mwaka, inakaa miaka kumi, labda mwingine amezeeka na hatajua ni nini iliendelea. Tungeomba wawe wakichukua huo wakati kwa muda mfupi na kutupatia ripoti haraka.

Mwisho, ningesema....

**Com. Bishop Njoroge:** Katika sheria iliyoko ni kwamba Commission za Enquiries, Rais amepewa mamlaka, ikiwa kuna kitu anataka kujua kwa ajili ya Serikali yake, anaweza kuitisha Commission of Enquiries, na sheria haijasema ni lazima awaambie wananchi. Isipokuwa mpende hiyo sheria iondolewe. Lakini kulingana na sheria iliyoko, hana wajibu wa kutuambia amepata nini. Kwa hivyo ni juu yenu kusema, tunataka ikae au isikae. Lakini sio makosa yake kwamba hakusema. Kwa sababu sheria inamruhusu kufanya nini? Kufanya hivyo.

**John K. Gichia:** Nilikuwa nikisema, kuliko labda kuna ripoti tunangoja tusikie mahali alifanya kitu fulani. Isichukue miaka mingi.

**Com. Bishop Njoroge:** Kwa hivyo ungetaka ikae au iondolewe?

**John K. Gichia:** Enquiries zindelee lakini zisikae muda mrefu.

**Com. Lethome:** Matokeo yake, ungependa yatangazwe kwa watu ama iwe siri ya Rais?

**John K. Gichia:** Hatutaki iwe siri ya Rais. Kama ni mambo kama kifo cha Ouko, ambao watu wengi walilia kujua. Hatukujua nani aliuu? Labda mpaka saa hii wanajua. Tungependa tuwe tukiambiwa wazi.

Ya mwisho, nasikia kuna watu wanasema mambo ya Administration iondolewe kama Chief. Mimi ningeonelea Administration yote, ikae hivo hivo. Security pia ambayo iko nchini, iendelee hivyo hivyo. Kwa sababu sioni sababu uondoe Chief. Labda anayelalamika Chief aondolewe, labda ni mkatili katika eneo lake. Kwa hivyo naomba Administration ikae hivyo hivyo. Asanteni.

**Com. Bishop Njoroge:** Asante John. Tupate Samuel Nyaoga. Medingi Ole Mlaroni. Karibu Mzee. Taja jina lako kwanza.

**Medingi Ole Mlaroni:** Mimi kwa majina naitwa Medingi Ole Mlaroni. Mimi ni Mzee ambaye anaishi sehemu ya Ole Leti, katika sehemu za Rongai. Mimi naeleza mapendekezo yangu; ya kwanza napendekeza Raisa awe na uwezo wa kusimamia Kenya mzima. Halafu pendekazo la pili, ninapendekeza ya kwamba, Kenya iwe na Serikali ya Majimbo lakini iwe Rais ndiye anasimamia wote.

Pendekazo langu la tatu ni kwamba katika sehemu ya Wa-Maasai. Kuna sehemu nyingi imeenda kama Amboseli. Kama sehemu hiyo ambayo ilikuwa inaitwa Tsavo. Irudishwe iwe mikononi ya wenyeji.

Jambo lingine la tatu ni kwamba masomo katika sehemu ya Wa-Maasai inakuwa dhiifu kidogo. Ningeomba Ma-Chief wapewe nafasi, kabisa waweze kuwa na sheria ya kusema watoto wapelekwe shuleni. Kwa sababu tunaona masomo siku hizi ndio kitu kikubwa ambacho unaweza kumuachia mtoto wako. Kwa hivyo Ma-Chief, mimi napendekeza Ma-Chief wachukue sheria hiyo, iwe ni sheria katika nchi ya Wa-Maasai ama katika Kenya.

Jambo lingine Councillors: Ma-Councillors ambao wanachaguliwa katika Kenya, wao wenyewe wanachukua madaraka yao na hakuna kitu anaweza kuwapa wananchi sawasawa kulingana na vile inatakikana. Iwe plots, Councillor awe na kamati yake, ambayo inatoka katika ile eneo ambayo inasimamia Ward yake ili wakae na kugawa zile plots. Isiwe anakuja na agawie watu wale anawapenda. Anaweza kuwa anagawia ndugu yake ama anagawia mtu ambaye alikuwa rafiki yake. Kwa hivyo tunataka Councillors wawe ni watu ambao watakuwa na kamati ambayo itasimamia plots.

Ma-Chiefs: Nafikiri Ma-Chiefs, ninaweza kusema ya kwamba Ma-Chiefs wakae vile walikuwa wakikaa na wawe ni wale Ma-Chiefs ambao wamechaguliwa katika ile sehemu ambayo wananchi wamezaliwa hapo. Awe ni wa hapo. Sio kwamba tunaweza kupendekeza iwe eti ni watu wa kwenda transfer. Hiyo hapana na sasa wawe ni wale ambao ni wananchi katika ile sehemu. Kwa hivyo kwa hiyo ninasema asante sana, sina mengi sana ila tu, niongeze ya kwamba, Serikali ibadilishe hayo mambo kwa njia ambayo inafaa. Kwa hivyo asante sana, mimi sikuwa na mengi.

**Com. Lethome:** Asante sana. Jiandikishe. Daniel Molunkei.

**Daniel Molunkei:** Kwa majina naitwa Daniel Molunkei, mkaaji wa Loitoktok. Kwanza ningependa tu kuzungumzia mambo ya Administration. Kwamba Administration ibaki vile vile na kuwa na PC, DC, hadi ngazi za chini za Chiefs, na Assistant Chiefs. Ila tu, ni kwamba iangaliwe Review Act ya uajiri wa Ma-Chiefs kwa kuwa tunaona ya kwamba wakati wakitangaza kuajiriwa kwa Ma-Chiefs. Unakuta ya kwamba hawafuati ile sheria, wengine wengi hapa katika eneo hili letu ni kwamba tumechaguliwa Ma-Chiefs ambao hata hawajui kuandikia mkubwa wake Bwana D.O. ripoti, ambao ni aibu kubwa sana. Sijui hiyo sheria mchunguze muangalie ni wapi kumekosewa. Kwa upande wa Ma-Chiefs pia, tungelipenda sheria ile ya zamani ya miaka zilizopita ya kwamba Ma-Chiefs wawe wakichaguliwa na raia wao katika eneo lao.

Lingine ni mambo ya masomo, limezungumziwa zaidi lakini kwa upande wangu na maoni yangu, ningependa tu kwa mambo ya marks. Ya kwamba irudishwe ile sheria ya zamani ya kujaribu kuangalia zile remote areas na marks za watoto wa remote areas an wale amao wanaishi katika rural areas zipandishwe. Isiwe mtoto anafanya K.C.P.E na marks zake zitakuwa ni sawa na yule ambaye ako Nairobi. Kwa upande pia ya waalimu, itafutwe sheria ambayo ilikuwa hapo awali. Sijui imepotelea wapi, ya public funds mis-use ambapo Ma-Headmaster wengi wametumia fedha za shule na shule kuadimika. Na nafikiri hiyo ndio imeleta shida nyingi ya hapa watu wengi wanaanza kusema mashule na vitu kama hizo. Turudishe zile sheria za zamani.

Mambo ya health: Health pia tungeliomba iwe completely free kama zamani ila tu in-patients waweze kulipa yale madai kidogo tu ya kitanda. Lakini kila kitu mpaka madawa iwe ni huru. Pia sheria iangaliwe ya kuanzisha mambo ya clinics, hizi private clinics. Imekuwa kwamba watu wegini wameanzisha tu private clinics. Unakuta ya kwamba kuna mtu ambaye yeye ni daktari mkuu na ameruhusiwa katika ki-profession na sheria lakini anatumia watu wengine ambao sio professionals wa kuweza kuendeleza ma-private clinics. Kwa hivyo tungeliomba sheria hiyo ya Ministry of Health, iangaliwe kwa maakini kwa sababu tuna mahospitali ambazo ni duni na kulingana na mambo ya utajiri ama mambo ya kipekee tuna shida hizo.

Ya pili ni mambo ya K.W.S., ningeliomba sheria za zamani ziweze kuwa kwa sababu K.W.S. ni parastatal na sheria za wanyama wa pori ambayo iko katika Ministry of Tourism, iangaliwe irudi hasa kwa upande wa compensation. Compensation tulikuwa tunalipwa fedha na nafikiri kulikuwa na sheria ambayo ilikuwa imewekwa. Hapa mtu akiuawa na wanyama kama vile wale wa mbele walisema hakuna fedha ambazo wanalipwa. Mashamba hailipwi.

Ya pili kwa upande wa tax: Zile pesa za tax, kuna pesa ambazo Serikali ilikuwa imepitisha kitambo, ilipwe wale watu ambao wako katika eneo la... wako jirani na eneo la game reserve na national park. Kwa sababu watu hawapati. Ya pili, ni mambo ya school bursaries, school bursaries tunazungumzia pesa zinazopatikana kwa National Parks, gate fee. Imekuwa ya kwamba every National Park within Kenya ni kwamba itasaidia wale watu wako kwa community. Lakini haikuwi hivyo.

Tungelipenda sheria iangaliwe vizuri kwa sababu zile pesa ambazo zinapatikana kwa kila National Park, hazisaidii wale wenyeji wa eneo lile. Wanapeana 1% badala ya kupeana nusu kwa nusu ambapo ingesaidia the local people around the National Parks and Game Reserves. Amboseli National Park, Chyulu Hills National Park, Tsavo West National Park, tungeliomba ile sheria ya 1952 ambayo ilikuwa imewekwa kwamba hawa ni wenyeji, irudishwe na iangaliwe kwa sababu hawakuuza. Hakuna sehemu ambayo wazee walikaa katika eneo hilo na waka-sign kwamba Serikali imechukua hiyo sehemu kama National Park. Waulizwe tena na iwe reviewed. Tujue ni kwa nini hiyo area ilienda na hatujui ni kwa nini. Kwa hivyo tungeliomba na tunahakikisha ya kwamba sisi Wa-Maasai wa eneo hili pamoja na Maasai Mara na Wataita kutoka Tsavo West, tumeanza (inaudible) sanctuaries zetu, kuonyesha Serikali ya kwamba tuna uwezo wa kuweza ku-manage our national reserve and tax irudi kwetu.

Elected Councillors: Elected Councillors and Chairmen should be elected by the people themselves katika grassroot. Nominated Councillor mimi ningeonelea kwa maoni yangu ya kwamba hatuoni kazi ya nominated Councillor tukiwa na elected Councillors kwa sababu wamechaguliwa na sheria ya elections. Kwa sababu hawa nominated wanachaguliwa na wanachama, wanachaguliwa na MP wa area hiyo akikupenda. Kwa hivyo nominated Councillors out. Wale ambao wamekuwa elected na Election Commission iwe hivyo. Pia hapo wachukue tu miaka mitatu na waweze kubadilishwa. Asante.

**Com. Bishop Njoroge:** Unajua kuna shida kwa sababu akina mama, wengi hawachaguliwi Bunge. Kuna watu kama disabled ambao hawawezi kuingia Bunge, kwa sababu hawezi kufanya campaign kama wale wengine. Hutaki tuache nomination kama iingie special groups? Hiyo itaweza kuwa namna gani?

**Daniel Molunkei:** Nafikiri kulingana na sheria kwa upande wangu mimi. Nafikiri mtu yeyote ambaye huwa elected ni kufanya siasa zake. Nimewahi kuona Kenya mtu ambaye hana miguu na ametembea na amekuwa Mbunge. Kwa hivyo sijaona sababu mtu yeyote kusemekana ni mlemavu na anataka kuwa Mbunge ama Councillor. Kwa hivyo kwa upande wangu, mtu ambaye anataka kuwa amechaguliwa, kuna ile sheria ambayo iliwekwa. Kuna sheria ambayo ilikuwa imewekwa. Kwa hivyo sio sababu ya hiyo. Kama kutakuwa na special groups, kwa upande wa watu wowote. Basi itatangazwa. Kutakuwa na special ambapo kila mmoja ana uwezo. Kwanza siku hizi akina mama ndio wako na nguvu zaidi kuliko wanaume. Ni wengi zaidi.

**Com. Bishop Njoroge:** Wacha tuongeze kidogo. Katika ile Act ambayo inaongoza Commission hii, inasema kuna kitu inaitwa National Constitutional Conference na hiyo ndio itaamua ile ripoti ambayo tutaandika iwe Katiba. Katika hiyo National

Conference inasema, lazima iwe na watu watatu kutoka kila district na hiyo Act inasema specifically, mtu mmoja ni lazima awe mama. Tulipokuwa tukichagua committees za constituencies, Act ilisema 1/3 wawe akina mama. Kwa sababu mara nyingine akina mama.....kwa hivyo unasema hata akina mama wapigania uongozi?

**Daniel Molunkei:** Sawa.

**Com. Bishop Njoroge:** Sawa. Stephen Kariuki. Charles Kimani.

**Charles Kimani:** Majina yangu ni Charles Kimani na nina maoni yafuatao. Kwanza ningependekeza kuhusu ukulima. Kwa wakaaji wa hapa, tunapata shida nyingi sana kuhusu ukulima, tunashindwa mavuno yetu tutayapeleka wapi kwa sababu hakuna ready market ambayo tunakuta iko. Especially kama cereals board ambayo tuko nayo hapa, inafaa kuwa under long run. Lakini unakuta iko under short run. Ningepomba Serikali iangalie kuhusu jambo hilo.

La pili, ni taxrate. Unakuta taxation rates ziko juu sana kwa wananchi wa kawaida ambaye ukijaribu biashara yako ndogo ndogo, huwezi faulu. Kwa hivyo ningeponelea Serikali pia to consider that point.

Pointi ya mwisho ni kuhusu job opportunities. Kazi zingefaa zinagawanywa kulingana na elimu na experience yako. Unakuta kama ni job opportunity mahali imetokea, unakuta the people who are there, hawafai kufanya ama hawana experience. So, that point also to be considered. Ni hayo tu.

**Com. Bishop Njoroge:** Thank you very much Charles. Thuo Chege? Akifuatwa na Masalia Ole Kima. Masalia Ole Kima yuko? Na Saitoti Ole Maniki. Saitoti yuko? Patrick Maina yuko?

**Thuo Chege:** Kwa majina ni Thuo Chege. Maoni yangu kuhusu Katiba ni kwamba national resources ziwe zikisaidia, 75% ya mapato ambayo itakuwa ikipatikana kwa national resources iwe ikisaidia watu wa ile area yaani locals.

Land: Kuhusu schemes na land ambayo imekuwa ni ya Government, inapaswa ku-sub-divided ili any citizen ambaye ni eighteen years ambaye ametoka pahali land hiyo iko na kama land inapatikana, igawanywe kulingana na vile iko. Wasted land: Kuna mashamba mengi wasted. Kuna watu wako na kama ekari elfu tano na hawazitumii. Katiba ingebuni njia, watu wawe wakipata, wale ambao hawajatumia hiyo land, Serikali iwang'anye iwe utilized kwa wale wako as citizens. That is, it should be reduced.

Powers za President zinapaswa kuwa limited, kama appointment of Judges na Commissions zinapaswa kuwa kwa raia. Quota system....

**Com. Bishop Njoroge:** I beg your pardon. Judges wawe wakichaguliwa na raia?

**Thuo Chege:** Wawe wakichaguliwa na Judicial groups kutoka kwa nini.... Quota system kwa upande wa kazi, sioni kama ina maana kwa sababu ina-promote illiteracy na vitu zingine ambazo ni incompetency kwa kazi. Kwa hivyo tunapaswa kuwa criteria ambayo tunapaswa kufuata kwa kuchagua watu, inapaswa kuwa ni merit. Interviews mimi naona, interviews zingefanywa away with kwa sababu kama wewe huna godfather hutapata kazi, basi you should send your certificates kwa wale wanachaguana sio personal presentation. Kwa sababu ina-promote kwenda kinyume cha sheria.

Uuzaji wa Parastatals, haupasi kuwa unafanywa kabla haujakubalianwa na watu wote. Parastatals zinapaswa kuuzwa na citizens. Kwa hivyo uuzaji wa Government owned houses, zisifanywe hivyo hivyo local local. Zinapaswa kuwa nini...

**Com. Bishop Njoroge:** Thank you very much Thuo. Patrick Maina.

**Patrick Maina:** Kwa majina naitwa Patrick Maina na maoni yangu ama pendekezo yangu ni juu ya land distribution countrywide. Kusiwe na mambo ya ethnic groups, yaani ardhi igawanywe ili tuweze kuleta mambo ya ukulima ili tupunguze umaskini nchini. Mambo ya wildlife, kuna mahali ambapo ni suitable for wild animals, isukumwe huko na mahali ambapo kunafaa kilimo watu wagawiwe. Ndio tusiwe na mambo ya kuomba omba chakula nje. Mambo ya education, kwa ofisi kuwe na watu waliosoma. Sio biashara ya kusukumia watu ambao hawajasoma kwa sababu ya godfathers. Kama kwa mfano kwa ofisi ya D.O's kuwe na watu graduates. Kama vile kwa njia moja ama nyingine tumekuwa na manufaa kwa wale ambao wamesoma kwa sababu wanakuwa na techniques za ku-solve za watu yaani za wananchi wa kawaida.

Mambo ya elections, ama mambo ya Chiefs wawe wanachaguliwa na raia na wawe na makamu. Hii biashara ya kusukumia Ma-Chiefs ambao ni vijana ambao hata ukiwapelekea kesi za mababa zao, ku-solve enyewe inakuwa ni kazi. Kwa hivyo ni vizuri kuwe na umri. Umri wa kwanzia miaka hamsini kuenda juu mpaka miaka themanini na tano.

**Com. Lethome:** Chiefs wawe from fifty to eighty five years?

**Patrick Maina :** Yes. Mambo ya nomination. Kusiwe kuna-nominatiwa MPs, Wabunge ambao wamekataliwa na watu. Kwa sababu yule mtu amekataliwa halafu anarudi anasukumiwa nomination, na huku raia hawamtaki. Kuwe kunachaguliwa mtu ambaye alikuwa neutral ambaye anaonekana ana knowledge ya kuongoza.

Mambo ya powers kwa Parliament, nayo isiangaliwe eti mtu ni wa chama gani. Hii iwe kwa Serikali, ichukuliwe ya kwamba, Mbunge akishachaguliwa basi distribution ya finance kwa constituency iwe equal. Sio biashara ya kusukumwa kwa sababu chama fulani ndio imeshinda, ndio anasukumiwa anapendekeza maendeleo mahali pale ndio aweze kuchaguliwa the next election. Kwa hivyo mambo ya distribution ya finance, iwe kwa kila Mbunge.

Mwisho ni juu ya polisi: Mamlaka ya polisi kuna mahali ambapo imekuwa torture. Mambo ya kupigwa kwa raia, unakuta hata



mtu hajafanya makosa lakini ile vita anapigwa inabidi akubali mambo mengine. Kwa hivyo ni vizuri ingewekwa sheria, tusiwe na biashara ya watu kupigwa kupigwa. Mtu awe na uhuru wake wa kusema yale mambo anayoyajua. Kwa sababu katika ile criteria ambayo wanawekwa, kuna njia ile wamefundishwa ya kujua mtu kama amefanya makosa ama hajafanya makosa. Kwa hayo, nasema asante.

**Com. Bishop Njoroge:** Patrick, hata kupigwa ni biashara. Karibu hapa. Au ni lugha ya siku hizi, unajua bado tunazeeka. Tupate Christopher Wakaba, ameenda? Kenneth Manyeki? Joyce Senewa? Julius Kamwanga? Mkumbuke nilisema tusifanye kelele kwa sababu hatutaki hii recording ichukue makelele tafadhali.

**Julius Kamwanga:** Mimi ni kama vile mlivyosikia, naitwa Julius Kamwanga na ningependa kuanzia na kule juu kabisa, the Executive. Hii ningependelea Rais wa nchi hii, awe amechaguliwa na raia wote lakini awe na mamlaka kidogo. Awe ndio amri mkuu wa jeshi na awe ndio baba wa taifa. Makamu wa Rais pia awe wakuchaguliwa na raia. Halafu chini ya hao, tuwe na Executive officer wa Serikali ambaye atakuwa Prime Minister, ambaye huyo atachaguliwa na Wabunge. Wale ambao watachaguliwa kufika Bungeni, watuchagulie Prime Minister ambaye ndiye ataunda Serikali kule.

Jambo la tatu ningependea Ma-Councillors wateule, sioni maana yao. Ningependa hiyo kitu iondolewe kabisa, wale watu ni pesa za raia tu wanakula bure. Halafu wabunge wateule, ningependekeza kama vile wale wengine walivyopendekeza ya kwamba, ipewe special groups, kama walemavu, akina mama, vijana na wasiwe na nguvu ya kupiga kura Bungeni. Kazi yao iwe ni kwenda tu kunena na kushiriki katika ule mjadala lakini ikifika kupiga kura, wasipige kura kwa sababu hawana mamlaka ya kuchaguliwa na yeyote yule. Kwa hivyo watakuwa wameteuliwa na zile groups ambazo zitakuwa zimewateua. Na ningependa hiyo group iongezwe kutoka wale kumi na wawili, mpaka ifike arobaini na nane.

Ningependa pia kupendekeza ya kwamba, baraza la mawaziri, isiwe tu wanaangalia wale watu wameenda bungeni. Maanake tunaweza kuwa na watu kule bungeni ambao hawana elimu ya kutosha. Kwa hivyo huyu Waziri Mkuu ama Prime Minister apewe uwezo wa kuteua mtu yeyote bora anaweza kuendesha wizara. Ningetaka pia hapo kuja kwa makatibu wakuu. Pia makatibu wakuu lazima kama ni wizara amepewa wizara tuseme ya ardhi ama ya ujenzi, awe taaluma yake ni ile. Kama ni Waziri wa afya ama wa elimu, lazima iwe taaluma yake ni ile, kwa sababu kama sio hivyo, tunakuwa na watu wengi ambao wanaenda kujaza maofisi bure. Makatibu wa kudumu.

Jambo la tatu, ningependa kupendekeza, kukitokea shida pengine Rais, amekuwa mgonjwa ama kwa bahati mbaya, unajua ni mwanadamu kama wale wengine afariki, sioni haja ya mwanasiasa mwingine kusimamia Serikali kwa ile miezi mitatu, zile siku tisini. Ninaona hilo jukumu lipewe hakim mkuu, Chief Justice, ashikilie kwa sababu atakuwa hana upendeleo wa upande wowote. Na yeye iwe Katiba pia imemzuia kutokuwa na tamaa ya hiki kiti. Ashikilie mpaka siku zile kipindi kikisha, aitische uchaguzi na ahakikishe ya kwamba ameendeleza huo uchaguzi mpaka wakati wake uishe.



Sasa naenda upande wa elimu. Upande wa elimu, ningeomba elimu iwe ya bure, na faini kubwa zipigwe wale watu ambao wanapeleka madawa ya kulevya mashuleni na pia wale ambao wanaoa wasichana wadogo ambao umri wao ni mdogo. Wanaoa ama kuwaoza watoto wachanga. Ningependa pia upande wa afya, hii National Hospital Insurance Fund haisaidii. Ningependa iwe re-structured. Instead ya hii kitu kuwa ina-expire baada ya mwaka mmoja, iwe reduced kwa sababu tunachangia, unakuta mtu amechangia mpaka kifo chake na hajawahi kufaidika na huu mfuko. Kwa hivyo ingefaa hospitali zote za Serikali, ndio hii kitu iweze kusaidia watu wote, ziwe zimeandikishwa kwa hii nini, na ziwe zinapata zile fedha ndio wale watu wako katika maeneo yote ya Kenya waweze kufaidika.

Ningeomba pia Tume hii iangalie juu ya walemavu. Tuna walemavu wengi wako manyumbani. Iangaliwe vile watakavyopata elimu bora, afya bora na pia waangaliwe kwa upande wa kazi, kwa sababu hawana uwezo wa kwenda kujitafutia na kuna wengine wana elimu ya kutosha ya kuweza kufanya kazi mahali popote. Kwa hivyo nashukuru sana.

**Com. Bishop Njoroge:** Thank you very much Julius for those very good points. Tupate Daniel Somoire na atafuatwa na Shadrack Ole Lapi.

**Daniel Somoire:** Mimi kwa majina naitwa Daniel Somoire na nafikiri nitapeana haya maoni lakini pia niko na written memorandum ambayo nita-present baadaye. Nikianza mambo ya Serikali, kwa maoni yangu naona ni afadhali kuwa na Serikali ya Majimbo, federal system. Lakini tukisema federal system, haimaanishi Serikali ya ukabila ama kuwa na majimbo ya ukabila, inamaanisha tu majimbo ya wale watu, vile watu wamekaa. Na inamaanisha mapato ya hilo jimbo, iwe ikiwa-controlled locally. Kwa sababu Central system of Government, inafanya resources za nchi zitumie kulingana na ule uongozi uko wakati huo. Nafikiri Wakenya wengi wanajua, mambo ya, tukule kwa sababu huu ni wakati wetu. Lakini hiyo mali ni yetu wetu. Lakini tunakula kwa sababu ni wakati wetu wa kula hayo matunda. Na naona ikiwa de-centralized tuwe na federal system, mwananchi wa kawaida atakuwa na usemi katika matumizi ya natural resources za nchi. Katika hiyo federal system, tungependelea tuwe na Prime Minister ambaye ndio anawajibika Ki-Serikali, Bungeni, kila wakati na ndio in control ya cabinet na pia awe na deputy yake.

Mimi kwa maoni yangu ninaona system ya Provincial Administration ingeondoka. Kuondoka kwake haimaanishi ni wale individuals ambao hawatumiki, ni system yenyewe. We have very good officers, wawe absorbed kwa departments zingine za Serikali. Kitu kama Administration police wawe absorbed katika police force. Kwa sababu ukiangalia nchi zote independent, ni vigumu sana ukute nchi iko na Provincial Administration ambayo iko independent. Wale elected leaders, Councillors watachukua role ya Ma-Chiefs. MPs watachukua role ya constituencies zao na tukiwa na federal system of Government, governor ama whichever title atakuwa akipewa, atakuwa in control na atakuwa pia local. Kwa hivyo ninaona kama Provincial Administration ilikuwa chombo cha ukoloni. Ilichukuliwa ya kwamba hatuwezi kuji-control kwa hivyo lazima tuwe-controlled.

Tukija kwa mambo ya ufugaji (Pastralism). Nafikiri tunafahamu wote, ma-agreement, wafugaji walifanyiwa hapa Maasai kutoka

1904 na 1911 ambayo Serikali ya ukoloni ilifanya treaties ya kunyang'anya Wamaasai ardhi yao. Hizo treaties zilifanywa na watu ambao hawajasoma na Mzungu amesoma na wale Wa-Maasai hawajasoma. Wakapeana ardhi ya Wa-Maasai ikaenda yote. At least, nchi kubwa ya Wa-Maasai ilienda wakati wazungu walichukua. Nayo successive Government, independent Government, hazijatafuta maarifa hata kidogo ya ku-compensate Wa-Maasai kwa kile walichopoteza miaka hiyo. If anything, they continued following the same system of marginalization.

**Com. Bishop Njoroge:** The history we know, can you recommend what should be done please.

**Daniel Somoire:** So, what I recommend is that, there should be a deliberate mutual\* plan in promoting the lifestyle of pastoral people. There should be recognition that pastoralism is an economically viable lifestyle. There should be a Ministry that specifically deal with pastoral issues. The mutual plan which should be put in place should allocate a percent, I propose twenty percent of the national budget towards pastoral community. It should be a mutual plan for between ten to fifteen years. That the Government focuses deliberately its efforts in pastoral areas.

Jambo lingine ni jambo la ardhi, just the way pastoralism is dismissed by our Government, so is the policy of our land and pastoral areas. Watu wengi wanaona ile ardhi huko inasemekana ni idle land, lakini area ya wafungaji inahitaji ardhi kubwa na si idle kwa sababu ina-sustain life ya watu wengi. Kwa hivyo tukiona area haijalimwa, tusione kama ni idle. Ni ile ambayo inabeba maisha ya watu wengi na vile mnavyojua mambo ya ufugaji inahitaji ardhi kubwa. Ng'ombe inahitaji ekari mingi lakini watu wengi wa kutoka hapa Nelias, wakiona sehemu ile wanaona kama hiyo ni idle na pia tungependekeza, ardhi katika sehemu hizo, isiwe sub-divided into unreliable units.

Lazima Serikali iwe na mechanism ya kusema, 'usigawanye ardhi kavu mpaka kiwango ambacho haiwezi kuwa productive tena.' Kwa sababu ukigawanya sehemu kama Legisini kwa mfano, mpaka eka tano, sijui mtu ataishi huko namna gani. Kwa hivyo ni lazima kuwe na policy ya Serikali ya kuangalia ardhi kavu, inafaa igawanywe mpaka kiasi gani halafu Serikali iseme, usigawanye zaidi ya hapo.

Jambo lingine ni mambo ya Natural Resources: Tukiona mambo ya Natural Resources hapa vile ziko sehemu kavu ama semi-arid areas, unaona ni kama rip off tu, unaona kama Serikali inachukua hiyo mali yote, inaenda kusaidia Central Government. Ni kama for example, tukiangalia mambo ya wanyama wa pori, wildlife. Unakuta wildlife ama tourism ambayo mara ingine inakuwa leading foreign income earner. Lakini watu adjacent to the National Parks, hawawezi ku-afford hospitali, hawezi ku-afford masomo.

Kwa hivyo tungependekeza, management ya Natural Resources particularly wildlife iwe localized. Kwa hivyo Amboseli National Park for example irudi katika Kajiado County Council ili iwe manufaa kwa watu wa Kajiado badala iwe tu ni mahali Central Government inapata faida na wenyewe wanaumia. Na zile communities zinadharau hizo national parks, lazima ijulikane,

they are foregoing some costs for co-existing with wildlife. Therefore, priority should be given to ploughing back some of the income to the local community. Because there is a cost of sustaining wildlife. Wildlife should justify its existence in this area. Kwa hivyo tunaona community ambayo inakaa na wildlife iangaliwe kwa sababu saa hii ni kama tunachukuliwa kama tuko sawa na hawa wanyama. Wacha waishi vile wanavyoishi lakini unaambiwa three hundred million, two hundred million imepatikana kutoka Amboseli lakini mtu wa hapa hata hapati maji ya kunywa.

**Com. Bishop Njoroge:** I have already given you eleven minutes. I will add you one more.

**Daniel Somoire:** Thank you. Pia katika system ya Local Government, ninge-propose Local Government election date yao isiwe ina-tally na ya National Assembly. Kwa sababu unakuta vile watu wana-collude kushikana Councillor na Mbunge, mtu anafaa awajibike kivyake so it sounds like we are not electing a lineup of candidates for the Local Authority and Parliament. The election time should be separated. Thank you very much.

**Com. Bishop Njoroge:** Thank you very much Daniel Somoire. Shadrack Lapi na atafuatwa na Ntumei Ole Mwenda.

**Shadrack Lapi:** Asante. Nitaongea kidogo tu maana sina mengi. Enyewe watu wameongea mengi mengi tu lakini hapa nikiongeza si makosa ama nikisema si makosa. Watu waliongea habari ya Ma-Chiefs ya kwamba hivi na hivi, Chief inatakiwa awe. Haiwezekani kukaa bila Chief. Chief anatakiwa awe. Lingine la pili kutoka hilo, inasemekana habari ya Rais na nini na nini, huwezi kupewa ofisi na usipewe mamlaka. Ukiwa katika ofisi, kama sasa nyinyi mnakaa hapa, labda una mamlaka fulani, na yule ofisini apewe mamlaka yeyote. Apewe mamlaka na apewe ofisi. Lingine la tatu nikitoka kwa hiyo, ni habari ya hospitali.

Tukiongea habari ya hospitali, maneno mengi mengi iko ndani. Na tukiongea hapa hivi tunaanza kuonekana ya kwamba tunafanya kama fitina. Matibabu ya hospitali tupate ya bure. Shule pia ni hivo hivo. Tuwe na elimu ya bure. Lingine la nne nikitoka kwa hiyo, ni Amboseli area. Amboseli hapo mbeleni ilikuwa ni yetu. Irudishwe katika Local Government na iwe wananchi nao tufaidike na mali ya nchi yetu.

Majimbo: Tunataka hii nchi iwe ya majimbo. Yangu imeisha. Asante.

**Com. Bishop Njoroge:** Shadrack umesema mambo mengi ya maana kwa muda mfupi. Asante. Tupate Ntumei Ole Mwenda. Wapi Chief? Utaongea kwa Kiswahili? Na useme jina lako.

**Ntumei Ole Mwenda:** Eeh. Mimi naitwa Ntumei Ole Mwenda. Sina mengi, nasema nataka machifu wakuwe. Ya pili, tunataka masomo iwe ya bure. Ya tatu, hatutaki wale waalimu inasemekana wanatoa watoto shuleni haswa wasichana. Na hao wasichana warudi shuleni na hao waalimu wachukuliwe hatua kali. Sina mengi.

**Com. Bishop Njoroge:** Asante sana. Tupate Maeleshi Ole Ntwasa. Joshua Gathegi. Amina Abdullahi. Anafuatwa na David Toniki. David Toniki yuko? Ibrahim Kailepi? Yuko?

**Amina Abdullahi:** Kwa jina mimi ni Amina Abdullahi na ningependa kuzungumzia habari ya wamama. Urithi wa wamama, usiingiliwe na familia ama late husband's brother. Mali yake isimamiwe na mama na watoto wake. Ya pili, girl-child education. Lazima tuzingatie girl-child education chini ya miaka kumi na tano, kuo msichana wa miaka hiyo, ashitakiwe na sheria. Economy of land and natural resources: Development ya economy, lazima 10% ama 20% iwe inajulisha akina mama.

Pesa za umma za Serikali: Lazima pesa za umma zijulishwe umma na isitumiwe kwa kuibiwa ama kutumiwa ovyo ovyo. Kila umma itumiwe. Ziwe certain groups, wachaguliwe kama private, wasuluhishe pesa zao vile wataweza kuzitumia. Public and private land need to be based on a clear framework.

Culture: Utamaduni wetu sisi Waafrika tusiwache hasa kwa upande wa wasichana, tohara yao, kila mtu ana tabia yao. Maasai, Somali, Samburu, lazima ipitie kwa elders. Thank you.

**Com. Bishop Njoroge:** Asante sana Mama Amina kwa maoni hayo. Ibrahim.

**Ibrahim K. Kailepi:** Mimi naitwa Ibrahim Kailepi kutoka eneo ya Lasiti. Maoni yangu; Rais achaguliwe na umma. Rais akija aweke (inaudible) yeyote ya nchi yake, wananchi wapewe nafasi ya kuuliza maswali Rais. Watoe maoni yao mbele ya Rais. Kwa sababu Rais akija tu hivi, raia aruhusiwe kusema nia yao mbele ya Rais. Tena, pahali kuna vyama vingi, inaweza kuwa mwenye chama fulani ana maoni ya kutoa shida ya area yao lakini hajapewa nafasi na msimamizi wa area hiyo. Kwa hivyo Rais akisha chaguliwa, raia apewe nafasi ya kusema shida zake.

Mahakama: Kungestahili kuwe na wazee wa mahakama kwa sababu wazee wa mahakama wanaweza kiutetea mtu mchanga. Kwa sababu siku hizi mahakama wanategemea pesa. Inaweza kuwa wazee wa mahakama watamtetea mtu mnyonge.

Shule: Shule hasa Sekondari, katika Sekondari kamati za board zivunjwe, P.T.A. ipewe isimamie shule zao. Wazazi wasimamie shule zao. Wajue pesa ya shule inaenda aje, maendeleo ya shule inaenda aje. Itolewe kamati za boards kwa sababu boards, unakuta mfanyikazi yuko katika idara fulani, ambaye anakuja kuchukua hizo pesa, hana mtoto katika shule hiyo. Kwa hivyo hana uchungu na pesa ya shule hiyo. Mwalimu Mkuu akipatikana na kosa siku hizi hachukuliwi hatua kisheria anapigwa transfer shule zingine. Sasa ameumiza shule hii, bado ataenda kuumiza shule ile. Kwa hivyo achukuliwe hatua ya kisheria na sio transfer.

Vijijini: Vijiji yafaa tuwe na wazee wa vijiji. Wazee wa vijiji watakuwa na nafasi ya kujua shida za wananchi wao. Kwa sababu wenye shida, watakuwa na shida ya kuuza ardhi yao. Lakini wale wazee wa vijiji wataahidi kuwa huyu mtu anauza shamba bila sababu maalum ama vile kwa sababu inajulikana tabia yake. Kwa hivyo wale wazee wa vijiji wapewe nguvu ya kusimamia vijiji

ndio wanajua shida za wananchi wao.

Soko huru imeumiza umma. Kwa hivyo hiyo soko huru ifutiliwe mbali. Ma-Chiefs wawe lakini wachaguliwe na watu wa eneo lake. Sio Bunge. Kwa sababu kunaweza kuwa kuna mpinzani, atachagua mwenzake na pengine hajaridhisha umma. Kwa hivyo Ma-Chief wawe lakini wachaguliwe na umma.

Hospitali: Tuna shida ya mahospitali kwa sababu madaktari wetu wakuu wanafanya biashara. Unakuta daktari mkuu wa hospitali, anakuandikia madawa ya kwenda kuchukua kwa clinic fulani. Kumbe ni clinic yake. Kwa hivyo iangaliwe mfanyi biashara na muhudumu wa umma.

**Com. Bishop Njoroge:** Unataka kusema ya kwamba, madaktari wanaofanya kazi kwa mahospitali ya Serikali wasikubaliwe kuwa na clinics zao?

**Ibrahim K. Kailepi:** Wasikubaliwe kuwa na clinics zao. Wanaumiza umma na waalimu wasikubaliwe wawe na biashara zao. Asanteni.

**Com. Bishop Njoroge:** Thank you very much. Joseph Kulare.

**Joseph Kulare:** Kwa majina ni Joseph Kulare kutoka Ilasit Loitoktok. Nikizungumzia hoja ya kwanza ni kwa President. President apunguzwe madaraka yake. Asiwe na madaraka ya juu zaidi kwamba akitaka kuvunja Bunge, anavunja tu bila taarifa yeyote. Ma-Chiefs, MPs, wawe wakichaguliwa na wananchi na wahudumu kwa muda wa miaka mitano ndio wafanyiwe elections. Hata President asikae kwa muda wa miaka kumi. Iwe full term. Mambo ya culture: Culture itupiliwe mbali kabisa especially Wa-Maasai wenzetu wanasoma kutoka form one, form four, wanaenda mambo ya ukarani, na hawa Ma-MPs wanatumia hawa makarani ku-succeed, kupitia kura daraja ya kwenda Bungeni. Pia the formation of the Government:

Tunataka Serikali ya Majimbo ili Serikali iwe na uwezo wa kuangalia watu katika eneo hiyo na wajue idadi ya watu walioko katika eneo hilo. Especially ya kwetu Loitoktok, sijapendelea sehemu zingine ziwe hivyo lakini kama kwetu Loitoktok, tuna watu kutoka Tanzania, Rwanda, Burundi, wamepotelea huko for ages na huyo mtu akifa analeta shida. Hujui huyo mtu ametoka wapi na haujui alikuwa mharifu kutoka nchi fulani ndio akahamia upande huu. Kwa hivyo tuwe na formation ya Majimbo. Ikinge wale wenyeji wa hizo sehemu za hapo karibu.

Land Act: Mashamba mimi nafikiria kwa council isiuzwe bila kupitia kwa familia iwapo tu kuna shida ya dharura ambayo ingefanywa waweze kuuza hiyo shamba. Kwa ajili mashamba unakuta inauzwa maofisini, iki-signiwa tu na yule karani wa land, unakuta familia haijui mtoto wao ameua shamba. Ukienda kwa Chifu, Chifu anakwambia wewe angalia ile sehemu yako uliachiwa, wacha huyu ale mali yake. Kwa hivyo Chiefs nao wasiwe na powers, kuwa na Kangaroo courts katika ofisi zao.

Unaenda pale, yeye ndio anatatua kesi na hiyo kesi ingekaguliwa tu na elders wa eneo hilo.

Tukija upande wa hospitali: Hospitali ziwe za bure, maji iwe ya bure na education. Kwa ajili watu wengi wameshakuwa maskini kabisa kwa ajili mkulima analima shamba, Serikali haitilii maanani huyo mkulima, chakula yake anatoa. Hajui specific price anaenda kuuza bei gani. Akikula leo mahindi ni shilingi mia tatu, mtoto anatakiwa elfu ishirini na tano Sekondari, kwa hivyo elimu iwe ya bure.

Madaktari waongezewe mishahara na wanyimwe kufungua clinics. Ukienda especially our district hospital here Loitokitok, unaenda unaambiwa hakuna dawa, nenda clinic fulani. Na unakuta the same medicine imetoka kwa hiyo hospitali kubwa na ikaenda kwa hiyo. Kwa hivyo madaktari waongezewe mishahara, wasiwe na biashara yeyote ya hospitali ndogo ndogo kando ya hospitali kubwa kubwa.

Group ranches at least isimamiwe na wenyeji na iwe na auditing kwa ajili hizi pesa tunapewa na K.W.S haitoshi. Tunataka iongezwe na iwe na auditing ijulikane hiyo hela kama ingesomesha watoto au ingetumiwa na individual. Unakuta mtu ameenda kununua gari, amenunua (inaudible) zake, unakuta hizo hela hazi-educate wale members wa group ranches, unakuta ina-educate mtu fulani kwa ajili ni Chairman. Especially unakuta wengine walikuwa wanasimamia group ranches, they are not helpful for the area. Unakuta anapewa pesa ya kwenda kusoma kwa masomo ya juu na ingali watoto native, wako nyumbani hawajasoma na hawajapewa hela ya kuwasaidia. Ni hayo tu.

**Com. Bishop Njoroge:** Thank you Mr. Kulare. Francis Wambua? Akifuatwa na Paul Njenga. Paul Njenga yuko wapi? Peter Koptitat yuko? Unamfuata.

**Francis Wambua:** Asante sana. Kwa majina naitwa Francis Wambua na mimi ni mfanyikazi wa sehemu hii ya Loitokitok. Ningependa kutoa maoni yangu juu ya hii Commission. Mwanzo ningependa kuangalia katika uchaguzi wa MPs na Councillors. Nikianza na uchaguzi wa Rais, Rais angechaguliwa bila kuwa MP mahali popote. Achaguliwe asimame tu kama mtu kwa kiti cha Rais peke yake. Ili asikuwe mtu wa kupendelea sehemu yake aache sehemu ya nchi yake. MPs nao wachaguliwe watu ambao wamesoma hasa kwanzia kidato cha Form four. Wawe na elimu ya kutosha, sio watu wa kwenda kulala kwa Bunge, kuchukua mishahara mikubwa bure. Tukiangalia tena wangetakiwa wakae kwa miaka mitano ili uchaguzi ufanywe tena.

Ya pili ningependa kuongea juu ya Land issues: Ardhi ya Kenya ingetakiwa kuwa ni ardhi ya Serikali na mwananchi kama angekuwa na kubwa, aruhusiwe kuwa tu na less than fifty acres. Akiwa na zaidi ya hiyo anyang'anywe, ipewe wale ambao wanahitaji ambao hawana land na waendeleze. Kama mtu amepewa na hawezi kuendeleza, ichukuliwe ipewe mwingine anaweza kuiendeleza.

Kabla hujatoka hapo, tumeambiwa hapa kuna watu kama Wa-Maasai ambao ni wafugaji na wanahitaji ardhi kubwa katika

eneo ili kuweza kulisha ng'ombe. Sasa ukisema ceiling iwe acre hamsini, unasema ukitofautisha upande wa ukulima na nini?

Asante sana. Ninatofautisha kwa sababu nilikuwa na sehemu ningekuwa kuongea juu ya pastoralists ambao ni wa makabila ya kuhamahama. Makabila ya kuhamahama ambao wako na land kubwa, ningetofautisha kusema ile land ambayo ni arable, land ambayo inaweza kulimwa, ndio ninasema mtu asikuwe na zaidi ya ekari hamsini. Akiwa na zaidi, anyang'anywe wapewe wale wengine waweze kulima. Lakini makabila haya ya kuhamahama, wangetakiwa kusaidiwa sana katika ardhi yao.

Wajengewe maviranga, hizi earth dams, mabarabara yatengenezwe wasaidiwe katika mahali pa kuuza mifugo yao. Kwa sababu hawezi wakapata mapato mahali pengine bali na mifugo ambayo wanaifuga katika sehemu hizo zao kame. Zisiachwe kame hivyo eti kwa sababu ni kame ama ni kwa sababu ni makabila ya kuhamahama ambao hawana elimu ya juu. Wanatakiwa kusaidiwa zaidi ili mapato yao yatoshane na ya wale ambao ni wa kulima. Wasiachwe nyuma. Wainuliwe, watoshane na wale wengine ambao wana biashara zingine.

Tukiangalia katika....

**Com. Bishop Njoroge:** Wale wazee wanaofanya kelele pale nyuma, tafadhali msizungumze. Mkitaka kuzungumza mtoke pale nje mzungumze, mkimaliza mnarudi. Kwa sababu maneno yenu itaingia hapa na watu Nairobi watasema, watu wa Loitokitok ni kelele tu, hakuna maneno walitoa. Sawa? Na nyinyi ni waheshimiwa.

**Francis Wambua:** Asante. Ningependekeza kila Ministry iwe na Minister mmoja na msaidizi wake mmoja. Sio kuwa na Minister chungu nzima ambao wanapokea mishahara mikubwa na wale wahitaji ambao ni maskini wako huku, hawawezi wakapata kitu kwa sababu kama rasilimali za Kenya zikienda kwa mtu mmoja ama watatu, hasiwezi kusaidia watu wengine. Kwa hivyo tuwe na Minister mmoja na Assistant mmoja. Uchaguzi usimamiwe tu na ile Commission ambayo imeteuliwa kuwa ndio inasimamia uchaguzi. Ndio itakuwa iki-set date ya uchaguzi na sio Rais wala sio Mbunge kwa sababu hii Commission iko na mamlaka ya kufanya kila kitu ya uchaguzi. Ipewe nafasi ya kujisimamia, kuitisha uchaguzi na kila kitu ambacho kinahusu uchaguzi. Tukija katika madiwani:

Madiwani wengi hata hawajui kazi yao katika sehemu zao na ni wengi katika nchi yetu ya Kenya. Unakuta katika kila location, kunao wanaitwa ward hii ward hii na hawana kazi maalum ambayo inawahitaji. Wanakula pesa za county council bure. Tungekuwa na diwani mmoja tu katika kila division. Vile tulivyo na D.O mmoja. Kwa sababu diwani mmoja kazi yake itakuwa tu, hiyo inatosha katika kijiji mzima. Kwa sababu kuna makarani wa county council katika hiyo division watafanya kazi zile zingine. Diwani tu atafanya hiyo kazi.

Ya mwisho ni natural resources: Ukiangalia sanasana, watu walio katika mamlaka ndio wanaharibu natural resources kwanzia forests. Utakuta Serikali inaachilia watu wakubwa wanaenda kukata mbao katika sehemu zile zimekuwa restricted sizikatwe



mbao kabla ya miti kuwa imetoshea. Ningeomba kuwe na sheria kali ambayo mtu ataadhibiwa, hata awe ni Rais, awe ni nani, aadhibiwe kama anapeana ruhusu ama amepatikana akipasua mbao katika forest. Sehemu za chemchem ya maji ama mito, kando kando ya maji, ningependekeza kuwekwe sheria, mtu ambaye shamba yake imekaribia kwa maji, at least hatua fulani ziwe ni za miti, sio za kulimwa, ikabe hiyo maji.

Kwa mfano katika hii sehemu yetu ya Nodrues, watu wale ambao wanaishi hiyo sehemu, ingetengwo hiyo ardhi iwe ni water catchment na ipandwe miti na wale wako hapo wahamishwe wapewe shamba mahali pengine ambao ni pazuri kama hapo. Lakini wale watafutiwe mahali kwa sababu wataharibu maji, kwa sababu mwanzo wata-pollute hiyo maji na tena watafanya ikuje kukauka haraka. Kwa hivyo national resources ni lazima zitunzwe kwa njia ya hali ya juu. Pawe na sheria inasimamia hivyo. Asanteni.

**Com. Bishop Njoroge:** Elijah Ole Koptitat, akifuatwa na Simon Gachuru. Simon Gachuru yuko?

**Elijah Ole Koptitat:** Mimi ninaitwa Elijah Koptitat, sio Peter. Yangu ya kwanza ni juu ya Rais. Rais awe ni mtu ambaye anachaguliwa na watu wote. Waziri Mkuu pia nafasi yake ipatikane. Nafasi ya Waziri Mkuu pia ni nafasi ambayo ingefaa ipatikane. Mbunge achaguliwe mtu ambaye amemaliza form 4, isiwe chini ya form 4, form 4 na juu. Pia nominated MPs kuwe ni mama au mlemavu. Asiwe ni mtu ambaye ni mwanamume anaweza kwenda kujitafutia kura. Lakini maana mama hawezei kutembea sana, labda anaolewa. Au mlemavu hawezi kutembea kwa hivyo ningesema hiyo nafasi ya nominated MP, iwe ni ya akina mama na walemavu.

Councillor awe pia ni mtu wa form four and above. Asiwe tena mtu wa chini wa Primary school. Provincial Administration idumu kama kawaida. Iendele tu kama kawaida lakini ningeomba kwa nafasi ya Ma-Chiefs, Chief awe ni mtu wa kutoka pia naye O'level na kuendelea juu. Asiwe chini ya O'level. Na pia awe anachaguliwa na wale watu wa hiyo location anayotaka kusimamia. Maana hii kazi ya kwenda interviews huko kwa wilaya, saa ingine inachaguliwa mtu ambaye hafai kabisa. Kwa hivyo ingefaa kabisa awe anachuguliwa na wale watu wake wanaotaka kumsimamia. Mambo ya national parks iwe chini ya Local Authority kama game reserves kwa hivyo isiwe tena chini ya Central Government.

Serikali, mimi kwa maoni yangu ningependa Serikali ya Majimbo kabisa. Serikali ya Majimbo ianzishwe hasa kutoka uchuguzi huu ambao tunaenda sasa.

Land Control Boards: Mashamba yauzwe na familia nzima na sio mzee tu au mama kama hana bwana. Awe ni mama tu mwenyewe anaenda kuuza shamba kwa sababu ana familia mwenyewe. Iwe inauzwa na familia nzima, wakubaliane na wote waende kwa Land Control Board waseme ya kwamba, tumekubalia kwa ajili ya hili tatizo na hili basi lipewe kwanza.

**Com. Bishop Njoroge:** Wacha nikuulize kabla hujafika hapo. Huko Kimana, tuliambiwa kwamba ili kuzuia kuuzwa kwa



mashamba kwa njia hiyo, mama na mzee wawekwe katika Title Deed. Kwa sababu hiyo itazuia mzee kuuza kama mama hajui. Hata mzee mwingine alisema mama, mzee na watoto waingizwe katika Title Deed. Ungefikiria namna gani?

**Elijah Ole Koptitat:** Ardhi: Kuna ardhi ambayo inataliwa na mtu anaitwa Commissioner of Lands. Mimi kwa maoni yangu ningesema ya kwamba, iwe inaangaliwa iko chini ya wenyeji wa hapo hapo na sio Commissioner of Lands maana huyo anauza bila wenyewe kujua ardhi imeenda wapi.

Elimu: Elimu iwe ni ya lazima kwa watoto wote, wavulana kwa wasichana na iwe ni ya lazima. Watoto wakifika umri wa kwenda shuleni, mtoto aende kwa lazima shuleni na elimu iwe ni ya bure. Pia mzazi au mtu yeyote akitoa mtoto wa kike shuleni kwa njia ya kwenda kuoza au mtoto wa kike akiwekwa mimba au kutoa tu mtoto wa kike kwa njia yeyote, huyu mtu ashitakiwe mara moja. Pia nafasi, intake ya Teachers Training Colleges, watoto wa sehemu kame, wafikiriwe kwa upande wa marks. Maana labda hawatakuwa sawasawa na watoto wa miji. Kwa hivyo mimi ningepomba watoto wa sehemu kame wafikiriwe wakati wa kupelekwa katika Teachers Training College.

Uongozi katika sehemu mbalimbali: Uongozi uwe mikononi mwa wenyeji wa eneo fulani. Kwa mfano Chifu, Councillor na Mbunge, mtu ambaye ni mgeni aliyekuja kutoka mbali, aje kutafuta U-Chifu hapa katika sehemu ambayo yeye ni mgeni kwanza. Au Councillor aje kutafuta kazi ya Council hapa, wangepatiwa nafasi wenyeji, Chiefs, Councillor na hata Mbunge lakini sio mgeni. Kazi pia ya Serikali.

**Com. Bishop Njoroge:** Sheria ambayo inatutawala inasema Mkenya ambaye yuko mahali fulani, huwezi kumnyima haki kuwa katika cheo fulani. Sasa unataka tubadilishe hiyo sheria sasa tuseme kila mahali, mtu ambaye hajazaliwa hapo, hawezi kupata cheo fulani katika mahali pale?

**Elijah Ole Koptitat:** Ndio sababu Bwana Commissioner tuko hapa tunabadilisha. Tunataka tubadilishe. Kazi ya Serikali ifikiriwe wenyeji wa eneo hilo kwanza. Kwa mfano kazi ikipeanwa interviews, watu ambao ni wa nje ndio hupatiwa zaidi kwa ajili inasemekana ya kwamba ndio wana market zaidi. Kwa hivyowatu wa area hiyo hiyo hata kwa kazi ya Serikali, kwa interviews first priority iende kwa wenyeji.

Ya mwisho, ni watu kujipatia majina ya mahali ambapo sio kwao kwa ajili ya kutafuta kazi au kupita mitihani. Kuna watu wengi ambao katika nchi hii yetu ya Kenya wana majina ambayo si ya kwao. Lakini kwa ajili ya mitihani, ili waende Secondary schools au University au kazi, wanasema mimi ni Ole. Na kumbe sio Ole, yeye ni wa mahali pengine. Lakini kwa ajili ya kupata kazi, anajipatia jina la bandia. Kwa hivyo imi yangu ningesema ya kwamba, mtu achukue jina la kwao na kama hiyo ni riziki ya kazi kutoka kwa Mungu, atapata tu hiyo kazi. Kwa hivyo, mimi hayo ndio yangu.

**Com. Bishop Njoroge:** Asante Bwana Koptitat kwa maoni hayo. Njoo hapa ujiandikishe katika register. Tukimaliza na huyu

nitawaita waalimu. Kuna waalimu na wanafunzi tungepatia nafasi ili waweze kurudi mashule.

**Simon Gachuru:** Kwa majina naitwa Simon Gachuru. Kuhusu maoni ningependa kwanza kuongea kuhusu President. President powers zake ziwe retained lakini baadhi ya powers fulani ambazo nitazitaja ziwe removed. Kama vile appointing heads or sensitive institutions kama vile colleges, Judges, Chief Justice na Chief of the General Staff. Nikigusia, hivi majuzi kulitokea ubishi Bungeni kwamba head of Kenya Medical Training College ambaye ametoka kwa jamii ambayo President ametoka. Wakati wa intake ya kuchukua.....

**Com. Bishop Njoroge:** Wajua nimesema hapa kwamba tuzungumze mambo ya kubadilisha. Kama umesema public appointments, what you are saying is public appointments be vetted so that the right person gets the right job. You have already made the point. So don't tell us particular cases because we are not supposed to do that. Unasikia?

**Simon Gachuru:** Ndio. Kwa hivyo mimi ningependelea kuwe na independent committee ambayo President akipendekeza mtu fulani atakuwa ana-head labda hiyo college. I-scrutinize huyu mtu na kama ikiona ni vizuri huyu mtu ana elimu ya kutosha, sio mtu anaweza kuwa na ufisadi ama anaweza kuwa na shida za kitabia za maumbile. Hiyo committee iwe inapendekeza na inapitisha.

Lingine ni kuhusu relationship ya polisi na raia. Serikali ifanye relationship ya polisi na raia iwe nzuri kwa sababu watu wengi hata wakitaka kutoka tip off wanaogopa. Hizi sheria tunaongozwa nazo ni za kikoloni ambazo wakoloni waliziweka kwa Katiba ili waweze ku-safeguard their interests. Kwa hivyo mimi nilikuwa naonelea raia afanye urafiki na polisi ili akitaka kutoa tip off anatoa bila shaka. Kwa sababu kuna mtu anaweza kusema kuna jambo fulani limetokea, akipelekwa aseme ni fulani amefanya hivi. Huyu mtu akifika polisi baada ya kushikwa, polisi akitoa kitu, polisi anasema ni fulani aliniambia. Kwa hivyo huyu mtu anakuwa maisha yake yako hatarini. Kwa hivyo Serikali itengeneze uhusiano bora kwa raia na polisi.

**Com. Bishop Njoroge:** Hivi nikusema ungetaka training ya polisi ifuate njia ya kwamba itaweza kuleta uhusiano mzuri?

**Simon Gachuru:** Mzuri, mimi namaanisha hivyo. Lingine ni kwa upande wa ukabila, ningependelea.....sijui kama nitarudi kwa President kidogo. Ningependelea labda kwa sababu ya ku-appoint mtu labda wa kutoka jamii yake, hiyo independent body ile nilisema, iwe mtu kama anapewa cheo, iwe hiyo cheo inakuwa distributed in various communities. Si eti kwa sababu President ame-appoint huyu mtu. Anaenda anachota watu kama ni watu wanaajiliwa jeshi, madaktari, wapi na wapi. Huyu mtu anaenda anachota watu na malori kwao na hawajasoma, wengine hawana elimu. Wanawekwa pale mpaka wanaharibu ile taasisi ama hiyo kazi inaharibika kabisa. Kwa hivyo kuwe mambo kama hayo si mzuri.

Upande mwingine ni upande wa land: Jina squatter sioni kama ni vizuri kuwa na hilo jina na hali kadhalika wale walipata mashamba makubwa, ni mtu anaenda pahali anatoka na hapo ndio anaonesha (inaudible). Kwa hivyo hawakununua. Kwa hivyo

Serikali ifikirie wale hawana kwa sababu kuna watu wanarundikana kwa railway line, hii reserve. Hiyo railway line ambayo ni reserve iko na railway, watu wanarundikana huko hawana mashamba na sio kupenda kwao. Zilinyakuliwa na wale wenye mamlaka zamani.

Lingine mtu kama awe tortured na ichunguzwe ionekane hakuwa na hatua, huyo mtu anakuwa compensated kwa sababu labda ni madai ya uwongo na rushwa ilitendeka labda pale. Kwa hivyo yangu ni hayo tu.

**Com. Bishop Njoroge:** Hebu nikuulize, si ni heri ku-recommend kwamba kusiwe na torture. Mtu akishikwa anapelekwa mahakamani kuliko baadaye. Kwa sababu hiyo ni rahisi. Mtu akishikwa anapelekwa wapi? Mahakamani. Si hivyo ndivyo ilikuwa? Sawa. Nenda pale. Let's have Benjamin S. Masharen, headteacher. Karibu.

**Benjamin S. Masharen:** Asante sana Mwenyekiti, ningependa pia kutoa maoni isipokuwa mambo haya ya Katiba ni magumu sana na yanakuwa na detail yaani mambo yanaenda ndani sana lakini hata hivyo nitajaribu kutumia wakati mchache sana kwa sababu mimi ni Mwalimu wa historia. Nikisema ni ku-lecture itachukua muda mrefu sana.

Jambo la kwanza muhimu zaidi ni kwamba mimi niko proponent au kwa kinaganaga, mimi naunga mkono Serikali ya Majimbo. Lakini sio hii Majimbo ya wanasiasa wa Kenya ya ukabila ya kutaka makabila fulani wafukuzwe katika jimbo hilo. Ile federal government kama ile ya United States of America, Canada na nchi zingine ambazo zimeendelea. Sitafafanua sana kwa sababu itachukua muda lakini ijulikane kwamba maoni yangu ni kwamba naunga mkono Serikali ya Majimbo. Nije hapa nyumbani kwa sababu mimi ni mtoto wa hapa nyumbani, ningependa kusema kwamba kwa sababu Katiba inahusu haki za watoto. Hapa tuna makabila ambayo wanahamama katika nchi yetu, zinaitwa pastoral communities. Kuna pengine Wa-Maasai, Wa-Rendille, Borana, Wa-Somali na kadhalika. Ningependa Serikali au Katiba yetu ambayo tutakuwa tunatengeneza wakati huu, ichukulie maanani makabila haya. Natumai Mwenyekiti wakati ulikuwa unakuja huku kwa gari, ukiangalia huko sehemu zimeachwa kabisa.

Ningependa Katiba ichukulie maanani makabila yanayohamama na wawe classified kama endangered species. Kama vile tumesema ukimwi ni janga, tuseme pia makabila hawa, wawe endangered species na kuwe na Wizara maalum ambayo itahusiana na hali ya kuchunguza haki ya makabila haya. Kuwe na Wizara katika Serikali ya kuangalia masilahi yao. Masilahi kama elimu ya bure. Wawe hao watoto wanapewa chakula ya bure kama incentive. Kitu ya kuwaweka moyo wawe shuleni. Wawe na free medical services au matibabu ya bure. Wakimaliza shule wawe wanapewa priority katika employment.

Wanapewa mstari wa mbele katika kuajiliwa ili wawe kama wale wengine na wawe pia kama incentive kuwapa moyo wale hawajasoma ndio waweze kusoma. Na wawe wanapewa priority katika admission, katika enrolment. Hata saa ingine pengine hawajafanya vizuri katika mitihani yao kwa sababu ya shida, kwa sababu ya ukame, sehemu wanaoishi wawe wanapewa priority. Jambo lingine kidogo kugusia tu kwa sababu muda hautaniruhusu ni kwamba pia wananchi na wanyama. Hawa

makabila wanaishi na wanyama, mnyama akiua, mnyama akimuua binadamu, hali hiyo iwe inachukuliwa kama binadamu ameua binadamu mwingine. Katika Ki-Maasai kwa mfano, binadamu akiua binadamu mwingine, kuna sheria, kuna ng'ombe fulani inatolewa. Iwe kitu kama hicho. Mnyama akiua binadamu kabisa ichukuliwe maanani katika Katiba ambayo tunaitaka, wale ambao tuko in danger.

Jambo lingine ni kwamba twataka Katiba ya kutetea vijana. Twataka Katiba ya kutetea vijana. Jambo la kwanza ni kwamba tunataka Wizara maalum ambayo sijui itaitwaje. Itakuwa inaitwa Wizara ya Jua-kali, Ministry of Jua-Kali and Youth Activities, kama sports. Jua-Kali, kama nchi yetu tunataka. ....tuseme kwa mfano Serikali imesema ya kwamba nchi yetu inatajikana iwe industrialized. Iwe nchi ambayo imejimudu kiviwanda katika mwaka wa mia mbili na ishirini. Kama tunataka hivyo ni heri Serikali yetu ichukulie maanani hata Ki-Katiba kwamba vijana wapewe push katika hii hali ya Jua-Kali. Na pia katika sports, vijana wengi hawana kazi na tunaona kwamba mchezo wa mpira umekuwa ni mchezo wa dunia mzima.

Kwa hivyo tuwapatie nguvu na tuwapatie Wizara hiyo ambayo ndio itakuwa inaangalia masilahi yao. Kwa haraka haraka Bwana Mwenyekiti, ningependa kusema kwamba sheria ya hukumu ya kifo iondolewe. Hiyo ni sheria ya zamani na ni ya kinyama. Saa ingine watu wanahukumiwa kifo, wananyongwa bure na baadaye inajulikana kwamba hawakuwa na hatia wakiwa tayari wameshakufa. Sheria ya viboko. Kama viboko vimeondolewa shuleni, kwa nini wazee wanapigwa viboko? Kama hatuwezi kurekebisha watoto wetu kwa viboko, kwa nini mzee anaenda kupigwa viboko? That is barbaric, primitive kind of law. That should be eradicated and completely arbitrated\* in the history books.

**Com.Bishop Njoroge:** One more minute.

**Benjamin S. Masharen:** Thank you very much, I am on the verge of finishing. Ningependa pia kuwe na sheria katika Katiba yetu Ma-Councillors wawe at least wamefika kidato cha nne kwenda juu na wawe na ujuzi maalum. Ujuzi fulani. Pia Wabunge wetu at least wawe na shahada ya degree na kama katika sehemu hiyo hakuna mtu ana shahada ya degree, Serikali iteue Mbunge kutoka jirani. Wateuliwe Mbunge ndio wakipenda sana wasome. Pia katika Katiba yetu tunataka sheria ya 'one man one job.' Kila mtu awe na kazi moja. Sio eti uko Mkurugenzi pale, uko nini pale, uko nini pale halafu mnaimba ya kwamba hakuna employment. 'One man one job.'

Ya mwisho kabisa kwa sababu nafikiri muda unaendelea, kuwe na sheria ya watu kuweza kununua silaha ya kujikinga. Kwa sababu kuna insecurity. Kama una uwezo wa kununua silaha ya kujikinga, kuwe na sheria ya kuruhusu. Ni hayo machache tu kwa sababu muda hautaniruhusu lakini nafikiri hiyo itachangiza na itasaidia ili kubunu Katiba ambayo ni ya watu wote katika haki ya watu wote. Asante.

**Com. Bishop Njoroge:** Thank you very much Bwana Headmaster. Those are very important views. Can you register there please? Now you came with students? Who is Josphat Kilungu, what about Esther Wangechi? James Ngugi? Tafadhali mje

hapa mbele. Hawa ni wanafunzi wa shule na tutawakubali kupeana maoni ili waweze kurudi kwa shule. James Ngugi aje basi.

**James Ngugi:** Asante sana. My name is James Ngugi, Mwalimu wa shule ya upili ya Ilasit Secondary School na nina maoni machache kuhusiana na kubadilishwa kwa Katiba ya Kenya. Kwanza nitazungumzia sana hasa kuhusu idara ya elimu kwa sababu mimi ni Mwalimu. Ningependekeza katika shule za msingi, kuwepo na shule maalum ambazo zitashughulikia wanafunzi ambao ingawaji sio wazuri sana katika yale masomo ya darasani na ni wazuri katika ile elimu nyingine kama ya ufundi, tailoring na kadhalika. Kuwe na shule maalum ambayo itanzia kushughulikia masilahi ya hawa watoto wao kutoka katika shule za msingi hadi katika vyuo vikuu. Hata kuwe na mitihani ya kitaifa ambayo inahusiana na hiyo.

Hiyo ni ya kwanza. Pili ningezungumzia kuhusu lugha ya Kiswahili na ningependekeza ya kwamba lugha ya Kiswahili iwe inafundishwa ama iwe ni somo la ufundishwaji kutoka katika shule ya msingi hadi vyuo vikuu. Hata vyuo viweke ile ndio ili kuleta ushikamano na ili kuleta hali fulani ya umoja katika nchi hii ya Kenya. Kwa hivyo kufungamana na hayo, ningependekeza ya kwamba kuwe na chama fulani ama kuwe na idara fulani katika wizara ambayo itahusiana na kuleta mbinu fulani ama mitakati fulani ambayo itachangia katika kuhakikisha ya kwamba Kiswahili kinafahamika na kila Mkenya.

Ya tatu ningependekeza ya kwamba hizi shule za kitaifa, zilikuwa chache sana na hizi shule kwa maoni yangu zilichangia sana katika kuleta ya ushikamano Kenya nzima na nikechangia ya kwamba hizi shule ziongezwe. Kwa sasa tuna shule kumi na nane tu za kitaifa hapa Kenya na tukiangalia hata katika wilaya hii, hakuna shule hata moja kama hiyo ya kitaifa. Na ningependekeza shule hizi ziongezwe kwa kupitia Wizara ya elimu, ihakikishe ya kwamba zitakuwa nyingi zaidi. Angalao kila wilaya kuwe na shule moja ya kitaifa. Halafu nikizungumzia kidogo kuhusu vyuo vikuu, ningependekeza ya kwamba wale Vice-Chancellors ama wale wakuu wa vyuo hivyo, ningependa ya kwamba, isiwe Rais wa nchi ndiye ambaye ndio kiongozi pale. Bali iwe ni kiongozi msomi wa pale chuo kikuu. Kwa sababu inakuwa ni vigumu sana kuingilia au kuchanganya siasa na uongozi. Kwa hivyo ningependekeza ya kwamba hawa wawe ni wasomi ambao wanachaguliwa na wale wasomi katika chuo kile.

Halafu pia ningependa pia kuzungumzia kuhusu swala la waalimu na ningependekeza ya kwamba mishahara ya waalimu pamoja na marupurupu yao na hali zozote zile za kikazi, zishughulikiwe na Katiba ambayo itakuja sasa. Iwe ya kwamba, maongezi ama mapatano yeyote kati ya Serikali na vile vyama vya waalimu, iwe ni kama sheria na isiwe inaweza kubadilishwa kwa hali yeyote ile.

Halafu nikimalizia ningependa kuzungumzia pia kuhusu somo la Katiba. Ningependekeza kwamba pawe na somo la Katiba kutoka katika shule ya msingi. Ndio ili watu waweze kujua nchi yao. Kuna mifano mingi sana ya watu ambao hawajui nchi yao, hawajui namna nchi inavyoongozwa. Hawajui mambo ya haki yao na ningependekeza ya kwamba kuwe na somo la Katiba ama somo la Serikali - jina lenyewe, wale ambao wanahusika wanaweza kutoa jina nzuri. Iwe inanzia katika shule ya msingi hadi kufikia katika vyuo vikuu. Asante sana.

**Com. Bishop Njoroge:** Jiandikishe pale. Josephat Kilingu? Ningetaka kuwaambia sasa tuzungumze kwa haraka. Tuna listi ya watu mia moja thelathini na sita na tumefikia tu namba hamsini na nne. Kwa hivyo mnaona ni watu wengi. Msipofanya haraka, kuna wengine hawatazungumza.

**Josephat Kilungu:** Nashukuru sana kwa kupata nafasi hii. Kwa majina yangu ni Josephat Kilungu kutoka shule ya upili ya Ilasit. Niko hapa kutoa maoni yangu kuhusu.

**Com. Bishop Njoroge:** Which form are you in?

**Josephat Kilungu:** Form four.

**Com. Bishop Njoroge:** How old are you?

**Josephat Kilungu:** I am twenty-two years. Nimekuja hapa kutoa maoni yangu kuhusu Katiba ya Kenya. Kwanza kabisa ningependa kuzungumza kuhusu masomo ya shuleni. Kwa kweli kabisa kama sisi wanafunzi tunaumia sana kwani masomo shuleni yamekuwa mengi sana kiasi kwamba yanatuchosha. Kwa hivyo kama ingewezekana ni vyema kama masomo yangepunguzwa. Masomo yapunguzwe yawe angalao hata kama ni tano, halafu wanafunzi ndio waweze kupata nafasi ya kusoma masomo hayo. Pia katika shule, mashule mengi humo nchini, kuna wazazi ambao ni maskini ambao hawawezi kuwafundisha wanafunzi au hawana fedha za kuwafundisha wanafunzi wale. Kwa hivyo ni vyema kama Serikali ingetoe msaada wa fedha na pia vyakula katika mashule yetu. Ndiposa, wale wazazi ambao hawawezi kuwahitimu wanafunzi wao kifedha ama kivyakula, wafaidike katika masomo yetu pia.

Pia, kuna mashule ambazo zimechanganyikana. Kuna shule zetu Kenya, zile shule zinafanya vizuri unakuta ni shule ambazo ni za wavulana peke yao ama wasichana peke yao. Kwa hivyo ningependa Serikali yetu iweke shule zote ziwe, kama ni za wasichana ziwe - za wasichana peke yake. Kama ni za wanaume, basi ziwe za wanaume peke yake. Hizi shule za mchanganyiko, zisiwe kabisa katika nchi yetu. Kwa sababu ukiangalia, shule zinafanya vizuri ni hizo.

**Com. Bishop Njoroge:** Don't explain. Go straight to the point.

**Josephat Kilungu:** Pia ningependa mashule yapewe magari kwa sababu shule nyingi ziko na shida za usafiri. Kwa hivyo ni vyema Serikali kama ingepata magari ya kusafiria huko shuleni. Pia tungependa Serikali kama ingepeana mafunzo kuhusu Katiba. Mambo kama haya ya Katiba kuna mashule mengi sana hayajui mambo ya Katiba. Kwa hivyo ni vyema kama tungepata mafunzo ya Katiba huko shuleni. Pia mafunzo kuhusu afya ni vyema. Magonjwa kama haya hatari hatari, ni vyema kama Serikali ingetupatia mafunzo kuhusu haya magonjwa. Tungefurahia sana. Pia kuna haya masomo ya computer. Ingekuwa

ni vizuri sana kama computer lessons zingekuwa compulsory kwa kila mwanafunzi. Kwa sababu kuna mashule mengi hawana computer. Kwa hivyo ni vizuri kama ingekuwa compulsory kwa kila mwanafunzi.

Pia usalama shuleni. Mashule mengi hayana usalama. Ni vyema kama Serikali ingepeana usalama huko shuleni ili mambo kama kuchomwa kwa wanafunzi, kesi kama hizo ziishe. Pawe na usalama. Masomo kama ya hesabu ama haya ya science, masomo haya yamekuwa magumu sana na hapo mbeleni ukiangalia ni vyema, watu walikuwa wanafanya vizuri haya masomo. Kwa hivyo inamaanisha kuna jambo fulani ambalo limefanya au vitu vimeongezwa, haya masomo yakawa magumu mno. Kwa hivyo ni vyema kama ingerahisishwa ili angalao wanafunzi wawe wakipita maana mbeleni walikuwa wanapita lakini sasa hawapita. Kumaanisha ya kwamba kuna vitu ambavo viliongezwa huko ambazo zinasababisha wanafunzi waanguke.

**Com. Bishop Njoroge:** Unasema standard iletwe chini ili wanafunzi wapite?

**Josephat Kilungu:** No.

**Com. Bishop Njoroge:** Sema yako ya mwisho.

**Josephat Kilungu:** Langu la mwisho, Muungano wa Jumuiya ya Afrika Mashiriki. Ingekuwa ni vizuri sana, wakati viongozi wanakutana kwenda kutoa maoni yao katika Muuungano wa East Africa, ni vyema pia kama wanafunzi wangepewa nafasi wanashiriki katika hiyo mikutano ndio tujue ni nini inaendelea. Kwa hayo machache, nashukuru sana.

**Com. Bishop Njoroge:** Thank you very much. Very clear thinking, come here and register. I wish you well in your studies. Tupate Esther Wangechi. Karibu.

**Esther Wangechi:** Nashukuru sana kwa nafasi hii ambayo ninakuja kutoa maoni yangu kuhusu Katiba. Jina langu ni Esther Wangechi kutoka shule ya upili ya Ilasit. Kwa maoni yangu, ningependa katika kila shule kuwe na hii ofisi ya guiding and counseling. Ukiangalia wanafunzi wengi, wengine wanaacha shule kwa kukosa mawaidha.

Jambo la pili shule ziongezwe. Shule na pia waalimu waongeze ili elimu katika mashule iwe bora. Jambo lingine ni, ukiangalia si wazazi wote wana uwezo wa kuwasomesha vyema watoto wao. Kwa hivyo ningependelea Serikali ipeane kama ni bursaries za shule na pia vitabu hizi za textbooks ili wanafunzi waweze kufaulu vizuri.

Jambo lingine ni elimu ya wasichana. Wanafunzi wasichana wapewe nafasi ya kusoma katika viwango vyote vya elimu. Ukiangalia wanafunzi wengi hawamalizi shule maana wanaozwa. Jambo lingine ni usawa wa vifaa katika mashule. Ningependa mashule yote yawe na usawa wa vifaa. Si kwamba mashule mengine ni bora kuliko mengine. Kwa mfano katika maabara, vifaa viwe sawa katika shule zote.



Jambo lingine ni kazi: Wanafunzi wengi wanapomaliza shule wanakosa kazi wanakuwa ni kuzurura tu huko mitaani. Kwa hivyo ningependelea kwamba, kuwe na kazi ambayo mwanafunzi akimaliza shule anapata, elimu isiwe haina maana.

Jambo lingine ningependelea Serikali ipatie mashule televisioni na maredio. Hii ni kwa sababu kupitia hivi vyombo, inafanya elimu iwe bora zaidi kwa sababu wanafunzi watapata maarifa zaidi kupitia vyombo hivi.

Jambo lingine, wanafunzi wapewe wakati wa kushiriki katika michezo. Sio kila wakati wako darasani tu wanasoma lakini washiriki hata katika michezo. Asante.

**Com. Bishop Njoroge:** Asante sana. Tutarudi kwa list, nilisema hivi; watu wataitwa kulingana na vile walivyokuja. Kwa kawaida yetu ni kwamba, isipokuwa wanafunzi na waalimi, hatupendi kupita mtu. Yule aliyependa kuzungumza, angekuja mapema zaidi. Ukiwa hujaitwa ujue ni mahali ulikujia na utangoja mpaka jina lako lifikiwe. Tulipoanza niliwaambia nitakubali mjamzito, nitakubali waalimu na wanafunzi warudi shule lakini hao wengine watafuata ile orodha ya majina, kila mtu nafikiri angependa kwenda. What is your problem? You are a teacher? Which school? You come here, you qualify.

**Stephen Gacheru:** I am Stephen Gacheru Thaita and I think you will have to bear with me because I will have to make my submission in English. In respect of our Government system, I wish to propose the retention of our unitary system but the Local Authorities should be strengthened.

In respect of the Executive, I wish to propose the following changes in the Office of the President. One, he shall have to swear an oath of allegiance subscribing to the oath that since this office is a Constitutional creation, he shall be subject to any subordinate to the Constitution. Secondly, I wish to propose that the Vice-President should be voted for directly by the people and upon the death, resignation or dismissal of the President, he should assume all the powers and prerogatives of that office. In such an event, the Vice President shall be deemed to have completed his first five-year term. I also wish to propose the inclusion of an impeachment Act in our Constitution, clearly stipulating grounds upon which the President can be removed through a vote of no confidence. I also wish to propose the creation of the Office of the Prime Minister who shall be the Head of the Government and who shall be responsible for making all senior appointments subject to parliamentary scrutiny and ratification or rather approval.

I also wish to suggest that the Police Act should be changed so that the Commissioner of Police shall be appointed by the Prime Minister subject to parliamentary approval and that he shall be answerable to Parliament for all acts of commission or omission committed by his staff.

I also wish to propose the creation of a new office, the office of the ombudsman. This office shall be tenured, the office shall be



tenured and shall be responsible for addressing and remedying all grievances arising from civil service excesses.

**Com. Lethome:** Can I ask you? The office of Ombudsman, do you want it to start from the locational level?

**Stephen Gacheru:** No, at the national level.

**Com. Lethome:** What happens to communities like here when they have a problem with police, where are they going to report? If you want to help people, then you start where they are and then it goes up. Or you want it to be there? You want it to be at the national level?

**Stephen Gacheru:** Yes. It should be a national office that is tenured but I should also propose or suggest that there should be mechanism at the grass root level where somebody can lounge a complain. On the side of the office of the Comptroller and Auditor General, I suggest that he should be empowered to prosecute any person who misappropriates our social right to property. Although, Parliament is the supreme law making body in this country, I wish to suggest the following limitations. One, Parliament should not enact any registration intended to dis-enfranchise the people of Kenya or to pass any bill retracting on the inalienable rights of the Kenyan people.

The memorandum is a bit long and I think I will have to leave it here. I want to talk briefly about land. Land is a very important resource and I believe every Kenyan is entitled to a piece of land. So, all land or leasehold land that is in the hands of foreigners, should be nationalized and distributed to the landless. Another suggestion is that a (inaudible) should be introduced or imposed on all arable land that is lying idle. Lastly, on national parks, I wish to suggest that their ownership should revert to the County Councils and that the proceeds accruing from the tourism business be shared equally between the Central Government and the Local Authority. Thank you.

**Com. Bishop Njoroge:** You have very important suggestions and I can assure you we are going to get into that memorandum. Thank you very much. Very important views. Asante. Tupate Simon Gacheru. Alice Thande. Dorcas Makuleiyo. Samuel Kahiu. Njoo hapa. Mama unataka kuzungumza? Kuna mama mwingine hapo anataka kuzungumza?

**Dorcas Makuleiyo:** *Kaji ta nanu enkarna ai kaji Dorcas Makuleiyo.*

**Translator:** Jina ni Dorcas Makuleiyo.

**Dorcas Makuleiyo:** *Nara entasat kake ara si enekisomo meta kore tena kata ati ene nemayiolo enkisuma na kayiolo si atudungo ake ntokitin pookin nati.*

**Translator:** Yeye ni mama na hajasoma lakini anajua mengi, anaweza elezea shida zote.

**Dorcas Makuleiyo:** *Na ore na nanu ati ene wueji na kayieu naitetea ntasati amu ore tenkaraki engirororto nairoroki tene neiteteai ntasati.*

**Translator:** Kulingana na maoni yangu ama nikisimama hapa, niko kwa kutetea akina mama kwa sababu nimesikia mazungumzo.....

**Dorcas Makuleiyo:** *Ore na tena kata nadolita irpayiani ebore ena aji nemeti ntasati.*

**Translator:** Na kwa wakati huu ninaona wazee ni wengi na akina mama hawapo.

**Dorcas Makuleiyo:** *Na tenkaraki ena apa kimila ake naibayu ntasati neta meti ntasati dukuya ekiroro amu etoki na apa ake nena.*

**Translator:** Na hiyo inaonekana ni ile culture tu ya kuchukua akina mama kuwa ni watu wa hali chini na ndio maana hawajahusishwa katika mkutano huu.

**Dorcas Makuleiyo:** *Nayieu na naitetea ore tena kata ore iyiok intasati kita apa ilntuturi nikijing erikore nemelio enjukuro amu ore hata ereutata iyiok kiwaita irpayiani siadi.*

**Translator:** Kulingana na upande wa akina mama, sisi nasi tumekuwa viongozi, tumeingia katika vikundi mbalimbali lakini haionekani kwa sababu mpaka wazee wanaturudisha nyuma.

**Dorcas Makuleiyo:** *Netapate ore ntasati na naida ngakitie.*

**Translator:** Na itakiwa ipitishwe katika Katiba ya Kenya kwamba akina mama ndio boma. Mama ndio boma.

**Dorcas Makuleiyo:** *Ore na tena kata nayieu na najo ore tena kata enasai ekatiba naewuo nimikiyiolo ntasati kiyieu si iyiok nikiyiou ena narik iltunganak pookin meenarik oltungani obo.*

**Translator:** Kulingana na Katiba inatakiwa akina mama watambulike na wawe katika misitari ya mbele kwa sababu Katiba hii inatetea kila mtu.

**Dorcas Makuleiyo:** *Ore na tata entoki nayieu naiteteare entasat, naitetea erishoi oenkisuma.*

**Translator:** Yeye kwa upande wa mama anatetea elimu.

**Dorcas Makuleiyo:** *Amu ore tena kata enkisuma iyiok nena nopeny nkera ore tena kata enkisuma nikiyieu na enkisuma e pesho amu mikidim doi ata entoki nikilakie kira ntasati.*

**Translator:** Angeomba Serikali iwapatie watu elimu ya bure kwa sababu watu wengi hawana uwezo.

**Dorcas Makuleiyo:** *Amu ore tena kata ore enkisuma ore tena kata iyiok ntasati ormaasai kiata ntasati nemeeta irpayiani nikiata ntasati nemeeta enkotolia terikore onkishu, ilchambai neaku na ore tata enkerai peisuma na*

*tenkaraki entasat amu nayiolo apa enkisuma,amu eitu aisoma apa. Kake ore na nanu tena kata kayieu nayiolou maanake enkisuma na keyieu naaret ake serikali tenkaraki ina kisuma amu kidolita ajo kiti duo siadi ntasati ormaasai.*

**Translator:** Kusudi ya kusema kuwe na elimu ya bure, wamama wengi siku hizi hawana mabwana na wana watoto na hawana uwezo. Hakuna mzee wa kuweza kusimamia yule mtoto kusomesha, kwa hivyo angeomba Serikali iweze kutoa elimu ya bure kwa kila mtu ili wale hawana uwezo wapate kunufaika na elimu.

**Dorcas Makuleiyo:** *Nayieu ore tena kata enkisuma niyieu nipikipiki maanani oleng amu ore tena kata eyanalu nguvu neshukuni ake enkerai amu atala embuku. Na tenkaraki mata engolon amu maitore olchamba paamir, nemaitore engiteng paamir.*

**Translator:** Angeomba Serikali pia itoe vitabu katika mashule ili watoto waweze kuwa na faida ya masomo kwa sababu watu wengi hawana uwezo wa kununua hata vitabu. Kwa hivyo Serikali itoe vitabu.

**Dorcas Makuleiyo:** *Ore ta amu malo enda amu meyieuni neiroro naleng amu ata nai nkumok nalimu, nayieu ore tiatua siaitin esirikali neingoruni sininche eneikuni ntasati nayiolo enkisuma onemeyiolo peretoki tiatua ina siai petum sininche entoki naingori nena kera enye.*

**Translator:** Angeomba Serikali ipate kujali akina mama na wapewe ngazi za juu katika Serikali maana hata wao wamesoma na wanaweza kuendesha nchi kama wanaume.

**Dorcas Makuleiyo:** *Nayieu naomon ena serikali pejoki kulo arikok lang likiata peingor iyiok naleng tiatua enkisuma amu kira iltunganak lemeyiolo onyo kake ore tenkaraki baa pookin erikore na keyieuni neingori ngoro iyiok peidim ninye aitaruoshi nine ntasati.*

**Translator:** Angeomba Serikali ama viongozi wale ambao wako katika ngazi za juu, waangaliwe sana ili wawe wakiangalia upande wa akina mama. Kwa maana viongozi wengi wanapochaguliwa kama Wabunge, Madiwani, hawajali akina mama. Kwa hivyo wajaliwe sawasawa.

**Dorcas Makuleiyo:** *Neta nalotu aishiraki ol DO ajoki elio iji nayieu nangamu naleng amu ara oltungani oshal nara oltungani nemeta ontoki naitore pejuk ormaasai e kweli meta entoki nintore.*

**Translator:** Basi hata kwa upande wa Provincial Administration ama upande wa ofisi ya D.O., ofisi ya Chief, ipate kuwa inajali masilahi ya akina mama.

**Dorcas Makuleiyo:** *Enyoito si enkoraki iyiok erikore amu kiyieu siiyiok ntasati ningorakiki iyiok lorikan amu kinyoito apa asuj intae nemeeta esiai nincho iyiok. Kiyieu na tata nikijing erishoto ena kata.*

**Translator:** Kwa wakati huu sisi akina mama sasa tuko sambamba kung'ang'ania viti kwa hivyo wanaume hamna bahati.

**Dorcas Makuleiyo:** *Meta aitabaiki ine amu mayieu naipitisha enkata amu ata nai nkumok nalimu kake...*

**Translator:** Kwa hivyo ni hayo tu. Asanteni.

**Com. Bishop Njoroge:** Mama njoo pale. Unasikia wanaume sasa tuko katika shida. Njoo hapa Mzee.

**Samuel Kahiu:** Jina langu ni Samuel Kahiu. Nikichangia mjadala huu wa Katiba, tunaona Ma-Chifu watu wakichaguliwa kama zamani. Ma-Chifu wawe wakichaguliwa na raia kama zamani wakati wa enzi ya Mzee. Mwananchi wa Kenya ana haki ya kukaa pahali popote anataka kukaa na akimaliza kama miaka ishirini, awe akigombania kiti chochote, akiwa ni Chifu, akiwa ni Mbunge, awe akigombania maanake watoto wale wamezaliwa hapo wamekua na wakuwa watu wakubwa. Kwa upande wa wananchi, mwananchi wa Kenya apewa heshima kama watu wale wengine kama Wahindi, Waarabu, maana ukiangalia kama mtu anaitwa Mwarabu, anaweza kupiga mwananchi wa Kenya na asiulizwe na mtu. Maana yake mwananchi wa Kenya hana nafasi ya kujitetea maana ni pesa inaingia.

Kitu kinaitwa Majimbo, hiyo itupiliwe mbali. Maanake kuna kufunikwa kwa watu (inaudible). Na hii Majimbo ndio huleta utata, ukiangalia kama Uganda, kwingineko kuko na uchacha shauri ya hii Majimbo. Watu wale mia nne, watu wale wana taabu, hawapatiwi pesa ya kuridhisha. Wapatiwe pesa ya kuweza kuenda kuangalia kazi yake maana sasa ameacha kazi.

Madiwani: Madiwani wale wanateuliwa, wawe wakiteuliwa juu ana masomo. Kwa hivyo sina mengi ni hayo tu.

**Com. Lethome:** Asante sana Mzee Samuel. Julius Ntei Korati yuko? Simon Maritei? Lawrence Karanja. Muteli Minduti, Tepai Tapokoi, James M. Wahome. Karibu Wahome. Joseph Kiutho yuko?

**James Wahome:** Kwa majina ni James Mburu Wahome. Yangu ninapendekeza Rais awe anachaguliwa na wananchi wote bila kutoka kwa chama chochote na awe hana mamlaka makubwa kama hiyo ya kuteua wasimamizi wa sehemu hizo za kama Ma-Judges na wale wengine ambao wanasimamia hata kama ni kuchagua hao wasimamizi wa vyo vikiu. Wawe wanachaguliwa kupitia kwa Parliament. Pia ninapendekeza wanaochagua wawe na uwezo wa kupitisha vote of no confidence na Mbunge wao kama hawatendei vyema.

Pia ninapendekeza habari ya mashamba. Kwa kweli tuna watu ambao wana mashamba vikundi vikundi ama hapa na pale na bado ana shamba moja kubwa ambayo haitumiki. Unasikia mtu ana acre elfu ishirini na tano na hali kuna mwananchi ambaye hana hata chochote. Ninafikiria iwe ni haki ya mtu yeyote katika Kenya apate ardhi. Pia ninapendekeza iwe ni haki ya masomo kwa kila mtoto ama yeyote yule ako Kenya. Iwe ni haki. Upande huo wa masomo kutoka kiwango cha chini mpaka cha juu, Serikali iwe inaangalia. Kama ni hao walimu wapate mishahara mikubwa na kwa njia hiyo tutaepusha hawa watu wa chokora na hao watu wengine ambao tunaona hawana elimu. Kufikia hapo, ninaona iwe ni haki ya mtu kuishi popote pale na ikiwa ana rasilimali mahali pale anaishi, awe na haki pia ya kugombania kiti chochote kile cha utawala. Kwa hayo machache asante.

**Com. Lethome:** Unasema kuna watu wako na ardhi kubwa sana na wengine hawana. Ungependekeza mtu mmoja awe na ardhi kiasi gani ya mwisho kabisa?

**James Wahome:** Kwa sehemu zingine zile productive ama kama (inaudible) awe na kama ekari hamsini na kama ni sehemu zile za wafugaji awe na kama eka mia mbili.

**Com. Lethome:** Joseph Njogu? Karibu. Harisson Kang'ethe yuko?

**Joseph Njogu:** My first point is.....my name is Joseph Njogu. Education level for the President should be a graduate and the MP should be a graduate. Councillor should be form four or O'level. The Vice President be elected by the people. The Attorney General to be elected by the Members of Parliament and for five years term. People to be able to vote for their MP, for vote of no confidence through constituency level. To have two Houses of laws in Parliament. We can have Upper House and Lower House so that the amendment of law from the Parliament can come through the Lower House. One Ministry to be having one Minister. Not like this time, we have two Ministers for one Ministry. To scrap Assistant Ministers and instead of them we have three Permanent Secretaries and other Secretaries to create more jobs.

Education to be free upto form four level. President should not contest for Parliamentary seat.

Freedom of Worship: We have so many religions in this country, so we have the role of reducing the number of religious denominations.

Elections: Counting of votes. When the time of elections come, the counting should be done, where the people have done the voting. So that they can tally the number of votes but not the masandukus. There at the polling station. Thank you very much.

**Com. Lethome:** Are you saying that the number of constituencies should be reduced?

**Joseph Njogu:** Be reduced yes.

**Com. Lethome:** Which is the criteria? How do we know which one to de-register?

**Joseph Njogu:** We can know, for example, I can say, I was in Nairobi for the last two weeks. There is a sect we call Thai. Religious sect. If you see even their rituals, you can't imagine you are in a county like Kenya because of what they were doing. So that thing can be (inaudible) or any way of de-registering the religions.

**Com. Lethome:** Pemoa Paritimo

**Pemoa Paritimo:** *Ore ta enai edukuya. Kajo ashe oleng tesiai e Katiba teneihushishae iltunganak. Jina langu ni Pemoi Partimo.*

**Translator:** Jina langu ni Pemoa Paritimo.

**Pemoa Paritimo:** *Ore na nai e dukuya na esiai e sipitali.*

**Translator:** Ya kwanza ni kazi ya hospitali,

**Pemoa Paritimo:** *Neshukuni meta enepesho.*

**Translator:** Serikali irejeshe kuwa ya bure.

**Pemoa Paritimo:** *Ore eniare na esiai esukul.*

**Translator:** Ya pili ni kazi ya shule pia.

**Pemoa Paritimo:** *Peshukuni meta ene pesho.*

**Translator:** Masomo iwe ya bure.

**Pemoa Paritimo:** *Ore ene uni na majimbo.*

**Translator:** Ya tatu ni Majimbo.

**Pemoa Paritimo:** *Nikiunga serikali ena siai e majombo. neasayu ina siai e majimbo.*

**Translator:** Ningeunga mkono kazi ya Majimbo. Majimbo iwekwe.

**Pemoa Paritimo:** *Ore ene uni.*

**Translator:** Ya tatu,

**Pemoa Paritimo:** *Ne esiai oltunganak laramatak lo nkishu oingor ebiotisho onkishu.*

**Translator:** Ni kuhusu madaktari wa ng'ombe.

**Pemoa Paritimo:** *Ore ina siai onkishu na kajo peingori oleng amu kijo mekure oshi eetai peshukuni metiu ana enapa, amu ore tata esiai eramatare onkishu neta eneta nkishu moyiaritin yoyote na mpaka neaku iyie oloopeny oloaingoru negharamia epiki engari niyaki. Neaku kajo eimie na enasiai na enaikash teneshukuni metiu ana apa laramat lo nkishu amu mekure eetai lelo aramat oshi lo nkishu.*

**Translator:** Anazungumzia kuwa madaktari wanaoshughulika na mambo ya ng'ombe, ni kwamba siku hizi hawako. Ni kama hawaonekani. Kwa hivyo kama itawezekana, itafutwe namna, madaktari hao waweze kuwa watu wa kufanya kazi yao vile inavyofaa.

**Pemoa Paritimo:** *Ore na enkae na ina siai eji na ina siai apa kijoito ore ta esiai enkop ang ormaasai na kewaki apa tenkoitoi emesimisi nimikiyiolo ajo kai eikunayieki ana Amboseli, ashu Tsavo nikijo peshukuni ina kop meta ena ang ake ena enopa kata.*

**Translator:** Kuhusu mambo ya ardhi, ardhi ya Wa-Maasai imenyakuliwa kwa njia ambayo hatujajua ni njia gani. Kwa hivyo tungependekeza ardhi hiyo irudishwe ikae kama zamani.

**Pemoa Paritimo:** *Ore na enkae naake naimaki najo nanu naninye ene mwisho na esiai enkingorata oltunganak, peijalieki na tenkagaki nena kishu nikiboitare nara nguesi amu kijoito megira oshi serikali aijalie iltunganak nguesi enyor alang iltunganak nikijo peijalieki vile nikijaliki iyiok oltungani tenear olikae amu kijali si iyiok ormaasai nikijo ore pemeijalieki eetai ina siai omoni tiatua enkop nanyo obori olotu arik enkop enye neaku ina si pemeijalieki ina siai ormaasai tenear nguesi nkishu naboitare amu anata eijalieki ana vile nikijali oleikae tungani tenear olikae.*

**Translator:** Kuhusu mambo ya wanyama wa pori, anasema ya kwamba, Serikali huwa haijali Wa-Maasai. Kwa sababu mara Mu-Maasai anapoumizwa na mnyama, haizingatiwi. Ni kama anachukuliwa ya kwamba ni mnyama ameu mnyama mwininge. Kwa hivyo angeomba Serikali ijali Wa-Maasai kwa sababu uongozi, inaonekana haijali sana upande wa Wa-Maasai. Kwa hivyo iangalie sana Wa-Maasai na wajue. Kwa sababu hata Wa-Maasai wenyewe kulingana na desturi na mila, mtu anapoua mwingine, watu wanaweka maanani na sijui ni kwa nini Mu-Maasai asiwekelewe maanani anapoumizwa na mnyama.

**Pemoa Paritimo:** *Ore na enkiti wueji na naigusia na esiai olaiguenak ochifi nake ore nai duo te duata ai, najo peshukuni amu ajo pearaisisi amu iltunganak na sininche ota duo erishata nati naingunisha iltunganak pookin telulungata kake eitu eshukuni peaku wananchi nagelu amu ninche nayiolo oltungani oidim aijalie iltunganak amu eya oshi nepuoyi agelu te shumata teoltungani obo nakidimi aisho iltunganak opuo lemeijali iltunganak.*

**Translator:** Kuhusu mambo ya Provincial Administration hasa upande wa Ma-Chief, angependekeza Ma-Chifu wawepo na waendeleo lakini sasa kabla ya Chifu kuteuliwa, ingefaa irudishwe kama zamani, wazee wakae na kujua ya kwamba mtu fulani ndio anaweza kuwasaidia wale watu.

**Pemoa Paritimo:** *Ine wueji na aitabaiki.*

**Translator:** Kwa hivyo yake ni hayo.

**Com. Lethome:** Ngoja kidogo. Hii Majimbo unataka iwe katika kiwango gani? Kwa mfano Kajiado district iwe ni jimbo moja au Province ya Rift Valley ama location ya Loitokitok. Unataka iwe kiwango gani?

**Pemoa Paritimo:** Nataka Majimbo ianze ngazi ya juu mpaka chini. Nataka ianze na tuseme Majimbo.

**Pemoa Paritimo:** *Ore majimbo nikiyieu na neishori pookin tunganai majimbo teneti majimbo neaku ore mejimbo*

*nikiyieu na tenkaraki oltungani loiti ene majimbo naatae oltunganak oti Oloitokitok.*

**Com. Lethome:** Kwa hivyo *majimbo* iwe katika kiwango gani?

**Translator:** Anasema ya kwamba Majimbo kama kuna wakaaji wanaoishi katika hii sehemu, wawe chini ya hilo jimbo la hiyo sehemu ama hiyo wilaya. Yaani kulingana na vile anavyoelezea ni kwamba angetaka iwe kwanzia ngazi ya juu mikoani mpaka wilayani. Ndio anasema.

**Com. Lethome:** John Komoi. Afuatwe na Tairiam Malinka.

**John Komoi:** Kwa majina mimi naitwa John Theiya Komoi, mkaaji wa Loitokitok. Kwanza nikianzia na uchaguzi, ningetaka Rais awe anachaguliwa na wananchi wote na pia awe na siku ya kuchagua uchaguzi wa Rais peke yake, ule wa Wabunge na Ma-Councillor, siku ziwe tofauti.

Pia la pili tungetaka katika ofisi ya Rais, watu kama Katibu Mkuu, cheo cha Katibu Mkuu iondolewe kwa kuwa mimi sioni kuwepo na Katibu Mkuu na pia kuna Waziri ndani ya hiyo ofisi.

**Com. Lethome:** Permanent Secretaries?

**John Komoi:** Permanent Secretaries. Na ni wizara moja. Iwe Waziri yuko, Katibu Mkuu yuko na sijui nani mwenye nguvu hapo. Mmoja aondolewe kama huyu Permanent Secretary aondolewe, iwe Waziri peke yake ndio wanahudumu katika hizi ofisi.

Nikija upande wa ukulima maana mimi ni mkulima wa Loitokitok niseme kwa kweli soko huru hii ambayo ililetwa inatumiza sisi kama wakulima na inaturudisha nyuma sana. Kwa hivyo Katiba ambayo tunayoongea ya kileo, tungetaka itazame na iondolewe kabisa. Pia nikija upande wa forests ambayo inazunguka eneo zingine, forests za aina yeyote katika Kenya hii yetu. Ningetaka wale wananchi ambao wanakaa karibu wawe ndio watawala wa ile forests na wawe ndio wanaangalia masilahi ya zile forests kuliko forester ambaye anatolewa kutoka pengine Mt. Kenya ama anatolewa kutoka Pwani, anakuja kumiliki ile forest, anafanya kama mali yake. Wale wananchi wanao zunguka zile forests wanakosa kuelewa ile forest inawaaidia kwa njia gani. Wanakosa matumaini, haina faida yeyote ambayo wanapata. Inakuwa kama ni mali ya yule forester ambaye amewekwa pale.

Upande wa elimu: Ningependa elimu iwe kama zamani. Iwe kwamba elimu ni ya bure kwanzia nursery mpaka form four. Lingine kwa upande wa Amboseli areas ama sehemu ambayo ilinyakuliwa kitambo kabla sisi hatujazaliwa pengine ilikuwa imeshanyakuliwa. Tungetaka irudishiwe wale wananchi ambao ni area zao zilinyakuliwa. Nikisema hivyo nasema tu, sio area ya Ki-Maasai peke yake maana Wa-Taita wako karibu na sisi, pengine wao wamenyakuliwa ardhi yao. Kwa hivyo ningetaka



irudishwe kwenye mamlaka ya wale watu ambao wako karibu na zile sehemu.

Pia kama haitazekana kabisa, iwe asilimia themanini na tano ya mapato ya kutoka kwenye yaani sehemu kama Amboseli na Tsavo, iwe inaandikwa wale wananchi wanaozunguka ile sehemu. Kwa kuwa wale wananchi ndio wanaumia, ng'ombe zao zinaumia na wanyama wa pori na pia hata wao wenyewe ndio wanaliwa na simba. Kwa hivyo kwa njia ile ama nyingine, wale watu ndio wanaadhirika kuliko watu wa mbali ambao wanakuja kutoa pesa pale na hawana faida yeyote, anawachia wale wananchi wanaozunguka hizo sehemu.

Lingine ningetaka hizi Title Deeds za mashamba, ziwe zinakaa kwenye ofisi kama ya D.O. na asiwe mtu kama Registrar ambaye anakaa sehemu ile, baada ya miaka mitano yeye ametajirika hata kuliko hata Waziri aliyeko kwenye Ministry. Kwa ajili mtu yeyote akitaka Title Deed, yeye mpaka tulipe yeye kwa namna ile ama nyingine. Kitu kama hicho ningetaka iwe katika ofisi ya D.O. Kuhusu Ma-Chiefs: Ma-Chiefs kwa maoni yangu ningetaka mimi kwa mawazo yangu ama kwenye hii Katiba tunayotengeneza wa leo, Chifu awe anachaguliwa na raia wa sehemu yake na awe amehudumu miaka saba.

Baada ya miaka saba iwe pengine ataangaliwa kwa kura ya maoni kama bado wananchi wanampenda au hawampendi. Ili asije kukaa na kujisahau kabisa kama ilivyo sasa. Maana Chifu hatujampata hata saa hii sasa. Anakaa hata miaka mia moja, sijui ni uzee utawaondoa hapo na anaweza kufanya chochote anachotaka maana yeye amekuwa ni mtu permanent. La mwisho kabisa ningomba Serikali za wilaya yaani hawa Ma-Councillors. Ma-Councillors wawe ni watu wamesoma kidogo. Ma-Councillor wateule wasiwe wanateuliwa kwa ajili ya chama. Councillor kama anateulwa awe ni mama ama ni mlemavu ambaye hawezi kujitetea kabisa. Asante.

**Com. Lethome:** Ugependekeza elimu yake iwe katika kiwango gani?

**John Komoi:** Awe kwanzia Form Four na kuendelea.

**Com. Lethome:** John Lemantu.

**John Ole Lemantu:** *Ore ta nanu nainei na naji John Lengeteo ole Mantu.*

**Translator:** Anaitwa Lengeteiyo Ole Lemantu.

**John Ole Lemantu:** *Namanya eda kop or lashanjani.*

**Translator:** Kutoka hapa Loitoktok.

**John Ole Lemantu:** *Ore ta nainei tendoropu na ore ene wueji olainguenak na ninye aiteru.*

**Translator:** Yeye anaanza kwa upande wa Ma-Chifu.

**John Ole Lemantu:** *Ore entoki nikiomon serikali na peyie eoki aku ore na olaiguenani na iltunganak leina location ogelu.*

**Translator:** Serikali itoe sheria ya kusema, Chifu ateuliwe na wakaaji wa sehemu yake.

**John Ole Lemantu:** *Nikiomonu ajo meishori iyiok kila location meta olaiguenani lotoni tene neaku iyiok ogela ate.*

**Translator:** Na tungependelea tungependelea tungepewa tupewe kila sehemu ama location. Sisi tukae tukichunguza na kujua Chifu wetu na kujichagulia.

**John Ole Lemantu:** *Neaku kidol ake olaiguenani nikiyieu neishori iyiok na oltungani likigelu oloidipa form four.amu ore na kulo oshi tata nearitae iyiok naleng amu oltungani obo ogelu.*

**Translator:** Na Chifu ambaye tutataka sasa ni mtu ambaye amehitimu masomo. Na Ma-Chifu siku hizi tunashindwa kwa sababu ni mtu mmoja anachagua.

**John Ole Lemantu:** *Neta kijoito serikali ang e Kenya naarita iyiok amu egelakini na iyiok oltungani lemeyiolo onyo.*

**Translator:** Na tunasema ya kwamba Serikali inatumiza kwa sababu wanachagua mtu ambaye haelewi.

**John Ole Lemantu:** *Ama oltungani loitu eroro darasa meti na tata kulo likijoito eisilisilito iyoik.*

**Translator:** Mtu ambaye hajakanyanga hata darasa. Sasa ni mateso anatutesa.

**John Ole Lemantu:** *Nikiomonu ajo peyie eishori iyiok uhuru teine mategelaki ate lelo.*

**Translator:** Kwa hivyo angeomba Serikali itoe uhuru, watu wapewe nafasi ya kujichagulia.

**John Ole Lemantu:** *Ore orkansolai tenebo orbungei nikilimu ajo pookin oltungani omunare nemoki serikali ang aisho iyiok aisho nafasi peitasho mategelu na oltungani ake oidipa form four neitu idialo.*

**Translator:** Kwanzia Diwani na Mbunge, tungeomba Serikali ipate yule mtu ambaye amemaliza form four na kuendelea. Diwani na Mbunge.

**John Ole Lemantu:** *Nelo ta neidipayu aikunaki neija.*

**Translator:** Hilo ndilo jambo la pili.

**John Ole Lemantu:** *Nena enkae, aningito nata ake nai iltunganak oitayu tene ojo esipa eeta pooki ngae uhuru te Kenya pelimu enaba eneyieu.*

**Translator:** Lingine kulingana na mazungumzo ya watu wengine ya kusema ya kwamba kila mtu ako na uhuru wa kutembea popote katika jamhuri ya Kenya ama kuishi.

**John Ole Lemantu:** *Na nisawa.*

**Translator:** Na hiyo ni sawa.

**John Ole Lemantu:** *Kake nena si entoki nikiyieu nikiomonu.*

**Translator:** Lakini katika pendekezo lake, kile angeomba,

**John Ole Lemantu:** *Ore ele tungani olotu neta olaya.*

**Translator:** Huyu ambaye anakuja kutoka mahali pengine, amekuta mwenyeji wa hapo,

**John Ole Lemantu:** *Na lekae osho eingua.*

**Translator:** Na ametoka mahali pengine.

**John Ole Lemantu:** *Etiu ake ana peitau iyiok enkai nkangitie kieta.*

**Translator:** Tunajua ya kwamba, sehemu ni sawa kama vile Mungu alivyopanga sisi tulivyo.

**John Ole Lemantu:** *Neti iltunganak lemeeta enkop enye.*

**Translator:** Hakuna watu wasiokuwa na kwao.

**John Ole Lemantu:** *Hata tena eikira lekenya pooki.*

**Translator:** Hata kama tuko Wakenya wote.

**John Ole Lemantu:** *Neyieu nelotu ilo payian nelotu matotoni tesidai.*

**Translator:** Huyo mtu akija akae vizuri vile tunavyotaka.

**John Ole Lemantu:** *Kake melotu ajing olchamba lai hata tena esapuk.*

**Translator:** Lakini kulingana na sheria, ningeomba idhibitishe sheria ya kusema mtu aingie kwa shamba la mwingine hata ni kubwa.

**John Ole Lemantu:** *Amu ore apa olchamba enye otunguaiye nakakeiputaki.*

**Translator:** Kwa sababu lazima hata yeye amezaliwa akiwa na baba yake na mama yake na alikuwa na shamba na aliacha.

**John Ole Lemantu:** *Na kaipot si nanu tolaini adolita ajo ninye esapuk, kaipot amu agira aisho ana ninye.*

**Translator:** Kwa hivyo naamini vile vile alivyojikuta nikiwa na shamba kubwa, niko ma watoto wangu na nimezaa kama yeye.

**John Ole Lemantu:** *Kake tenikitoni tenebo pekiningu iltunganak metejo ereutae naisho enetur.*

**Translator:** Lakini tunapoishi pamoja na ile sehemu ya kununua ama kulima.

**John Ole Lemantu:** *Na lotu ene wueji naji onguesi.kore ntarikini are ena apa tata nikit.*

**Translator:** Kuhusu K.W.S ama wanyama wa pori. Kutoka juzi,

**John Ole Lemantu:** *Nayakini chaque KWS ongalifuni ntomoni uni olalashelai apa otara engues.*

**Translator:** K.W.S. wameweza kuniletea mimi cheque ya shilingi elfu thelathini ya aliye uawa na wanyama.

**John Ole Lemantu:** *Amu ore ta ana pajoit nejia.oringolio apa naitobiruni KWS ajo pebaya amu torok naleng amu aitara nanu olntome kuna olongi tata*

**Translator:** Nikisema hivyo kuhusiana na wanyama wa pori, mimi nataka kusema idara hiyo ni mbaya kwa hivyo katika Katiba yetu tunasema ni mbaya.

**John Ole Lemantu:** *Ore iloalashelai neta larin tikitam nataara engues.*

**Translator:** Ndugu yangu aliyeuawa na mnyama, aliuawa miaka thelathini iliyopita ama ishirini.

**John Ole Lemantu:** *Nayaki ntarikini are e chaque ongalifuni tomoni uni.*

**Translator:** Juji tarehe mbili ndio nililetewa cheque ya shilingi elfu thelathini.

**John Ole Lemantu:** *Nalimu na ajo kore ina siai kore lelo tunganak ayakitia ina cheque naitamana mpaka tena kata iji.ore eduata nayieuni teine napeyie eaku ore nguesi esipa iyiok lopeny ngues.*

**Translator:** Anasema wanyama wawe chini yetu sisi kama wakaaji wa hapa.

**John Ole Lemantu:** *Ore ina kop najoitoi apa ewa serikali neshuki amu enaang.*

**Translator:** Kwa hivyo hiyo sehemu Serikali imenyakua turudishiwe maana ni yetu.

**John Ole Lemantu:** *Na kijo peshukokini iyiok ina kop.*

**Translator:** Turudishiwe.

**John Ole Lemantu:** *na tene idimayu te serikali amu ekenya tinikiomonu.*

**Translator:** Turudishiwe sehemu hiyo, Serikali itupee.

**John Ole Lemantu:** *Ore ena apa ore te duat ai ena serikali na peyie emoki alak aingoru iltunganak ana enaingorita nguesi.*

**Translator:** Kwa hivyo ningependekeza Serikali iwalipe watu fidia mzuri kama vile wanavyoangalia wanyama.

**John Ole Lemantu:** *Tana olaki imiet elaki engues nelaki si oltungani.*

**Translator:** Kama mnyama analipwa laki tano, hata binadamu alipwe laki tano.

**John Ole Lemantu:** *Tena milioni imiet na nelaki.*

**Translator:** Kama ni milioni tano, ilipwe milioni tano.

**John Ole Lemantu:** *Amu melakini na.*

**Translator:** Kwa sababu hawalipwi.

**John Ole Lemantu:** *Nejo ta nainei.*

**Translator:** Amemaliza.

**Com. Lethome:** Hassan Kilonzo? Philip Mosot yuko? Utamfuata huyu.

**Hassan Kilonzo:** Kwa majina naitwa Hassan Kilonzo na ningetaka kutoa maoni yangu, kwanza ni kuchaguliwa kwa Rais, ningenelea Rais awe na mihula miwili ten years na awe ni mtu ambaye amehitimu, aliye na kiwango cha University. Pia ningelitoa maoni kwa upande wa education, education iwe ya bure. Kwanzia Primary hadi University. Pia, matibabu yawe ni ya bure pamoja na maji. Pia ningelipendekeza katika Section 75 ambayo inapatia Serikali mamlaka ya kuchukua public lands, hiyo iondolewe ili iwe inaweza kusaidia mwananchi ambaye anaishi sehemu hiyo.

Ningependekeza pia Vice President achaguliwe na raia. Katika upande wa Local Government, Ma-Mayor wawe wakichaguliwa na raia. Pia Chiefs wawe wakichaguliwa na raia. Na pia ningependekeza kwa upande wa President's powers zipunguzwe ili powers zake zingine zipelekwe katika Parliament, kwa sababu MPs wamechaguliwa na raia na ambao ndio wangeliveza kushughulikia mambo yale mengi kuhusu raia. Kwa hivyo powers zake zingepunguzwa zipelekwe kwa Parliament.

Pia ningependekeza MPs wasiwe wakijadilia mambo yao wenyewe kama mishahara na other benefits. Kuchaguliwe kamati ama Commission ambayo itaangalia masilahi yao badala ya wao kuzungumzia masilahi yao.

Pia ningependekeza kwa upande wa registration of persons, ID cards, mtu ambaye amefikisha miaka kumi na nane, awe huru kupata kitambulisho wakati wowote na pia mtu aliyeoa, bibi yake awe anaweza kubadilishiwa kitambulisho bila kuambia aende mahakamani. Sheria ibadilishwe ili iwe inaweza kusimamiwa na wazee, elders wa hiyo area ambao wameoa sehemu hiyo au pahali anapoishi. Hii itarahisisha kazi hiyo badala ya kwenda kortini.

Pia ningetoea maoni kuhusu police force na public. Kuwe kunafanyika education kuhusu relationship ya public na police force ili raia wasiwe wakiogopa police force wakati wanapofanya kazi yao, wawe wako marafika.

Pia ningependekeza ya mwisho, kuhusu akina mama na watoto, kuwe na sheria ambayo ina-protect wao through torture ambayo sana imeumiza akina mama na watoto katika nchi yetu. Kwa hivyo sheria hiyo iwekewe mkazo sana, wawe protected na pia katika Bunge wapewe nafasi hata ya nomination na wale wamama, watoto hata wazee wale walemavu. Wapewe nafasi priority ya kuchaguliwa kama nominated MPs na Councillors. Asante.

**Com. Lethome:** Asante sana. Philip Mosot. Afuatwe na Stephen Gacheru.

**Philip Mosot:** Kwa jina naitwa Councillor Philip Osondo Mosot. Pendekezo langu la kwanza ni kuhusu Rais. Rais wa nchi hii awe anachaguliwa na wananchi. Wananchi wawe zaidi ya asilimia hamsini kwa kila kabila na sio mtu ambaye anachaguliwa Mbunge kwanza. Awe ni mtu, akija kwa chama, aje kwa chama lakini awe anachaguliwa katika nchi nzima. Uwezo wa Rais upunguzwe kulingana na kuchagua Makatibu ama nini, iwe naye zake zipunguzwe. Awe hana hayo mamlaka ya kuchagua. Awache watu ambao wanachagua. Kuwe na kamati ya kuchagua hawa watu.

Elimu: Elimu iwe kutoka Primary mpaka Secondary iwe ni elimu ya bure zaidi kwa watu ambao wanahamama. Tunataka sisi tukiwa Wa-Maasai ambao tunahamama, iwe elimu ni ya bure kwa upande wote. Iwe kuna boarding. Serikali ijengee sisi boarding kwa sababu kuna haba katika sehemu zote ya nchi ya Wa-Maasai. Ijengee boarding watoto nao wapate kusoma.

Mipaka: Mipaka izingatiwe. Hatutaki iingiliwe mipaka vile ilikuwa imewekwa, kama ni ya Wa-Maasai, mipaka yetu iwe inaangaliwa na Katiba ambayo tunaunda sasa. Kwa sababu kama hakuna Katiba ambayo inatungaliwa na itanyakuliwa vile nao beberu walipeana hizi sehemu nyingi katika nchi ya Kenya. Kwa sababu (inaudible) hii port ilikuwa ya Wa-Maasai lakini wabeberu wametunyang'anya. Kwa hivyo Katiba ambayo tunaunda sasa iangalie mipaka yetu.

Majimbo: Majimbo iwe iko. Lakini hatutaki majimbo ya kabila, tunataka majimbo ambayo inatungalia kwa sababu sisi Wa-Maasai, mazingira yetu, kila kitu yetu, inakuja kuchukuliwa kama hakuna majimbo. Kwa hivyo sisi tunataka majimbo kwa sababu ya kutungalia. Kwa sababu makabila mengine yameenda kilomita mia moja na sisi bado tuko nyuma. Kwa hivyo jimbo tukiwa na jimbo, tutajisaidia kuangalia masilahi yetu. Serikali ya mitaa ipewe nguvu, yale mazingira yote, maji, barabara, hospitali na masomo ipewe Serikali ya mitaa kama zamani iangalie. Ardhi yetu Wa-Maasai imechukuliwa kama Amboseli National Park irudishwe. Na irudishwe ipewe Local Government. Ipewe Serikali ya Kajiado ya mitaa. Kwa sababu ilichukuliwa bila sisi kujua kwamba imechukuliwa namna gani. Kwa hivyo parks zetu ambazo zimechukuliwa zirudi kwa County Council na wafanye management.

Wabunge: Wabunge nao wawe, sio waende wajipitishie mishahara kama wakati mwingine. Kuwe na kamati ambayo inaweza

kuangalia masilahi yao. Kwa sababu tukiwa sasa sisi Ma-Councillors hatuna mishahara lakini kwa sababu hatuendi Bunge, hatuendi Bunge, kwa hivyo hatuna watu wa kututetea. Lakini wale wanajitetea wenyewe, wanajipatia pesa chungu nzima.

Ma-Chiefs wawe ni watu ambao wanachaguliwa na wananchi kama zamani na wawe wamehitimu kidato cha nne. Wakati wa kukaa, kama ni miaka tano, akichaguliwa pamoja na Councillor naye aende kwa wananchi atafute tena, kama ni mzuri, apewe tena arudi.

Mishahara ya madiwani: Mishahara ya madiwani isiwe inaangaliwa na district, iwe mishahara inapeanwa na Serikali Kuu. Kwa sababu vile nao madiwani hawana mishahara, ni kwa sababu inarudishwa katika area zao. Zingine zina pesa, zingine hawana. Kwa hivyo iwe, Central Government ndiyo inatoa mishahara ya madiwani.

Mahakama: Mahakama iwe na wazee wa kuangalia ya kwamba huyu mtu amekuwa namna gani. Mahakama iwe na wazee wa kuangalia wale watu. Kama mahakama ya hapa kwetu ni kwanzia hapa wakazalia ya kwamba, huyu mtoto kweli hajafanya hivi, amedhulumiwa, hawezi kuwa namna hii. Kwa sababu wengine ni (inaudible) na mtu anataka Councillor apate ile kitu ambayo si haki.

Jela ya Kenya iangaliwe kwa sababu si kama wanadamu wanaenda ile jela ni kama wanyama. Iangaliwe. Kwa sababu yule mtu hata kukosa kwake ni nini kubwa sana. Kwa hivyo aangaliwe apate pahali mzuri, akule pahali mzuri na aende kazi. Kwa hivyo jela za Kenya ziangaliwe.

Hospitali: Hospitali iwe ya bure katika nchi ya Kenya. Mazingira yetu ama zile rasilimali Mungu alitupa. Serikali inakuja, inakuja kuchukua kama maji haya ya Loitokitok, haisaidii sisi wenyeji na sisi tulipewa na Mungu, sasa inaenda kusaidia watu wawili au watatu. Kwa hivyo kila kabila ikae na mali yao walipewa na Mungu. Kama ni mawe iwe sisi tunaangalia. Kama ni maji iangalie na tutoshereke lakini si kuja kuchukuliwa kupelekwa pahali pengine.

Wanyama wa pori: Wanyama wa pori katika Serikali iliyoko, ni heri mnyama kuliko binadamu. Ni heri mnyama kuliko binadamu na sisi kutoka tuzaliwe, sisi Wa-Maasai tunakaa na wanayama kwa miaka hii yote na wanyama ndio sababu iko nchi ya wanyama. Wanyama katika nchi yetu. Kwa hivyo tunataka, zile tunalipwa, si chini ya shilingi elfu mia tatu. Tunataka tulipwe kama vile sisi tunalipa (inaudible). Kwa sababu sisi mtu, tunalipa ng'ombe arobaini na sita, ukiwa Maasai ukifika. Na sisi tulipwe, tupewe ya kwamba, mnyama zamani kwa sababu tulikuwa tunakaa na nini...ikikosea hivi, tunalipwa nini. Sisi tupewe hilo jukumu la kuamua. Serikali irundi huko ituulize, mnataka pesa ngapi.

Mambo ya matangazo ya KBC katika Kenya. Inakuwa ni ya chama moja na tuko katika nchi ambayo iko vyama vingi. Hakuna kitu ambacho inasaidia kwa matangazo katika vyama vingine. Itakuwa ni ya chama moja. Kwa hivyo tunaonelea ya kwamba KBC irudi kuwa Kampuni. Isiwe inahusika na Serikali ile iliyoko. Iwe inajisimamia na itangaze na ifanye biashara. Nafikiri yangu

imefikia hapo.

**Com. Lethome:** Mtu akiuliwa na mnyama alipwe na K.W.S.

**Philip Mosot:** Ilipwe na K.W.S. kwa sababu ni Serikali.

**Com. Lethome:** Na sasa umesema, unataka Tsavo na Amboseli irudi kwa Wa-Maasai. Kwa hivyo iwe ni ya Wa-Maasai?

**Philip Mosot:** Ya Wa-Maasai.

**Com. Lethome:** Sasa ikiwa ni yao, ikiwaua nani atawalipa?

